BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

2016 - 2020

1.	**Mhe. Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe. Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe. Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe. Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe. Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe. Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe. Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe. Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**

9.	**Mhe. Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe. Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe. Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe. Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais**
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na**

			Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**

31.	**Mhe.**	**Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe.**	**Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe.**	**Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**

54.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem **-** **Katibu**

Kikao cha Sita – Tarehe 16 Mei, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Zubeir Ali Maulid) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 228

Uondoshaji wa Taka katika Wilaya ya Magharibi "B"

Mhe. Ali Suleiman Ali - Aliuliza:

Mkoa wa Mjini Magharibi uliwakabidhi Mabaraza ya Shehia vifaa kwa ajili ya kufanya usafi katika shehia zao. Tatizo kubwa lililojitokeza katika majaa mbali mbali hasa Magharibi "B" ni kukosekana kwa magari ya kuzolea taka katika majaa hayo. Kwa kuwa tatizo la taka katika majaa mbali mbali ni kero na pia ni hatarishi kwa maradhi ya mripuko.

Je, Wizara itachukua hatua gani ili kuziondoa taka hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake Nam. 228 kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba Mkoa wa Mjini Magharibi na hasa Manispaa ya Magharibi "B" unakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa magari ya kukusanyia taka. Kwa kutambua changamoto hiyo, mkoa unaendelea na operesheni maalum ya pamoja kwa manispaa zote ya kuondosha mrundikano wa taka. Operesheni hiyo iliyoanza tarehe 4 Mei itaendelea katika kipindi chote hiki cha mvua kama hatua ya dharura ya kunusuru jamii yetu na maradhi ya mripuko.

Mhe. Spika, pamoja na hatua hizo za dharura, mkoa katika mwaka ujao wa fedha umetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari makubwa ya kuzolea taka taka pamoja na kijiko.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, pamoja na jibu zuri la Mhe. Naibu Waziri la kusema kwamba kuna mpango wa kupatikana magari huko mbele baada ya bajeti hii swali langu la nyongeza liko hapa.

Kwa kuwa mpango wa bajeti utaendelea lakini kwa kuwa taka zinazaliwa siku hadi siku ukiacha siku za mvua za kuondoa maradhi zile siku za kawaida wana mpango gani wa kuendelea au kuwa endelevu wa kuzoa taka hizi kabla hayo magari hayajafika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuendelea kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mhe. Ali Suleiman Ali kama ifuatavyo. Ni kweli kama ambavyo nimesema kwamba tunaendelea na *operation* hiyo katika kipindi hichi cha mvua, lakini naomba niseme Mhe. Spika, kwa kuliambia Baraza lako Tukufu kwamba shughuli au jukumu la kuweka usafi katika miji yetu ya Unguja na Pemba ni dhamana ya Manispaa zetu. Hivyo, hatuna budi kwamba kila tunapoona kuna haja ya kufanya *operation* kama hizo kwa hali za kawaida tutaendelea na juhudi zetu zile zile ambazo tumekuwa tukizipanga, lakini suala la usafi ni jukumu letu kuhakikisha kwamba usafi unadumu wakati wote. Hivyo basi, manispaa zetu zitaendelea kuhakikisha kwamba mji huu unakuwa salama ili kukinga hiyo miripuko au uchafu katika maeneo yetu ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniona na mimi na kunipa nafasi. Kutokana na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, mradi huu wa uzoaji wa taka katika Mkoa wa Mjini Magharibi walipewa vijana wa Mabaraza ya Vijana ya Shehia na kwa bahati nzuri kazi zao walizifanya vizuri na hatimae kutokea mfadhili wa vifaa kama visaidizi katika shughuli zao. Mhe. Waziri nataka kujua kwanini shughuli hizo wamenyan'ganywa vijana wa Zanzibar na kuweza kuzipeleka katika Baraza la Manispaa moja moja.

(b) Je, kuna uzito gani wa kuwapatia vifaa vile ambavyo wamekabidhiwa hadharani na kuweza kuendeleza kazi zao. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuendelea kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli hivi karibuni Ofisi ya Rais kupitia mikoa yetu au manispaa zetu iliweza kutangaza fursa za ajira kwa vijana 3,630 ambao lengo lake ni kuhakikisha kwamba hawa wanafanya kazi za usafi. Lakini pamoja na hayo, kuna tatizo ambalo tumeliainisha hapa suala la ukosefu wa vitendea kazi ikiwemo magari ni changamoto kubwa hata vijana hawa ambao tumewapa hizo kazi ambao hatujawanyang'anya kama ambavyo labda imezungumzwa. Lakini kutokana na hali taka zinakusanywa lakini hatimae hazipelekwi kule ambako zinatakiwa zipelekwe katika maeneo ya kutupia taka taka. Sasa kutokana na hali hii zoezi hili limekuwa likisuasua ambalo ndio limepelekea malalamiko makubwa na kurundikana kwa shehena za taka taka katika maeneo yetu ambayo imelazimika kuchukuliwa hatua za dharura za kufanya *operation* kama hizo ambazo nimeweza kuzielezea. Kwa hiyo, nimfahamishe kuwa hatuna nia ya

kuwazuia vijana kufanyakazi hiyo, lakini tu mkumbuke kwamba jukumu hili la kufanya usafi lazima lisimamiwe na manispaa husika. Hivyo basi, pale tutakapoona mambo yamekaa vizuri tulishapata hizo nyenzo nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba taratibu za kufanya ili kwamba vijana wetu waweze kufanya kazi ile kwa usimamizi mahiri na makini kwani manispaa zetu ziweze kuendelea.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri basi niulize swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi ulifanya uzinduzi wa mradi huu wa ukusanyaji wa taka kwa kuwatumia Mabaraza ya Vijana lakini tatizo kubwa Mhe. Waziri anasema ni nyenzo na bahati nzuri walimwita Mhe. Rais.

(a) Nini kiliwasukuma mpaka kuanzisha mradi huu ikiwa bado hawana nyenzo za kutosha kwa ajili ya shehia zote za Mkoa wa Mjini Magharibi.

(b) Lakini kutokana na kadhia ya taka ambazo zimo mitaani hivi sasa unawaahidi nini wananchi wa shehia mbali mbali za Mjini Magharibi kuweza kuondokana na tatizo hilo kutokana na adha ambayo ipo hivi sasa. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuendelea kumjibu Mhe. Rashid Makame Shamsi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Spika, naomba nikiri kwamba mrundikano wa taka kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tuliuona umezagaa sana katika maeneo yetu na ndio tukalazimika kufanya *operation* hizo.

(b) Lakini kuhusu ahadi kwa wananchi naomba niwahakikishie kwamba jukumu la kuendelea kufanya usafi katika maeneo hayo liko chini ya mikono ya manispaa husika. Lakini kubwa zaidi naomba tuitumie fursa hii kutoa wito kwa wananchi watoe mashirikiano, nako kuna tatizo kubwa kumekosekana mashirikiano makubwa jambo ambalo wananchi utaratibu wa kuziweka taka hizo katika *site* ambazo zinakubalika hawafanyi na badala yake manispaa zetu zinatumia muda mwingi kutoa taaluma na kufuatiliana kulikokuwa hakumaliziki. Hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe, kupitia Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, Waheshimiwa kwa kila mmoja anakaa kwenye Manispaa na Halmashauri zetu watusaidie kuelimisha wananchi wetu kujenga utamaduni ule wa kufuata sheria bila ya shuruti ili kusudi tusaidie katika kufanikisha malengo ya serikali.

Lakini kitu ambacho Mhe. Spika, kimetusukuma, hakuna kitu ambacho kimetu-*force* tulifika wakati tukaona kwamba haja na muda umefika katika kuona makundi haya ya vijana yanaweza yakatusaidia katika kukamilisha hii azma ya kufanya usafi katika maeneo yetu. Lakini kubwa zaidi ni kwamba Waheshimiwa tunapokuwepo katika shughuli hizi mambo mengi tunafikiria ni lipi tunaweza tukalifanya ambalo linaweza likasaidia katika urahisishaji zaidi. Lakini bado tukubali na hao vijana ambao

tunawatetea sisi tutaendelea kuwa nao na tutafanya hatua kwa hatua kama ulivyosema, lakini kubwa zaidi tuone nao pia wanachangamoto zao, kuna miongoni mwao wanajaza mikataba lakini kufanya hizo kazi ndio hao miongoni mwao wanaokwenda kutupa taka sehemu ambazo si rasmi. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kutoa majibu ya ziada au ya nyongeza badala ya yale aliyotoa Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mwanana kabisa ambayo ameyatoa jambo ambalo lilisukuma Mkoa wa Mjini Magharibi kuwashajihisha vijana ni lile suala la vijana wengi kuwa hawana kazi za kufanya. Lakini kama mnavyojua kwamba serikali inapofanya jambo inabidi lazima ifuatilie na ifanye tathmini, tathmini ndio iliyotusukuma tukaona kwamba zoezi hili linahitaji kupangwa vizuri zaidi ili lisije likaleta madhara. Mhe. Spika, sote ni mashahidi kwamba Wawakilishi wengi waliochangia bajeti yetu wamezungumzia suala la mrundikano wa taka na suala hili kwa sababu vijana waliojiajiri kuchukua taka wanachukua taka na kuzitupa pahala popote pale bila ya kuzingatia na kuzipeleka katika majaa ambayo yamekusudiwa zipelekwe halafu yaende magari yakachukue kupeleka jaa kuu Kibele.

Kwa msingi huo basi, sisi tukaona ni vizuri zoezi hili likafanyiwa tathmini na likaratibiwa vizuri ili tutakapolianza tuwe tunafanya mambo yote mawili, kwanza tusafishe mji wetu, lakini vile vile na vijana wetu wapate nafasi ya kuweza kujiajiri kwa kujipatia kipato. Kwa hiyo, kilichopo sasa ni kwamba tumesimamisha zoezi hili na hasa baada ya kutokezea baadhi ya vijana na baadhi ya watu wengine kuona kwamba jukumu hili ni la kwao kwa hiyo wakaanza kupanga bei kwa wananchi kinyume na utaratibu. Sisi kama serikali tunapoona tatizo hilo lazima tuchukue hatua ya kufanya tathmini na kulisimamisha zoezi hili ili litakapokuja kuanza lianze kwa utaratibu mzuri kwa maslahi ya wananchi wote wa manispaa zetu au wananchi wote wa Zanzibar. Ahsante sana.

Nam. 6

Tathmini ya Utendaji kazi kwa Watendaji wa SMZ baada ya Kupandishwa kwa Kima cha Chini cha Mshahara

Mhe. Shehe Hamad Mattar - Aliuliza:

Kwa kuwa Wizara yako ina kitengo cha ufuatiliaji na tahmini katika Taasisi za Serikali.

(a) Je, tokea Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi apandishe kima cha chini cha mishahara na kufikia shilingi 300,000/- ni tathmini ya kiwango gani imefanyika baada ya kupandishwa mishahara juu ya utendaji wa kazi katika ofisi za Serikali hapa Zanzibar.

(b) Je, ni Taasisi ngapi imeweza kuzipitia kwa lengo la kukagua na kuona na kuthamini uwajibikaji kwa watumishi wa umma.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake Nam. 6 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kwanza kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein imekuwa ikifanya juhudi mbali mbali katika kushughulikia maslahi ya watumishi ikiwemo kupandisha kima cha mshahara kila hali inaporuhusu kwa lengo la kuimarisha utendaji na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi na jamii kwa ujumla. Katika kufanikisha hili, Serikali ya Awamu ya Saba imefanya marekebisho na kuimarisha maslahi kwa vipindi tofauti.

Mhe. Spika, mnamo mwaka 2011, serikali hii ya awamu ya saba imefanya marekebisho kwa kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka Tshs. 100,000/= hadi Tshs. 125,000/= sawa na ongezeko la asilimia 25, mwaka 2013 serikali imepandisha tena kima cha chini cha mshahara kutoka Tshs. 125,000/=hadi Tshs. 150,000/= sawa na ongezeko la asilimia 20.

Mhe. Spika, serikali hii hii ya awamu ya saba katika mwaka 2014 ilifanya mazingatio maalum kwa watumishi wenye uzoefu wa kuanzia miaka 15 na kuendelea na ambao wana mishahara baina ya Tshs. 150,000/= mpaka 225,00/= na mwaka 2015 serikali imerekebisha tena mishahara kwa wenye kiwango cha elimu cha Stashahada ya Kawaida *(Ordinary Diploma)* na wenye uzoefu wa kazi kuanzia miaka 15 kwa kupandisha nyongeza mbili ya tatu (2/3) ya uzoefu wa utumishi wao. Aidha, mwezi Aprili, 2017 marekebisho ya watumishi yalifanyika ambapo kima cha chini cha mshahara kimepanda kwa asilimia mia moja kutoka Tshs. 150,000/= mpaka Tshs. 300,000/= jambo ambalo limeongeza ari, ubora na ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma. Mabadiliko haya ya mshahara yanakwenda sambamba na marekebisho ya posho mbali mbali zinazohusu watumishi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, kwa kawaida tathmini ya utendaji kazi ni zoezi ambalo linafanywa kila baada ya kipindi fulani. Kwa upande wa Utumishi wa Umma, inatakiwa mtumishi kufanyiwa tathmini kila mwaka kwa kupimwa utendaji, nidhamu na ufanisi wake wakati anapotekeleza majukumu yake ya kazi. Mtumishi anapofanyiwa tathmini na kufaulu hupelekea kupata tunzo, kupewa nyongeza ya mshahara au kupandishwa cheo baada ya kukitumikia cheo chake cha awali kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu. Hata hivyo, naomba ieleweke kwamba utaratibu huu wa kiutumishi haujakamilika na kwa hivyo bado haujaanza kutumika rasmi. Ofisi Kuu ya Utumishi imetayarisha Muongozo na Fomu za

Upimaji Utendaji Kazi ambazo tayari zimeshawasilishwa kwa Makatibu Wakuu kwa ajili ya kupitiwa, kupata maoni na hatimae kuruhusiwa kutumika rasmi na Wizara na Idara zetu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ). Nje ya utaratibu huu wa kupima mtendaji mmoja mmoja, Tathmini ya Utendaji wa Kazi imekuwa ikifanyika kwa utaratibu wa kuwasilisha Mpango Kazi na kupitia utekelezaji halisi wa Taasisi za Umma (Bango Kitita) kwa kila robo mwaka. Viashiria vinaonesha kwamba utendaji kazi wa Taasisi za Umma umekuwa ukiongezeka siku hadi siku na huduma zinazotolewa na Taasisi zetu zinaimarika.

(b) Mhe. Spika, kwa sasa utaratibu wa tathmini ya utendaji kazi kwa kutumia utaratibu wa kupima mtumishi mmoja mmoja bado haujaanza kutekelezwa na Taasisi za Umma, utaratibu huo unatarajiwa kuanza kutumika rasmi baada ya Muongozo wa Upimaji Utendaji Kazi *(Performance Appraisal)* kuidhinishwa rasmi Serikalini. Nashukuru ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mhe. Naibu Waziri marefu lakini yenye kuonekana ni mazuri na nina swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Pamoja na kuwa serikali ilikuwa na nia ya kuinyanyua mishahara ya wafanyakazi lakini bado kuna wafanyakazi mishahara yao ilipunguzwa. Je, ni kwa nini.

(b) Pamoja na kuonesha kwamba mishahara kuanzia mwaka 2014 iliongezeka kwa njia mbali mbali kupitia vipengele mbali mbali. Je, Mhe. Waziri anajua kwamba Mabaraza ya Mji Wete, Chake Chake na Mkoani Pemba hadi leo wana madai ya *arrears* zao za mabadiliko haya ya mishahara hayajalipwa lenye thamani ya 123,144,000/- anafahamu hivi. Na kwa sababu yeye mwenyewe wizara yake ilitoa barua kwenda Wizara ya Fedha iliyopata kutoka Tawala za Mikoa kudai malimbikizo hayo hadi leo haijatoka taarifa yoyote wafanyakazi hawa wanadai malipo yao.

Je, ni lini malipo haya yatafanyika kupatikana wafanyakazi hawa wengine wakiwa wameshakufa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, katika suala la upandishaji wa mishahara vigezo mbali mbali huwa vinaangaliwa na pale ambapo panapotokea mapungufu au pale ambapo panapotokea kasoro basi afisi yetu huwa tunakaribisha malalamiko yoyote yaletwe kwetu ili tuweze kuyafanyia kazi. Kwa taarifa tu Mhe. Spika, tulivyokuwa tukibadilisha hii mishahara mapungufu na kasoro zilijitokeza na wale wote ambao waliokuwa wakidai kwa namna mmoja au nyengine mishahara yao ilipungua basi tuliweza kuwafanyia hiyo kazi.

Sasa nitoe wito kama kuna taasisi yoyote ikiwemo Baraza la Wete au Mabaraza mengine, kama kuna Taasisi yoyote, Idara yoyote, Wizara yoyote wafanyakazi wao katika haya mabadiliko ya mishahara ambayo tuliyokuwa tukifanya kutoka miaka hiyo hadi mwaka huu wa 2017, basi tunawaomba wafanyakazi hao kwa kupitia viongozi wao waje wizarani na tunahakikisha kwamba yale yote mapungufu ambayo yamejitokeza kama kawaida yetu tutawashughulikia na tutahakikisha kwamba kila mfanyakazi anapata ile haki yake ambayo anastahiki kwa mujibu wa Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011 na vile vile kwa mujibu wa kanuni zetu za Utumishi wa Umma za mwaka 2014. Ahsante.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri yenye kuleta sura nzuri katika kuwatetea wananchi au wafanyakazi kwa ujumla.

a) Mhe. Waziri ulisema kama wapo wafanyakazi au taasisi waje wizarani, lakini ipo taasisi ambayo ni Mamlaka ya Maji Zanzibar *(ZAWA)* wameshakuja na kilio hiki na ule wajibu ambao ulisema waje wizarani kwako, basi lile lalamiko serikalini lipo kwa mpaka sasa wanaishi na mshahara ambao wa kima kile cha zamani sio kima cha sasa. Je, kwa kuwa wao wameshafika sio wale ambao waje katika taasisi yako, ni lini serikali itakamilisha suala hili ili na wao wapate haki zinazostahiki kama lile agizo la serikali la kupandishwa mshahara lilivyotoka hapo awali.

b) Kwa kuwa agizo lilitoka kipindi kirefu je, watakapokamilishiwa huo utaratibu wa kufuata kupata haki zao litaanza sasa au litaanza pale wenzao walipopandishwa na kupata haki zao za msingi. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika majibu yangu mama na majibu yangu ya nyongeza ambayo niliyoulizwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar ni kwamba, kama kuna changamoto zozote katika marekebisho yoyote tuliyoyafanya ya mishahara, basi taasisi, idara au wizara husika ilete malalamiko hayo na tutaendelea kuyashughulikia kama ambavyo tunafanya.

Sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa amezungumza suala la Mamlaka ya Maji Zanzibar (*ZAWA*). Mhe. Spika, niseme kwamba kama Mamlaka ya Maji ikiwa ni miongoni mwa taasisi ambazo wanaona kwamba maslahi yao hayajakaa sawa sawa ya mishahara basi ni vyema wakaja, na kama wamekuja tuelewe kwamba shughuli hizi zinahitaji muda. Kwa maana ya kwamba sio suala la kukurupuka lazima tuweze kuangalia na ile hali ambayo ipo kwa maana kwamba tusije tukafanya tena kosa lile lile la kutokea mapungufu katika taasisi mbali mbali ikiwemo kama ulivyoeleza ile mamlaka ya *ZAWA*.

Kwa hivyo, kama wamekuja suala lao bado wanaendelea kushughulikiwa na tunaamini baada ya muda mfupi kama ulivyotaka swali la (b) ni lini baada ya muda mfupi suala hilo litakaa sawa. Usiwe na wasi wasi Mhe. Miraji Khamis Mussa naamini kwamba miongoni mwa watu hawa

pengine ni mwananchi wako wa jimbo lako, kwa hivyo usiwe na wasi wasi kama limekuja tutalishughulikia na tutahakikisha kwamba wanapata haki yao kama vile ambavyo wanapata haki wafanyakazi wengine wa idara au taasisi au wizara nyengine. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka nimuulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa suala la upandishaji wa mishahara linakwenda sambamba na sekta binafsi na sekta binafsi nyingi zimeonekana zinavunja utaratibu wa kisheria katika kupandisha mishahara kwa waajiriwa wao, na kwa kuwa wanaoajiriwa mara nyingi wanajenga hofu ya kuondoshwa katika kazi zao katika kudai haki zao.

Je, Wizara yako ina mikakati gani au mipango gani ya kuhakikisha sekta binafsi wanaendana na taratibu za kisheria katika upandishaji wa mishahara nchi hii.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri majibu kwa ufupi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya taasisi binafsi zimekuwa wagumu katika suala la upandishaji wa mishahara kama ambavyo serikali ilivyoagiza.

Mhe. Spika, niseme kwamba kwa wale wote ambao watakaoendelea kupinga amri hii ya serikali ya kuwapandishia mishahara …

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tusikilizane kidogo. Mheshimiwa samahani, Waheshimiwa Wajumbe tusikilizane kidogo nimepata *notice* kutoka kwenye mitambo inayorikodi *hansard* kuna tatizo la muingiliano mkubwa sana wa sauti zenu, kwa hiyo kama mnanong'ona kidogo sauti ziwe chini. Mhe. Waziri malizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nikiendelea na kumjibu Mhe. Ali Salum Haji ni kweli yapo malalamiko kwamba baadhi ya taasisi binafsi wanakuwa hawalipi ipasavyo mishahara kama vile ambavyo serikali ilivyoagiza. Lakini niwakumbushe kwamba serikali ipo na ikifikia hatua kuna kipindi cha ustahamilivu, lakini ifikie hatua kwamba tutaendelea kuwabana na tutahakikisha kwamba wale wote ambao hawajapatiwa mishahara yao kwa kile kipindi ambacho serikali imetoa tamko lile basi wahusika hao tutawalazimisha walipe wale wafanyakazi wao kile kiwango ambacho wanachodaiwa.

Nam. 40

Utoaji wa Mikopo na Kucheleweshwa kwa Mikopo ya Elimu ya Juu hasa Vyuo vya Nje ya Zanzibar

Mhe. Ali Khamis Bakar - Aliuliza**:**

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wapya na wa zamani ambapo jumla ya wanafunzi wapya 1,461 wamefungishwa mikataba ya mkopo kwa mwaka 2017/2018 na wanafunzi 2,582 wanaoendelea wamefanyiwa malipo.

(a) Je, ni sababu gani zilizopelekea kusitishwa mikopo kwa elimu ya juu kwa wafanyakazi wa Serikali wanaojiendeleza.

(b) Je, ni lini tatizo la ufinyu wa jengo la Ofisi ya Bodi ya Mikopo litatatuliwa.

(c) Je, ni sababu zipi zilizopelekea kucheleweshwa kwa fedha kwa baadhi ya wanafunzi walioomba mkopo hasa kutoka vyuo vya nje ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwalikilishi swali lake Nam. 40 lenye vifungu (a), (b) na (c). Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar imetoa mikopo kwa wanafunzi 1,461 katika mwaka 2017/2018 na wanafunzi 2,582 wanaoendelea wamepatiwa mikopo. Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu kama hivi ifuatavyo:-

(a) Serikali imesitisha mikopo kwa waombaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wafanyakazi kwa ajili ya kutoa nafasi zaidi za kujiendeleza kwa vijana wanaomaliza skuli na ambao hawana ajira. Serikali ilizitaka Taasisi au waajiri kuwasomesha wafanyakazi wao ili Bodi ya Mikopo iwahudumie wanafunzi tu ambao idadi yao imekuwa ikiongezeka kwa kasi. Hata hivyo, hivi sasa Serikali inafikiria kurejesha mikopo ya elimu ya juu kwa wafanyakazi wake kwa zile fani ambazo zina mahitaji makubwa kwa maendeleo ya nchi. Fani hizo ni kama vile Mafuta na Gesi, Udaktari, na Wataalamu wa Matumizi ya Vifaa vya Afya (mf. *CT Scan*), Wahandisi, na Walimu wa Sayansi na Hisabati.

(b) Wizara inakusudia kuandaa mchoro wa jengo ambalo litaingiza taasisi mbali mbali za elimu ikiwemo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ambayo hivi sasa ofisi zake ni ndogo na hazikidhi mahitaji ya chombo hicho.

(c) Ni kweli baadhi ya wanafunzi wanachelewa kupata fedha za mikopo ya elimu ya juu kutokana na wao wenyewe kuchelewa kukamilisha taratibu za mikopo. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, wanafunzi wote waliokamilisha taratibu zao tayari wameshalipwa malipo ya ada kwa vyuo vya ndani na nje ya nchi. Aidha, wanafunzi kumi (10) tu wanaosoma katika vyuo vya China waliochelewa kuingiziwa fedha zao kutokana na uandishi wa majina yao kutofautiana na akaunti zao. Ahsante.

Mhe. Ali Mohamed Bakari: Ahsante sana Mhe. Spika pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize suala la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni lini mchoro huu utaandaliwa na pahala gani jengo hilo litajengwa.

(b) Jengo hilo linatarajiwa kugharimu kiasi gani na kila taasisi itachangia kiasi gani. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:**
Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kwamba hivi sasa wataalam wanaandaa mchoro huo na sehemu ambayo itajengwa ni sehemu ile katika ofisi ya Wizara ya Elimu tunayo maeneo pale ndio ofisi hizi zitakuwepo. Hatuwezi kusema gharama kwa sababu mchoro ndio unaamua gharama, mpaka hapo mchoro utakapokamilika gharama tutaweza kuijua. Ahsante.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe Spika, kwanza nimsifu Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

(a) Katika majibu yake amesema kwamba serikali imezitaka taasisi na waajiri kuwasomesha wafanyakazi wao ili kuwapa nafasi zaidi vijana katika kusoma katika elimu ya juu. Je, ni wafanyakazi wangapi ambao wamekosa mikopo hiyo.

(b) Hakuna wafanyakazi ambao wanasoma kada hizi muhimu za mafuta na gesi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Ni kwamba tulisema msingi ilionekana ni busara kwa Bodi ya Mikopo kushughulikia wanafunzi na wafanyakazi wahudumiwe katika taasisi yao. Lakini katika kipindi hichi kifupi serikali ikagundua kwamba taasisi na wizara hazikujipanga kuwasomesha wafanyakazi wake na ndio maana ikaamua vyenginevyo kwamba ni vyema pia na wafanyakazi nao pia wakasomeshwa kupitia Bodi ya Mikopo baada ya kipindi cha mwaka mmoja kutathmini matokeo yakawa sio mazuri.

Hata hivyo, ni kwamba katika Bodi ya Mikopo wanafuata vigezo vya masharti vilivyowekwa na serikali vya vipaumbele, iwe ni mfanyakazi wa serikali au mwanafunzi kuna vigezo vilivyowekwa na Tume ya Mipango Zanzibar, kuna *priority* namba I, II na III hivi ndivyo ambavyo vinatumika hivi sasa na vinaendelea kutumika hapo baadae. Ahsante sana.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Spika, lakini nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Ila Mhe. Naibu Waziri katika jitihada za serikali za kuwasomesha vijana wetu hawa kuna posho zimetajwa kwenye kanuni ile ya Bodi ya Mikopo kama posho la *reaserch* na posho la *field*, mpaka muda huu tunavyozungumza hili limeondolewa kabisa na ni muhimu sana kwa wanafunzi wetu pale ambapo serikali inawasomesha.

a) Je, ni lini serikali itarejesha posho hili kwa kuwapatia maana kwenye kanuni limetajwa.

b) Kwa vile posho hili la kawaida la kujikimu pia limepitwa na wakati maana muda mrefu linatumika posho la aina moja lakini halikidhi katika maisha ya sasa. Je, ni lini serikali

itafikia kuongeza posho hili ili wanafunzi wetu waendelee kusoma bila ya changamoto ambazo zinawakabili katika kujikimu kimaisha katika masomo yao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa maswali yake kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba katika kanuni masuala haya yametajwa na wakati ambao hali ya kifedha itaruhusu jambo hili tutalifanyia kazi na posho nyengine nazo pia zinaweza zikapatiwa lakini hii itategemea pia na uwezo wa serikali utakapokuwepo.

Kuhusu posho la kujikimu ni kweli kulingana na hali halisi halikidhi vya kutosha nalo pia serikali italifanyia utafiti na pale hali itakapokuwa nzuri basi na wao pia watafikiriwa kufanyiwa mageuzi na wakati wowote serikali iko *sensitive* kusikiliza mahitaji ya watu. Ahsante sana.

Nam. 223

Mchango wa Madawati Nchini

Mhe. Ali Suleiman Ali (Jimbo la Kijitoupele) - Aliuliza:

Kwa nia njema kabisa, Serikali imewahamasisha viongozi na wananchi kuchangia madeski kwa ajili ya kuondoa tatizo la wanafunzi kukaa chini wakati wa masomo. Kwa kuwa serikali iliunda kamati kwa ajili ya kukusanya michango mbali mbali nchini.

Je, Mhe. Waziri, ni kiasi gani cha fedha kimepatikana hadi hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 223 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein aliunda kamati ya kukusanya michango ya fedha kwa ajili ya kuondoa tatizo la madawati katika skuli zetu. Pia, Mhe. Rais alizindua harambee ya kitaifa ya kukusanya michango hiyo na wananchi, wafanyabiashara, mashirika na watu mbali mbali waliitikia harambee hiyo na kutoa michango yao. Mpaka kufikia Mei, 2018 jumla ya TZS 1,342,709,581/- zimekusanywa. Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wale wote waliochangia na pia napenda kutoa wito kwa wengine kuendelea kutoa michango yao. Ahsante sana.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, kwanza nampongeza kwa dhati Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona kwamba umefika wakati tutoke kule tuliko tuingie katika karne ya kileo au wakati wa sasa. Mhe. Spika, kwa kuwa serikali ilifanya bidii kamati yetu hii naipongeza kwa kukusanya shilingi 1,342,709,581/-. Je, ni madawati mangapi yamepatikana hadi sasa.

b) Ni fedha kiasi gani zilizotumika kwa ajili ya madawati hayo ambayo yametangulia.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kwamba hadi sasa tunatarajia kupata si madawati lakini viti na meza thalathini elfu na mia tatu ambazo zitagharimu US$ 1,293,979 na hizi zitapatikana kutokana na kupatikana mzabuni kutoka China ambaye ataifanya kazi hii kwa gharama hizo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya serikali juu ya kadhia nzima ya suala la madawati tukumbuke katika Baraza lako hili tukufu katika miaka hiyo iliyopita ilipitisha tozo kwa msafiri atakayetumia bandari yetu ya Zanzibar kulipa shilingi elfu moja kwa kila *trip* kwa ajili ya kuchangia madawati. Je, zile fedha zote ni kiasi gani zilizopatikana hadi sasa pamoja na hesabu aliyopiga Mhe. Waziri aliyozungumza pale itakayogharimu dola milioni moja na *something.* Kuna tofauti ya kiasi gani hadi sasa hata sisi wawakilishi tumechangia fedha zile, madawati katika majimbo yetu atakwenda vipi. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba pesa zilizokusanywa katika harambee na zile ambazo anaziita ada ya bandari pale tumeweza kupata shilingi bilioni 1,429,237,421/- hizi zimekusanywa kutoka ada ya bandari zinachanganishwa na hizi tunaweza hivyo viti na meza tulivyosema. Ahsante.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini pia nataka kabla ya swali langu naomba niwapongeze kwa dhati wale ambao wamechangia madawati kwa njia moja au nyengine. Lakini nataka kujua hadi muda huu ni skuli ngapi za Unguja na Pemba zilizofaidika na madawati hayo na je, bado kuna mahitaji ya kiasi gani ili kuweza kukidhi haja ili wanafunzi wetu waweze kupata madawati ya kutosha katika maskuli yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Kuhusu ugawaji wa madawati Wizara ya Elimu haina takwimu za kutosha kwa sababu wagawaji wa madawati haya huwa wakati mwengine wanakwenda katika skuli moja kwa moja, wakati mwengine wanapitia halmashuri. Kwa hivyo, hatuna taarifa moja kwa moja anaweza kwenda mwananchi na mwananchi akapeleka madawati yake matano katika skuli fulani na hiyo ndio hali halisi na tulikemea kipindi fulani kwamba haya madawati yanayotolewa katika maskuli ni vyema Wizara Elimu ikawa na taarifa zake. Kwa hivyo, hatuna taarifa kuhusu jambo hilo.

Lakini ni kwamba mpaka tunafanya takwimu zetu tulikuwa na upungufu wa vikalio 1,187,790. Ahsante sana.

Nam. 128

Tatizo la Kuwapa Mimba Wasichana Wadogo

Mhe. Suleiman Sarahan Said (Jimbo la Chake Chake) - Aliuliza:

Nashukuru sana Mhe. Spika na mimi kwa asubuhi hii umeungana na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote na kumtakia kheri Mtume wetu Muhammad *(SAW).* Naomba swali langu Nam. 128 lijibiwe.

Pamoja na Serikali kuweka mifumo ya kulinda haki za wanawake na watoto, kumekuwa na tatizo la wanawake wanapopewa mimba nje ya ndoa na wanaume wanaowapa mimba kuwatelekeza wao pamoja na watoto na kuwaachia ulezi wa watoto hao.

a) Je, kwa nini mama ndio anaachiwa alee mtoto peke yake.

b) Kwa kuwa mtoto aliyezaliwa na mama ambaye hakuolewa kwa mujibu wa dini ya kiislamu mtoto huyo hana haki ya kumrithi baba huyo, Je, Serikali pia hakuna haki ya mtoto yule kumrithi baba aliyempa mwanamke ujauzito.

c) Katika nchi au maeneo mengine watoto kama hao huenda Mahakamani na kudai haki zao na kulipwa haki zao. Vipi hapa Zanzibar utaratibu huo upo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto - Alijibu**:**

Mhe. Spika, awali ya yote naomba niendelee kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma ambaye na yeye anaendelea kutupa pumzi zake na asubuhi hii tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako tukufu tukiwa wazima na wenye afya njema.

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali kwa ruhusa yako naomba uniruhusu niweze kusema machache.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwatakia waislamu wote duniani Ramadhan njema hususan wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba Mwenyezi Mungu *in shaa Allah* atupokelee saumu zetu na atujaalie amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, sasa kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 128 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kiutaratibu mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa analelewa na mama na ni mtoto wa mama peke yake. Kwa upande wa huduma za mtoto mama anaweza akadai huduma ya matunzo ya mtoto Mahakamani kupitia Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011 na Sheria ya Kumlinda Mwari na Mtoto wa upande mmoja ya mwaka 2005 ambayo katika kifungu cha 8 (1) kinaeleza kuwa mtu yeyote aliyethibitika au anayedaiwa kuwa baba wa mtoto

kumhudumia mtoto huyo kwa kutoa huduma zote za lazima zikiwemo mavazi, chakula, elimu na makaazi kwa mujibu wa uwezo wa baba. Kifungu hicho kinafafanua kuwa baada ya kuwa amethibitishwa na Mahakama kuwa ni baba wa kibaiolojia.

b) Kwa upande wa Serikali hakuna haki ya mtoto kumrithi baba aliyempa mwanamke ujauzito nje ya ndoa, Sheria ya Mirathi Zanzibar inaongozwa kwa misingi ya Dini ya Kiislamu. Hivyo, zinakataza mirathi kwa mtoto wa mazingira hayo. Hayo ni kwa mujibu wa Sheria ya Kadhi ya mwaka 1985.

c) Hapana utaratibu wa aina hiyo kwa Zanzibar kwa sababu sheria za mirathi zinaongozwa na misingi ya kiislamu.

Mhe. Spika, lakini mwisho napenda nitoe wito kwa wanawake wale wanoambiwa wanaotaka kuolewa waache kufanya haraka ya kufunga ndoa. Ni vizuri Mhe. Spika, ukafanya utafiti kwanza hii ndio inapelekea madai ya kwamba Mhe. Mwakilishi analolisema ni kuwasemea watoto hawa na kuwadaia haki zao. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru sana Mhe. Spika na mimi nimshukuru sana Waziri kwa nyongeza ya majibu. Mhe. Spika, kuna watoto wa aina mbili ambao tunao katika mitaa lakini kuna kauli inayosema hakuna mwana asiye baba yake kila ntu ana baba. Hawa watoto Mhe. Spika, tunaosema wa nje ya ndoa ndio wanaoleta sasa matatizo kwa sababu wengi wao wanakosa huduma hasa upande wa baba. Serikali yetu ya Zanzibar katika maelekezo yake inasema haina dini kwamba inachukulia haki zaidi kuliko hata dini, sasa hawa watoto waliokuwa wanazaliwa nje ya ndoa bado serikali haijawapa kipaumbele cha kuwa haki yao itapatikana wapi.

Mhe. Spika, sasa nilikuwa nasema mambo kama haya yameshatokea Dar es Salaam juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam akawaita wanawake wote wenye watoto wakaweza kutambua baba zao. Mimi hapa ningeshauri hawa waheshimiwa wakaanza kukuletea kimemo na mimi nimo ili tukapunguza haya matatizo kabla Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini pengine hapa hajaweza kufanya kama hayo.

a) Mhe. Spika, lakini niulize je, haoni Mhe. Waziri kuna haja ya kutunga sheria ambayo itaweza kutoa haki kwa mtoto ikiwa mtoto yule atazalishwa na akajulikana kwamba kuwe na kifungo au kuwe na faini ambayo itaweza kumlinda mtoto yule katika maisha yake mpaka atimie umri wa miaka kumi na nane.

b) Mtoto halali Mhe. Waziri ni yupi katika serikali, ni yule anayefanana na wewe au yule aliyekuwa anazaliwa kwenye ndoa. Sasa kuna wengine anarithi lakini hakufanana na baba yake yule mtoto halali au vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi amesema tutunge sheria ambayo itaweza kufanya yule mtoto ambaye amezaliwa nje ya ndoa kuweza kupata haki zake. Naomba nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba licha ya kutunga sheria wizara yangu ina utaratibu ambao watoto hao waliozaliwa nje ya ndoa ikiwa wana matatizo wazee wao hufika pale na tukaweza kukaa na pande zote mbili tukaweza kufahamiana.

Lakini swali lake la pili anasema mtoto wa halali anayetambulika ni yule aliyefanana na baba au mama. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba mtoto wa halali ni yule ambaye wazee wake wamefunga ndoa kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi.

Mhe. Spika, katika kesi hizi za utelekezaji watoto katika maeneo mengi yanayoongoza ni ya pwani na hasa wale ambao wanakwenda dago.

Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri katika ziara zetu na yeye ni shahidi tumekuta wanawake wengi wakilalamika kuhusiana na kesi zinazowakuta katika ndoa zao na sana sana kwa kuweza kuwaachia kundi kubwa la watoto na hatimaye kuhangaika na watoto wao. Je, wizara inachukua hatua gani ya kuweza kuwafikia na kuwaelimisha wanawake wale ile kuondokana na mzigo huu ambao wanaachiwa na wanaume.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli katika sehemu walizozitaja mazingira haya yapo, lakini naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi kwa jumla kwamba wanawake hawa wanaofikwa na kadhia hii ni vizuri kufika ofisini kwetu kujieleza matatizo yao. Lakini na sisi kama wizara tutafanya makusudi kuwafikia mama wale na kuweza kuwaelekeza dhidi ya kutatua matatizo haya yanayowakabili. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 28

Utaratibu wa Kutayarisha Vitambulisho vya Umiliki wa Matumizi ya Ardhi za Eka Zanzibar

Mhe. Mussa Foum Mussa (Jimbo la Kiwani) - Aliuliza**:**

Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati kupitia Kamisheni ya Ardhi katika mwaka 2017/2018 ilipanga kutayarisha vitambulisho 60 vya umiliki wa matumizi ya ardhi za eka tatu tatu.

a) Je, Waziri hili unalifahamu.
b) Je, limefikia katika utekelezaji gani.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 28 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, swali la kutoa vitambulisho 60 vya umiliki wa matumizi ya ardhi kwa ardhi za eka tatu nalifahamu na linafahamika na Kamisheni ya Ardhi ambayo ndio inasimamia suala hilo na maendeleo yake yanaripotiwa katika vikao mbali mbali vya Wizara na Serikali. Vitambulisho hivi vinatolewa kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa masharti yanayotolewa katika upewaji wa ardhi hizo na pia kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo hayo ya eka Tatu.

b) Mhe. Spika, vitambulisho 45 kwa ajili ya wananchi waliopatiwa ardhi za eka tatu vilitayarishwa na kukabidhiwa wenyewe, kati ya vitambulisho 60 vilivyopangwa kutayarishwa, hii ikiwa ni sawa na asilimia 75 ya shabaha iliyopangwa.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Waziri lengo lenu lilikuwa ni kutoa vitambulisho 60 na mmetoa vitambulisho 45 tu. Je, vitambulisho hivyo vilitolewa katika wilaya gani na je, hivi 15 havikutolewa kwa nini.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Vitambulisho hivi vinatolewa kwa mujibu na utaratibu, havitolewi tu kwamba tumepanga malengo basi tuvitoe. Kwa hiyo, inabidi mhusika aombe watu waombe vijadiliwe kwenye vikao mbali mbali na katika maeneo mbali mbali kutoka kwa Sheha kupitia kwa Mkuu wa Wilaya, maombi yale yakija yanatafakariwa ndani ya vikao na hapo ndipo vinapofanyiwa kazi.

Hatuwezi kutoa vitambulisho ambavyo hatimae baadae vikaleta migogoro kwa sababu tu ya kukidhi mahitaji ya namba ambayo tumeipanga.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa hapa lililozungumzwa ni swali la eka tatu na kwamba idadi ya eka tatu zilizopo ni nyingi karibu elfu nne na ambazo zimeripotiwa kwamba zimefanyiwa uhakiki zipo kwa sasa hivi. Je, ni utaratibu unaotumika gani wa hizi eka ambazo zinatakiwa zipewe vitambulisho kwa wale watu waliokuwa navyo na lini utaratibu huu utaanza kwa ajili ya hao watu walioguswa na kutengenezewa vitambulisho hivyo kutoka mwaka jana na mwaka huu. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Kwanza ni kweli eka zipo nyingi lakini utoaji wa vitambulisho kama nilivyosema awali unatolewa baada ya kufuatia maombi. Waliopewa eka tatu hairithiwi moja kwa moja, kwa hiyo kama mtu atakuwa ametangulia mbele ya haki maana yake watoto lazima waombe na watafuata taratibu za mirathi.

Lakini hata kama hana wa kumrithi eka ile inarudi serikalini na yule atakayetaka kuitumia inabidi aiombe na hatimaye ndio tunafikia hayo malengo ambayo tumekuwa tunayapanga. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kama tunavyofahamu kwamba eka hizi zilitolewa baada tu ya kupatikana uhuru wa nchi yetu lakini sasa hivi inaonekana kwamba wamiliki wengi wao tayari wameshatangulia mbele ya haki na kuna utaratibu kwamba watoto ndio ambao wanaomba ile hati kwa ajili ya kurithi tena. Je, kwa wale ambao bado hawajafanya hayo maombi na hizi tatu zinafahamika kwamba zipi wizara imepokea eka ngapi ambazo tayari zipo wizarani na wanazifahamu kwa wale ambao hawajaomba na wale ambao wameshatangulia mbele ya haki ni eka ngapi ambazo zipo tayari zimesharipotiwa. Je, kuna utaratibu gani wa kuzitoa tena kwa ajili ya wananchi ambao sasa hivi wapo ambao ni maskini na hawana uwezo wa kumiliki au kununua ardhi ya aina yoyote. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hidaya Ali Makame swali lake nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kwa mujibu wa utoaji wa eka mtu anayetaka eka lazima aombe haiji *automatic* lazima aombe na anapofanya maombi, maombi yale yanakwenda kwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Wilaya anatuandikia kama kutakuwa na eneo ambalo ameliomba *specific* basi kama liko tupu na anastahiki kupewa lakini pia kama ana vigezo vya kupewa hiyo eka.

Lakini pia kwa wale ambao bado wazee wao wamekufa na hawajarithishwa yale maeka tunaendelea kutoa elimu kwa sababu eka hurithishwi isipokuwa eka unaiomba, unapoiomba kama mzee wako ametangulia mbele ya haki unafahamishwa taratibu. Unaomba kwa Mkuu wa Wilaya lakini Sheha anathibitisha hatua nyengine za kisheria zinafuata na hatimaye unaweza kupewa zile eka.

Lakini pia inawezekana eka nyengine zikawa tupu labda hakuna warithi au zimerudi serikalini kwa njia moja au nyengine basi mwananchi yeyote sasa anaruhusiwa kuomba na aka-*identify* lile eneo na akaweza kupewa ile eka. Naomba kuwasilisha.

Nam. 103

Kampuni ya Ukaguzi wa Magari Zanzibar yaliyopo Nje ya Nchi

Mhe. Omar Seif Abeid (Jimbo la Konde) - Aliu1iza**:**

Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako kufanya marekebisho ya swali langu kidogo kabla ya kupatiwa jibu. Nilikuwa naomba lisomeke na liingie kwenye *hansard* kwa kuwa Kampuni ya Jabal Hira ya Kilimanjaro iliyopo Dubai iliingia mkataba na Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar kupitia taasisi za viwango kwa ajili ya kufanya *inspection* ya magari na vitu vyengine kwa ajili ya matumizi.

Baada ya marekebisho hayo naomba swali langu Nam.103 lijibiwe.

Nam. 103

Kampuni ya Ukaguzi wa Magari Zanzibar yaliyopo Nje ya Nchi

Mhe. Omar Seif Abeid – Aliuliza:

Kwa kuwa Kampuni ya Jabal Kilimanjaro iliyopo Dubai imeingia mkataba na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia taasisi ya viwango, ambapo miongoni mwa majukumu ya kampuni hiyo ni kufanya ukaguzi kwa magari yanayoingia Zanzibar kutoka nchi kama Uingereza, Japan, Hong Kong, Ghana na nyenginezo.

(a) Je, katika nchi hizo wapo mawakala wao wanaofanya *inspection* ya magari na vitu vyengine kwa ajili ya matumizi kabla ya kusafirishwa kuletwa Zanzibar na kama zipo kampuni hizo zinaitwaje na afisi zao ziko wapi kwenye nchi zao.

(b) Je, *ZBS* huwa wanachukua hatua gani kwa wafanyabiashara ambao wanakwepa kufanyiwa ukaguzi *(inspection)* ya magari kabla ya kuingiza hapa nchini.

(c) Je, magari yanayoruhusiwa kuingizwa nchini hivi sasa yanatakiwa yawe ya miaka mingapi kutumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu:

Mhe. Spika, kwanza naomba fursa hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima, lakini pili kuwatakia kheri waislamu wote duniani kwa kuanza kufunga mwezi mtukufu wa Ramadhan, wengine wameanza leo na wengine wanaanza kesho na wengine kesho kutwa.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 103 lenye vifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, nitaanza kwa kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS*) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Nam.1 ya 2011. Jukumu la kuanzishwa kwa taasisi hii ni kuandaa viwango pamoja na kusimamia matumizi ya viwango hivyo.

Mhe. Spika, *ZBS* imeanza utekelezaji wa ukaguzi wa magari kwa kutumia *Used Motor Vehicles* zinazoingizwa nchini kutoka nje ya nchi kwa kupitia mifumo miwili ya ukaguzi wa bidhaa hizo ambazo ni:-

- *Pre-Export Verification of Conformity to Standards* (*PVoC*) ambayo bidhaa hukaguliwa nje ya nchi kabla ya kusafirishwa na kuingizwa nchini.

- *Destination Inspection* (*DI*) ambapo bidhaa hukaguliwa baada ya kufikia nchini na kabla ya kungia nchini kwa matumizi.

Mhe. Spika, ukaguzi wa gari unaotumika kupitia mifumo yote miwili ulianza rasmi tarehe 01/08/2016. Kwa kutumia mfumo wa *PVoC, ZBS* imesaini mikataba na mawakala wawili kwa ajili ya kufanya kazi za ukaguzi wa magari kwa niaba ya *ZBS* nje ya nchi. Mawakala wenyewe ni:-

1. *East Africa Auto Mobile Company LTD* – ambayo makao makuu yake yapo nchini Japan, hufanya kazi za ukaguzi wa magari yote yanayotoka Japan, Uingereza, Hong Kong na Singapore.

2. Jabal Kilimanjaro *Auto Electrical Mech* – ambayo makao makuu yake yapo Mjini Sharjah katika Falme ya Kiarabu, hufanya kazi ya ukaguzi kwa gari zote zinazotoka Dubai.

Mhe. Spika, idadi ya wakala hawa wa ukaguzi inaweza kuongezeka kwa kila itakapohitajika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Katika nchi za Uingereza, Japan, Hong Kong, yupo wakala ambaye anafanya kazi ya ukaguzi ambaye ni Kampuni ya *East Africa Auto Mobile Company LTD*. Anuwani zao zipo zinapatikana katika tovuti ya *ZBS* ambayo ni www.zbs.go.tz. katika nchi ya Ghana mpaka sasa *ZBS* haina wakala wa ukaguzi wa gari hayo.

(b) Kwa waingizaji wa gari ambao hufanya ukaguzi wa gari zao nje ya nchi, kulipa gharama za ukaguzi na gari zao kukaguliwa kupitia mfumo wa *Destination Inspection*.

(c) Katika muongozo kuhusu gari zilizotumika huandaliwa na *ZBS*, kuhusu gari zilizotumika haujaweka mipaka ya miaka iliyotumika kwa gari zinazoingizwa nchini. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo moja kasema kwamba hakuna utaratibu wa miaka maalum ya magari kuingia Zanzibar. Lakini napenda kumuuliza swali.

Kwa kuwa na sisi Zanzibar ni nchi inayoendana na ulimwengu wa kileo wenzetu wote wameshaweka muda maalum wa kuingiza magari nchini mwao ili kuzuia kuingiza magari chakavu na bidhaa chakavu, sisi hapa Zanzibar tumeziona bidhaa chakavu na baadhi ya magari chakavu yanashushwa tunayaona.

Je, ni lini utaratibu wa kuweka muda maalum wa bidhaa kama magari ambayo yametengenezwa kuingizwa nchini ili kuzuia bidhaa chakavu zisiingie Zanzibar sambamba na vifaa vya matumizi ambavyo tunaviona vinaingia Zanzibar. Ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kwanza napenda kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwanza naomba tuipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuleta sheria Nam.1 ya 2011 ambayo imeweka Taasisi ya Viwango. Madhumuni ya taasisi hii ni kuhakikisha sasa Zanzibar tunaondokana na ule uzamani wa kutumia, kula na kufanya mambo yote ya vitu visivyo na viwango. Sasa Serikali ya Awamu ya Saba ya Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein imeweka Taasisi ya Viwango, na taasisi hii imeanza kufanya kazi sana.

Mhe. Spika, kwanza si kila nchi ambayo imeweka kwamba gari chakavu zisiingie, baadhi ya nchi bado gari chakavu zinaingia ikiwemo Zanzibar. Lakini kwa kusaidia *TRA* kama utaleta gari iliyozidi miaka 10 wao wana-*charge* pesa zaidi za uchakavu, na hiyo ndio *system* inayotumika kwa nchi nyingi duniani. Hata Uingereza, Marekani, Canada utakapopeleka gari zilizozidi umri fulani wana-*charge*, Kenya wao wameweka miaka minane, sisi tumeweka kumi kupitia *TRA*. Kwa hiyo, mheshimiwa hilo linafanyika. Mheshimiwa ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri chini ya Makamu wake ambaye alikuwa bosi wake Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii na ndio kwanza nimuone mara yangu ya mwanzo kujibu swali leo hapa mbele hayo ni matunda ya kamati mheshimiwa. Vile vile alikuwa na ahadi ya kuwatetea wakulima na wakwezi. Je, msimamo ule uko pale pale au tena baada ya kwishakupata fungu limeongezeka.

a) Mhe. Spika, swali langu ni kwamba unanunua gari Japan unapewa *certificate* na *TBS*, ikishakufika hapa gari ile *ZBC* ambayo iko chini ya wizara yako inakuwa na kigugumizi siku tatu au nne *certificate* ile wanairejesha tena Dar es Salaam. Je, huoni kama unacheleweshe wateja. Halafu vile vile kuna mali hapa Zanzibar kwenye makontena zinakaguliwa na *food drugs*, mali hiyo hiyo na *ZBS*. Hamuoni mnamkung'uta mfanyabiashara kwa kumuumiza huku na huku.

b) Kampuni ya Jabal Kilimanjaro ina mkataba wa miaka mingapi na muda wake unamaliza muda gani na kutafuta kampuni nyengine inachukua utaratibu wa kutangaza *tender* au ana-*renew* tu mkataba ule ule.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi aliyekuwa Mjumbe wa Kamati moja mimi na yeye, kwanza nimepokea shukrani zako.

Mhe. Spika, *ZBS* tumeingia mikataba na nchi mbali mbali nje ya nchi, ukiwa Japan, Uingereza, Dubai gari yako inakaguliwa na zile taasisi ambazo tumeingia nazo mikataba, na kama hujakaguliwa ikija hapa gari yako itakaguliwa. Sasa unauliza kwa nini kule ishakaguliwa na hapa

inakuja kukaguliwa. Mhe. Spika, naomba kumwambia *yes we have to* kwa sababu dunia imeongezeka kuna *fake* nyingi inawezekana mtu aka-*fake document* kwa hivyo tunafanya kitu kinaitwa *verification*, *we have to verify* kwamba hii *document* kweli imetoka katika taasisi yetu kule Japana au Uingereza au Dubai. Kwa hivyo, hicho lazima tuendelee kukifanya ni kuonesha umakini wa taasisi yetu kwamba sasa umefika wakati Zanzibar itumie vitu vyote ambavyo vina viwango.

Pili, Mhe. Spika wakala kwenye majibu yangu nimesema mkataba tulionao na taasisi hizi ni mikataba ya miaka miwili miwili. Kwa maana hiyo, tuna mkataba wa miaka miwili na hiyo Kampuni ya Kilimanjaro iliyokuwepo Dubai. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu mheshimiwa.

Mhe. Spika: Hapana mheshimiwa mlikuwa kamati moja akirudi utakaa nae mtafahamiana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa kuniona pamoja na majibu ya serikali yenye mchecheto naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kuwa tunao mkataba wa miaka miwili kwa kampuni ile ya kutekeleza viwango nilikuwa nataka kujua ni *process* gani ilipitia ya kufanyiwa *tender* na kampuni gani zilibidi ili kuipata ile Kampuni ya Kilimanjaro.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Kwanza nataka kumwambia majibu ya serikali hasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huwa hayana mchecheto.

Pili, nataka kumwambia kwamba kuna sheria ya kuzipata hizi kampuni kwa mujibu wa Sheria ya Tender ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nataka kumuhakikishia tulitumia sheria hiyo inayoongoza jinsi gani mtampata huyo mtu wa kuweza kuwa Nam.1. Kwa hiyo, sheria ilitumika na *tender* ilitolewa na huyo Kilimanjaro ndio aliyekuwa wa mwanzo na tulimu-*award* hiyo *tender* kufanya kazi hiyo kwa kipindi cha miaka miwili kwa mujibu wa mkataba wetu. Ahsante Mhe. Spika.

Nam. 94

Ukosefu wa Usafiri wa Uhakika katika Maeneo ya Chwaka na Kiwani

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:

Kwa kuwa eneo la Chwaka Kiwani ni sehemu ambayo wananchi wake ni wakulima na wazalishaji mazao ambayo kupeleka Chake Chake na Mkoani huku wakilazimika kutumia magari ya ng'ombe na punda.

(a) Je, serikali itawasaidia vipi wananchi hao kutokana na ukosefu wa usafiri wa uhakika wa kusafirisha mazao.

(b) Ni lini utafanya ziara ya kwenda kuiona barabara hiyo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, watu wa Chwaka - Kiwani wanapata usumbufu wa kupeleka mizigo yao sokoni kutokana na matatizo makubwa ya kupeleka mazao yao Mkoani au Chake Chake. Lakini si muda mrefu tatizo hilo litapatiwa ufumbuzi na mradi mpya wa barabara ya Ole/Kengeja unaopita katika eneo lao na tegemeo la serikali kwamba utakuwa ndio suluhisho la tatizo la wananchi wanaoishi katika eneo hilo, kwani barabara hiyo imepita karibu sana na eneo hilo.

Mhe. Spika, ili wakulima hao wapate ufanisi katika kilimo chao wanahitaji miundombinu ya barabara ya uhakika ili kupeleka sokoni mazao yao Mkoani au Chake Chake.

Kutokana na sababu hiyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshapitisha maamuzi ya kulipatia ufumbuzi tatizo hilo na muda si mrefu mradi wa barabara ya Ole/Kengeja unaopita katika eno lao utatekelezwa. Tegemeo la serikali ni kwamba itakuwa ndio suluhisho la tatizo la wananchi wanaoishi katika eneo hilo, kwani barabara hiyo imepita karibu sana na eneo hilo.

Mhe. Spika, kwa vile mheshimiwa kaniomba niende nitawanye barabara yao tukimaliza tu Baraza nitakuwa na ziara ya Pemba basi nitaiweka kwenye ratiba *inshaallah*.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo majibu haya yamenipa matumaini kwa wananchi ambao nimepakana nao katika Jimbo langu la Chwaka-Kiwani. Lakini naomba pia nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa barabara hii ya Ole-Kengeja imepakana na barabara nyingi ambazo ziko karibu sana ikiwemo barabara ya Dodo kuelekea Kibarini, barabara ya Kichanjaani kuelekea Mtakamaji. Je, Mhe. Waziri na barabara hizi nazo zitatengenezwa na mradi huu wa barabara ya Ole-Kengeja au barabara hizi ziko katika Tawala za Mikoa. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza. Mhe. Spika, kama nilivyosema Pemba sina uzoefu nayo sana na sijaenda kuzunguka katika hayo maeneo, ziara nitaifanya lakini kama yenyewe iko katika barabara kubwa basi barabara hizo zitatengenezwa na sisi, lah kama hizo ni barabara za michepuko za ndani ya Wilaya husika basi hizo zitatengenenzwa na Tawala za Mikoa. Sasa kwa nini siwezi kusema kwa sababu sina uhakika sizijui zilipo.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Waziri wananchi wa Kipange, Miwani, Kinumoshi wote asilimia kubwa ni wakulima ambao wanajishughulisha sana na mazao wanauza sokoni hasa marikiti ya Mwanakwerekwe na Shimoni wananchi hawa nao huwa wanahangaika sana kuhusu

suala la usafiri, hususan kipindi kama hiki cha mvua kutokana na ubovu wa barabara iliyopo Miwani-Kizimbani mpaka Bumbwisudi.

Je, Mhe. Waziri unawaambia nini wananchi hawa wa Miwani, Tomokani, Kizimbani mpaka Bumbwisudi kuhusu suala upatikanaji sahihi wa usafirishaji wa mazao yao kutokana na ufinyu au ubovu wa barabara ile iliyopo pale zaidi ya miaka 50 sasa hivi haijatengenezwa. Ahsante.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri samahani, Mhe. Mwakilishi hebu lilete kwa maandishi swali linaonekiana jipya japo linagusa barabara lakini eneo ambalo liliulizwa kwenye swali la msingi sio hili ambalo unatoa *detail* hizi. Sasa swali lako lingekuwa zuri sana kama likija kwa maandishi.

Nam. 196

Kukosekana kwa Mawasiliano ya Simu za Mkononi

Mhe. Machano Othman Said – Aliuliza:

Kwa muda mrefu wananchi wa vijiji vya Mwakaje, Mwachealale, Kitundu, Bumbwisudi na Mkanyageni katika Manispaa ya Magharibi "A" wamekuwa wakikabiliwa na tatizo la mawasiliano duni ya mitandao ya simu za mkononi, hivyo kusababisha kudorora kwa huduma muhimu za jamii katika maeneo hayo.

(a) Je, kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu ni sababu gani zinazopelekea kuwepo kwa tatizo hilo katika maeneo hayo.

(b) Kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo wanapata tabu sana ya mawasiliano Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Aliuliza:

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nakushukuru kwa kunipa fursa yakuweza kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 196 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, maeneo yaliyotajwa kweli yanakabiliwa na tatizo la mawasiliano duni ya mitandao ya simu za mkononi. Kwa kujua hivyo, wizara kwa kushirikiana na wataalamu wa mtandao wa simu za mkononi wamefanya ukaguzi katika maeneo tajwa kwa lengo la kujua sababu iliyopelekea matatizo hayo.

Mhe.Spika, baada ya kufanywa uchunguzi wa kiteknolojia na iligundulika kuwa minara mingi iliyopo karibu na maeneo hayo, haikuwa na nguvu za kutosha kufikisha mawasiliano na hivyo kutengeza mashimo (*holes*) ya mawasiliano, kwa lugha nyengine mawasiliano yake ni dhaifu (*signal weak)*, hivyo ndio sababu kubwa iliyopelekea matatizo hayo katika maeneo hayo.

(b) Mhe. Spika, kwa upande wa Kampuni ya Zantel, tayari kazi imeshaanza na kuzidisha nguvu (*optimization*) katika minara 35 ya Unguja na Pemba ambayo iliyogundulika kuwa na uhaba huo wa nguvu za mawasiliano, na tatizo hilo kwa kiasi kikubwa limetatuka. Mfano, ikiwemo minara ya Kombeni, Ndagaa na Kizimbani. Na ili kutatua tatizo hili kwa ujumla wake juzi tu tarehe 13/5/2018 Bodi ya Mfuko wa Mawasiliano katika wizara yetu wakafanya kikao na kwa sehemu ambazo mtandao haupatikani. Kuhakikisha kwamba nchi nzima mawasiliano yapatikane na kama kuna tatizo sehemu, wao watajenga minara na na zile kampuni zote zenye kuhusika na mawasiliano wataweza kuekewa antena zao na watazilipia.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kama lilivyo swali langu la msingi kwamba wananchi wa Mwakaje, Mwachealale, Bumbwisudi, Kitundu na Mkanyageni ambao ni wa majimbo ya Mfenesini na Bububu wamekuwa na tatizo hili kwa muda mrefu la mawasiliano ya simu. Na kwa kuwa wananchi hawa nao pia ni wananchi wa Zanzibar na wanahitaji huduma hii. Je, ni minara ya eneo gani ambayo yataimarishwa, minara ya karibu ili wananchi hawa nao waweze kupata huduma hizo za simu kama kawaida.

b) Pamoja na kwamba Bodi ya Mawasiliano imekutana juzi tarehe 13/05/2018 na kuamua hayo waliyoamua. Je, Mhe. Waziri anaweza kuwaahidi wananchi hawa wa Wilaya mpya ya Magharibi ‘A’ kwamba serikali itafanya juhudi za makusudi kujenga mnara mpya katika maeneo hayo ili kuweza kumaliza tatizo hili.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Spika, majibu yatakuwa ni yale yale, tatizo tunalijua na sehemu tunazijua. Bodi iliyokuja imekuja kutatua tatizo hilo kwa nchi nzima sio kwa Zanzibar tu Unguja na Pemba, bali kwa Tanzania nzima. Kwa hivyo, ni mategemeo yangu kwamba tatizo litatatuka nchi nzima na sio tu Magharibi hiyo anayoisema yeye.

Nam. 117

Kupambana na Maradhi mbali mbali Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Katika kupambana na majanga ya maradhi mbali mbali yaliyojitokeza katika visiwa vyetu vya Zanzibar, yapo maradhi yanayotibika na yasiyotibika, lakini mengine huhitaji mgonjwa kupata kufanyiwa matibabu kila wiki, mwezi au miezi mitatu au sita hasa usafishaji damu kwa wagonjwa wa figo (*dialysis*).

(a) Je, serikali imejipangaje katika suala la kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo ambao hupata tabu na gharama kubwa kwenda Bara kutafuta huduma hiyo.

(b) Je, kwa sasa huduma hiyo kwa Zanzibar inapatikana katika hospitali gani.

(c) Je, serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma hizo katika Hospitali za Wilaya au za Mikoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika ahsante, kwa ruhusa yako naomba kwanza uniruhusu niseme mambo machache kwa manufaa ya taifa letu.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri na Ramadhani njema Wazanzibari wote, pia kuwakumbusha kufuata kanuni za afya kwa kudumisha usafi katika mazingira yetu ili kuepuka maradhi ya miripuko yanayosababishwa na uchafu hususan katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani yakiwemo maradhi ya kipindupindu. *Insha Alla* Mola atupe wepesi kutekeleza hayo.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 117 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali hili naomba nichukue fursa hii kupongeza juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein za kuimarisha huduma za afya kwa kiwango kikubwa, pamoja na kusimamia utekelezaji wake katika hospitali zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, naomba kujibu swali la (a) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kuona usumbufu mkubwa unaowapata wananchi kwa kufuata huduma za usafishaji wa damu kwa wagonjwa wa figo (*Dialysis*), nje ya kisiwa cha Zanzibar, iliiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha inajipanga haraka iwezekanavyo ili kutoa huduma za usafishaji wa damu kwa wagonjwa wa figo angalau huduma hizo zianzie katika hospitali moja yoyote Unguja na Pemba ili kuwapunguzia gharama pamoja na usumbufu wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo.

(b) Huduma hii ya usafishaji wa damu kwa wagonjwa wa figo (*Dialysis*) kwa Zanziabr na katika hospitali katiak huduma za serikali inapatikana katika hospitali ya Mnazi Mmoja pekee.

(c) Lengo la wizara yangu ni kutekeleza kwa vitendo agizo hili la serikali kwa kufikisha huduma ya usafishaji wa damu kwa wagonjwa wa figo kwa ukaribu zaidi, angalau katika kiwango cha hospitali za Mkoa, mara mahitaji muhimu ya huduma hii yatakapokamilika. Kwa sasa tunawaomba wananchi waendelee kuiamini serikali yao na kuitumia Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja kwa kupata huduma hii na bila ya malipo yoyote.

Mhe. Spika, hudumahii pia inapatikana katika baadhi ya hospitali binafsi kwa malipo ya shilingi 250,000 na mgonjwa anahitaji kufanyiwa usafi wa huduma hii angalau mara mbili kwa wiki. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Spika, nashukuru sana na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya ufafanuzi, mojawapo likiwa ni kwamba huduma hii ni huduma muhimu sana kwa mgonjwa anayepata matatizo ya figo.

Lakini la pili, huwa ni uhai wake akisafishwa damu, lakini la pili alilosema ni kima kikubwa cha pesa ambacho kinampatia mtu katika hospitali zile ambazo ni za *private* na serikali na serikali niishukuru sana kulijua suala hili na kuweza kutekeleza. Lakini suala la kwanza ambalo ni (a) zipo kauli kwamba maradhi haya ya figo hasa Kisiwani Pemba yamejitokeza kwa sana. Sijui Mhe. Naibu Waziri atanambia ni kweli au si kweli, kama ni kweli ni sababu zipi zinazofanya mpaka hawa watu wanaokaa Pemba wakapata tatizo hili.

Suala la pili, kwa sababu wana nia njema ya kututekelezeana kupunguza gharama au kutuondoshea kabisa matatizo haya, Kisiwa cha Unguja na Pemba ni mbali na gharama. Je ni lini ataleta kipimo hiki cha usafishaji wa damu katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza enye (a) na (b) kama ifuatavyo. Mheshimiwa hatujafanya utafiti wa kutosha tukagundua kwamba maradhi haya kisiwa cha Pemba yako sana, lakini anatushauri na tutalichukua hili tulifanyie utafiti baadae tutatoa kwamba kweli Pemba wanaathirika zaidi na maradhi haya na kama wanaathirika ni kwa nini.

Pili, katika jibu langu la msingi nilijibu kwamba agizo la serikali ni kupeleka huduma hii katika hospitali zote, lakini angalau wakatwambia kwa hatua za awali anzeni na hospitali moja yoyote Zanzibar nasi tukaanza na Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, lengo la Wizara yangu ya Afya ni kuhakikisha kwamba huduma hii inatembea angalau katika ngazi ya hospitali za mkoa.

Mhe. Spika, tumo katika kufanya mipango mbali mbali kwa sababu huduma hizi zina vifaa vingi vifaa ambavyo ni ghali na ni huduma maalum na wafanyakazi wake ni wafanyakazi maalum ambao wamesomeshwa katika fani hii. Kwa hivyo, tumo katika mipango ya kuhakikisha baadae tunaweza kuzisambaza huduma hizi angalau katika ngazi ya hospitali za mkoa. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Mhe. Spika, ahsante na mimi kuniruhusu kuuliza swali dogo al nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri mimi ningependa kujua tu, kwa sababu vifaa hivi vinavyofanya usafishaji huu wa damu vinagharimu pesa nyingi serikalini. Je, hawa wahudumu wanaofanya kazi hii wamepewa mafunzo. Kama wamepewa mafunzo nchi gani na kwa muda gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mheshimiwa naomba kumtoa wasiwasi Mhe. Mwakilishi kwamba, hawa wahudumu ni wahudumu maalumu ambao wamepata mafunzo ya kutosha, siwezi

kukwambia ni nchi gani kwa sababu sina uhakika, lakini wamepata mafunzo ya kutosha kuweza kutoa huduma katika kitengo hiki na wanajitahidi kutoa huduma zilizo bora kwa wagonjwa wetu. Kwa siku moja wanawahudumia wagonjwa kuanzia 18 mpaka 20 bila ya matatizo yoyote. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, nami niungane na Mhe. Naibu Waziri kwanza kwa umakini wa Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein kuanzisha kitengo hiki. Nilikuwa nikisema na nitaendelea kusema mpaka dakika ya mwisho hata saa tisa za usiku ukiniamsha Dkt. Ali Mohamed Shein kafanya nini kwanza nitakwambia katika sekta ya afya, kwamba katika pahali alipojitahidi Mhe. Rais amejitahidi kwa kiwango kikubwa sana na watendaji wasiendelee kumuangusha.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Naibu Waziri katika kitengo hiki kilichoko Mnazi Mmoja (*dialysis*) kina changamoto. Je, anachukua muda gani kutembelea kuangalia kitengo hiki ambacho ndio hatua ya mwisho kwa mwanadamu. Kuna changamoto si moja, mbili, tatu, wala nne; anachukua muda gani kwenda kukitembelea kitengo hicho? Hilo la kwanza.
Pia ametaja kuwa huduma hii inapatikana katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tu pekee Pemba haijafika, najua huko mbele uhai wa Rais na Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na umri mrefu Dkt. Ali Mohamed Shein nafikiri na Pemba itafika. Ametaja Hospitali ya Mnazi Mmoja na hapa pana ahadi ya serikali kuhusu *lift* na kesho kutwa tunapitisha bajeti. Je, wamejipangaje ahadi ile ipo itatekelezwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, kitengo kile huwa nakitembelea karibu kila siku mara mbili na baadhi ya siku huwa sipati nafasi ya kutembelea. Lakini mara ya mwisho jaa niliingia katika kitengo kile mara mbili ili kuangalia hali inakwendaje na mapungufu niliyakuta kama kawaida ya mapungufu na niliyoyakuta nilichukua hatua za kuyatafutia *solution* na kwa wakati huu basi yanatekelezwa.

(b) Mheshimiwa nilikuwa namuomba Mhe. Mwakilishi arudie kidogo hili swali lake sikumsikia vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pana ahadi ya serikali hapa, suala hili alilolitaja la Mnazi Mmoja ndipo inapopatikana *dialysis.* Kwa hivyo, swali langu linaingia moja kwa moja hapa pana ahadi ya serikali kuwa *lift* itakuja, *lift* ile imekuwa mbovu siku moja alisema hapa alipanda usiku mimi nikasema nakwenda asubuhi, nikasema *lift* ile mbovu...

Mhe. Spika: Mheshimiwa uliza lile swali lako la pili.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tuna bajeti kesho kutwa je, pesa hizo zimetengwa kwa ajili ya *lift*.

Mhe. Spika: Mheshimiwa swali la *lift* usilijibu muache ajibu waziri mwenyewe.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana aliyoeleza, lakini nataka niongezee tu kwamba, hata mimi jana nilikuwa kwenye kitengo chetu ambacho kina *dialysis* na walikuwa na *shortage* kidogo ya dawa na bahati nzuri tukazungumza na *suppliers* na wakaleta dawa haraka sana na tunaendelea na matibabu kama kawaida.

Suala la *lift* tungoje tu bajeti tusiwe na wasi wasi. Kwa sasa hivi yale mawili yaliyokuwa mabovu moja linafanya kazi na jengine jipya tunategemea wakati wowote litaingia kuongeza yale yaliopo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wakati wa maswali umekwisha. Naam! Mhe. Hamza Hassan Juma kuhusu utaratibu.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa hii nafasi ya kutoa utaratibu, naomba kutumia kanuni ya 42 hoja ya kujadili jambo la dharura. Lakini kwa sababu ni mambo mengi sitaki kuyarejea, nafikiri wajumbe wote kanuni tunazo lakini nitaomba suala langu hili ikiwezekana serikali kama itakuwa ina majibu leo ni vizuri wakatutolea leo, lakini kama watakuwa hawana majibu leo basi nitaomba watumie kanuni ya 43 kuja kwa kauli ya serikali.

Mhe. Spika, hoja yangu ni kwamba, hivi karibuni ndani ya wiki hii tumepata taarifa kuwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) limevifutia Vyuo Vikuu karibu 11 kwa hapa Zanzibar. Katika vyuo hivyo vyuo vitatu ni vya serikali na vyuo vinane ni vya watu binafsi. Kwa kuokoa muda sina haja ya kuvitaja hapa lakini baadae nikitakiwa nivitaje kwa sababu orodha ninayo naweza nikavitaja.

Sasa hii kadhia kwa kweli imekuwa kubwa kwa sababu kwa kuwa vyuo hivi vimefutiwa usajili na sasa hivi kuna wanafunzi ambao walikuwa wanadahiliwa wameshazuiliwa, lakini pia kuna wanafunzi ambao walisoma katika vyuo hivi sasa hivi kwa kweli wapo katika taharuki kubwa sana. Sasa tunaomba kauli ya serikali katika hili ili kuweza kujua sasa. Je, hii kauli ya *NACTE* kanda ya Zanzibar serikali imeipata? Kama imeipata je, kuna kasoro gani na serikali itachukua hatua gani, *otherwise* kwa kweli wanafunzi wetu ambao wameshasoma katika hivi vyuo na kwa bahati mbaya vyuo hivi ni maarufu sana. Tulikuwa tunaomba kauli ya serikali kama kuna ufafanuzi tuweze kupata. Ahsante.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma hili jambo ulilolileta ni jambo muhimu kwa sababu linawagusa wananchi walio wengi na wengi wetu tuna watoto wetu katika hivyo vyuo mbali mbali. Sasa kwa sababu ya umuhimu wake nadhani serikali wamelichukua lakini ningekuomba Mheshimiwa uwape ile orodha pengine wao hawajaipata ya hivyo vyuo halafu baadae nitaruhusu serikali ije na kauli hapa Barazani ili wananchi wote waweze kusikia kinachoendelea kuhusiana na suala hilo.

Baada ya hapo Waheshimiwa nina tangazo la wageni, wageni wetu waliofika leo wa kwanza ni mgeni wa Mhe. Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Shehe Hamad Mattar. Mgeni mwenyewe ni Ndg. Maulid Khalid Juma ambaye ni *Co-ordinator* wa *Red Cross* kanda ya Pemba katika Mradi wa *LIFE***,** kama yupo naomba asimame. Karibu sana.

Mgeni anayefuata ni mgeni wa Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil, mgeni mwenyewe ni Mr. Runy Churtrin, ni mwekezaji kutoka nchini India. *You are most welcome in the House of Representatives*.

Wageni wanaofuata ni wageni wa Mhe. Hamza Hassan Juma jumla yao ni watu watano. Wa kwanza ni Mr. Craig Beeson *from* UK, *you are most welcome*. Wa pili, Mr. Salim Mohammed Al Busaid, *from* Oman, wa tatu Mr. Yahya Ahmed Al Hashmi, *from* Oman, wa nne ni Bwana Mbarouk Salim Mbarouk kutoka Zanzibar na wa tano ni Bwana Omar Talib Omar kutoka Zanzibar. Karibuni sana, karibuni Baraza la Wawakilishi.

Baada ya tangazo la wageni Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na uchangiaji wa hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini wachangiaji tulionao ni wengi sana, sasa nilikuwa nina ombi. Kwanza nitamtaka Mwenyekiti ambaye nitampisha sio muda mrefu ikiwezekana Waheshimiwa tukubaliane tuchangieni dakika 10 tuzipunguze zaidi kwa sababu ya wingi wa hawa waliyoomba. Lakini jengine katika wingi huo wamo na mawaziri wengi ambao wameomba kuchangia, nadhani katika kipindi hiki cha asubuhi tuwape *priority* Waheshimiwa Wajumbe angalau kwa dakika kumi, kumi waweze kuchangia, mawaziri wote tutakuja kuangalia ule muda na hawataweza kuchangia wote hata hawa wajumbe. Sidhani kama wote mtaweza kuchangia katika muda uliobakia. Kwa sababu lengo letu ni kuhitimisha hii hoja leo jioni. Sasa wajumbe tulionao kwenye *list* pamoja na mazingira ambayo tunakwenda nayo nilikuwa naomba sana waheshimiwa tujaribu kuchangia kwa yale mambo muhimu tu, ili kupunguza muda na ili waweze kupatikana wengi zaidi kuchangia.

Baada ya hayo naomba sasa nimwite Mwenyekiti wa Baraza ili aje achukue nafasi ili tuweze kuendelea tusipoteze muda mwingi zaidi. Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama tulivyomsikia Mhe. Spika kwamba muda wetu tumependekeza kuupunguza kwa ajili ya kuweza kuchangia watu wengi. Kwa hivyo,

tutafuata muda ambao amependekeza Mhe. Spika. Sasa naomba nimwite Mhe. Rashid Makame Shamsi akifuatiwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Bahati Khamis Kombo ajitayarishe.

Mhe. Rashid Makame Shamsi hayupo namwita Mhe. Suleiman Sarahan Said endelea.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasih ii na mimi kuchangia machache kutokana na hotuba hii ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri kwa kitabu chake kilichofafanua sana, ingawa ni kitabu kikubwa lakini muda wa kuongezea ni mdogo lakini tutakazia humo humo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na suala la Wakuu wa Mikoa. Wakuu wa Mikoa wote ni Wakuu wa Mikoa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkuu wa Kusini Pemba hawa wapo katika miji iliyokuwa ina mambo mengi sana na miji inajulikana ina vituo vyake sana. Lakini nataka nizungumzie kwamba Wakuu wa Mikoa hawa wameingia ndani zaidi kwa suala la makusudi la kupiga vita madawa ya kulevya na unyanyasaji wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Madawa ya Kulevya hakuna asiyelifahamu uzito wake. Sasa ningemuomba Waziri kwamba Wakuu wa Mikoa hawa ambao wamelipa kipaumbele sana suala la dawa za kulevya pamoja na unyanyasaji wa kijinsia. Lakini pia nataka nikwambie kwamba takwimu zinazoonesha katika masuala ya unyanyasaji wa kijinsia hizi sehemu za miji baina ya Mjini Magharibi na Mji wa Kusini Pemba takwimu ni ndogo sana. Takwimu zinaonesha zaidi ni maeneo ya Wete na maeneo mengine ya shamba yamefanya hivi, sijajua sababu gani iliyosababisha watu hawa lakini inaonekana pia zile sehemu za kupumzikia kule mashamba zinakuwa kidogo. Kwa hivyo, mawazo ya watu wengine yanawapeleka pahala palipokuwa sipo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba sana uongeze nguvu hawa viongozi wetu Wakuu wa Mikoa wa Mjini Magharibi pamoja na Kusini Pemba wameingia ndani zaidi katika masuala haya ya kujikita na dawa za kulevya na pia wakiwa katika miji. Kwa hivyo, ningeomba uwaongezee nguvu na ulinzi wa hali ya juu ili kupambana na mambo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la Mkuu wangu wa Wilaya ya Chake Chake. Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake alihamishwa katika nyumba kwa ajili ya matengenezo akawekwa katika kibanda cha *stand by* ili nyumba ile itengenezwe. Nyumba ile baada ya kutengenezwa imepata wenyewe sasa yeye mpaka leo amebakia mle mle kwenye kibanda kile. Sasa ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kile kibanda, maana sio nyumba ni kibanda hakiridhishi kumuweka Mkuu wa Wilaya mle anafanyakazi nyingi sana anafanyakazi katika jitihada kubwa sana lakini mazingira ya makaazi ni mazingira yaliyokuwa yanahitaji kuboreshwa sana.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua nchi yetu ni nchi ya joto na nchi yetu inahitaji mambo mengi lakini Mkuu wangu wa Wilaya kwa kweli bado hatumtendei haki. Mkuu wa Mkoa pia nae hana nyumba nzuri hivyo hivyo ambayo ya kufanyia kazi. Lakini basi ungefanya angalau jitihada Mhe. Waziri, Mkuu wa Wilaya ukamuhamishia kwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Mkoa

ukamtafutia eneo zuri zaidi hata kama la kukodi lakini ili mradi tukawawekea hadhi hasa kutokana na sifa zao na miji waliyonayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikupongeze sana Mhe. Waziri katika Mji wangu wa Chake Chake umeshafanya ziara sana na mimi mwenyewe ukinishirikisha na kwa kweli napata faraja sana unaponishirikisha kwa sababu tunajenga nchi yetu na tunajenga mji wetu. Nikuombe tena sina haja ya kusema mengi sana kwa sababu hayana haja ya kuzungumza sana. Lakini nakuomba tena ufanye ziara tena Pemba njoo tena tukae tuzunguke ili tuangalie taratibu ambazo zitatusaidia sana katika mji wetu ule wa Chake Chake. Mhe. Mwenyekiti, ni mji unaokuwa kwa kasi lakini bado mipangilio ya mipango miji inahitaji bado kukaliwa kitako na kuweza kushughulikiwa zaidi.

Mhe. Waziri wizara yako ina ugatuzi lakini bado huna eneo la kutosha katika Mji wa Chake Chake. Mimi ningekushauri sana bado tuna maeneo Chake Chake njoo tukague, njoo uweke eneo ambalo litahitaji kwamba shughuli zako na zana zako ambazo pengine zinaingia mpaka kwenye barabara wewe utakuwa na ma-*grader*, pengine utakuwa na vitu vingi ambavyo vitahitaji basi viwe na eneo. Na eneo lako liwe sio Afisi ya Baraza la Mji pale ambayo huna hata pahala pa kuweka gari iwe ndio eneo la ofisi kubwa kama hili hapana. Ningeomba sana uje utafute eneo yapo tu maeneo ili uweze kujenga eneo ambalo lina uhakika linaendana na hadhi yako.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la barabara za ndani. Mhe. Mwenyekiti, Chake Chake imekuwa na barabara nyingi ambazo zinahitajika kusafishwa ili kuweza kuangalia uwezekano wa kuupanua mji hasa. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, Chake Chake ina barabara ambayo inatoka Gombani kupitia Pagali ambayo hiyo inakwenda mpaka Wesha, nina wasi wasi ni barabara yako, kuna barabara ya Tinga Tinga nina wasi wasi ni barabara yako, kuna barabara ya Mapinduzi ambayo inakwendea Mgogoni nina wasi wasi ni barabara yako. Kuna barabara ya Polisi kuingia Machomane nina wasi wasi barabara yako, kuna barabara ya Mpendae kupitia Mkokotangozi ni barabara yako, kuna barabara ya Kiziwani ya Misooni. Nina barabara karibu kumi Mhe. Mwenyekiti, hizi zote zinahitaji mji na sioni vizuri mtu anakaa mjini kipindi kama hichi cha mvua anakuja kuvalia viatu barabarani akiambiwa anakaa Mji wa Chake Chake. Ningekushauri sana utakapokuja Mhe. Waziri njoo tuzipitie hizi barabara angalau tuzisaidie katika masuala hata ya *grader* ili kuweka angalau kifusi ziweze kupitika.

Mhe. Mwenyekiti, niongezee zaidi suala la kupongeza vikosi vyako. Mhe. Mwenyekiti, vikosi navipongeza sana kwanza vina nidhamu ya hali ya juu na vinajua wajibu wake hasa makamanda. Mhe. Mwenyekiti, mimi nikusifie sana tu maana yake wengine hawa askari kidogo waliokuwa wana ngazi za chini huwa tunatania taniana wengine hata saluti hawatupigii. Lakini hawa viongozi wakuu wako *up to date* Mhe. Mwenyekiti, ni kweli lazima niwapongeze sana wako katika umahiri kabisa wa jeshi lenye nidhamu. Kwa hiyo, hili nikupongeze pamoja na wewe umeshiriki katika masuala haya. Kwa hivyo, navipongeza sana vikosi vyako pamoja na utendaji wao wa kazi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la Michakaeni kuna soko lake pale. Mhe. Mwenyekiti, suala la soko la Michakaeni linahitaji kuja kukaa tena kama nilivyokwambia nakuomba uje ziara

ya siku nzima ulikague kuna maeneo pale sasa hivi yanatolewa tolewa ambayo haijapangwa lile soko la Michakaeni. Ningekushauri usimamishe chochote kinachoendelea pale Michakaeni mpaka mwenyewe ukakague uweze kutoa angalau maagizo watu wanajijengea jengea ovyo hatujajua na lile eneo tukilifuja hatuna eneo tena Chake Chake.

Mhe. Mwenyekiti, pia nikupongeze umeshakuja kufanya ziara sana Tibirinzi. Mhe. Mwenyekiti, sisi kwa maeneo ya mjini pamoja na Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati, maeneo pale ya Tibirinzi ambayo yapo mkabala na hoteli ya Archipelago au ya *ZSSF* bado pahala pale panahitaji *open space* ya kuweza wananchi kufika jioni na maeneo mengine ya kuweza kujipongeza katika masuala mengi. Mhe. Mwenyekiti, tusifanye makosa wenzetu wengi tunaona kwamba Ikulu haikaribiwi na majengo ya ghorofa na pale ni karibu na Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba sana Mhe. Waziri tushirikiane kuniongezea nguvu eneo lile ulipate wewe mwenyewe liweze kuwa ni vitendea kazi vya watu wa jioni kuweza kujipatia rizki na wengine kwa kustarehe. Ningekuomba sana nipo karibu sana na Mkuu wa Mkoa nashukuru ananiunga mkono sana na nashukuru ananishirikisha katika maeneo yake mengi sana, tunashauriana sana. Mimi nimsifu sana Mhe. Hemed pamoja na Mkuu wa Wilaya wangu Mhe. Halil tunakwenda vizuri sana na mimi hili napenda.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie tu nawapongeza sana mawaziri. Mawaziri wengi wanaokuja Pemba wakanipigia simu kwamba Mheshimiwa nipo katika jimbo lako maana yake mawaziri takribani wote wanaokuja wanafikia Chake Chake kwenye jimbo langu. Mimi sipendezewi wala sifurahii waziri kuja pale asinipigie simu, nimemuona kwenye gari au hata kuja kusalimia.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi nikusifu sana ukitaka kuja Pemba unanipigia simu nakushukuru sana hata kama hatuna *issue* yoyote na wewe lakini najua kwamba Mhe. Haji Omar Kheri yupo katika mji wangu, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed pia ananipigia simu, namshukuru sana Mhe. Salama Aboud Talib pamoja na Mhe. Amina Salum Ali. Hawa watu kwa kweli wananipa faraja wanapokuja Pemba. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, humu katika kitabu chako nimeangalia mambo mengi, lakini nimeona kuna eneo ambalo unahitaji pesa au umepewa pesa na Mfuko huu wa Barabara karibu sijui bilioni nne. Mhe. Mwenyekiti, kwa ushauri wangu mimi ikiwezekana hata hizo barabara zangu tutazipiga piga hivyo hivyo lakini ningeshauri kama kuna mpango maalum wewe ungejikita katika kununua makatapila na vijiko katika hizi bilioni nne ukajua angalau unaanzia wapi, halafu hivi vijiko ndio vitakufanyia kazi, kuliko pesa hizi ukawapa wakandarasi wakazila au wakazifanyia mambo mengine. Lakini wewe kila siku utakuwa hukui na wewe sasa hivi majukumu ya barabara za ndani kwa kweli tumekutwika mzigo mkubwa na bado huna nyenzo.

Kwa hivyo, ningeomba nimeona katika kifungu chake hapa kwamba utapewa pesa bilioni nne kwa ajili ya matengenezo ya barabara za ndani. Basi nikushauri kama itawezekana fanya tenda uzijue haya makatapila, pamoja na kupata ushauri *UUB* kwamba tunapataje vifaa ili uanze kusimama kwa miguu yako katika barabara za ndani. Ningekushauri sana Mhe. Waziri hilo.

Lakini pia nizungumzie Mhe. Mwenyekiti, nimeona kuna huu Mfuko wa *Welfare.* Mhe. Mwenyekiti, wazee wetu hawa wameshatutumikia sana bado kuna shilingi elfu tano ambayo unatoa haidhuru ukizijumlisha karibu bilioni nne, karibu milioni mia ngapi sijui nimeona katika kitabu hapa. Lakini nikushauri tu ikiwezekana basi waongezewe pesa kidogo angalau wafike kama ule mfuko wa Mhe. Rais elfu ishirini kutokana na hali ya matumizi yaliyoendelea nimeona hapa Mhe. Waziri. Kwa hivyo, nakuomba shilingi elfu tano sasa hivi imekuwa ni pesa ndogo sana inahitaji tuwaongezee hawa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie kwamba vikosi vyako nataka viige kama Jeshi la Wananchi wa Tanzania kule upande wa Pemba maeneo ya *Ali Khamis Camp.* Mhe. Mwenyekiti, wale wameanza na skuli na skuli sasa hivi imekuwa sana Skuli ya *Ali Khamis Camp* na ni skuli ya mfano na inachukua watoto Pemba nzima na watoto hawa wana nidhamu.

Ningeomba Mhe. Waziri na wewe kwa utaratibu wako ukaanzisha skuli moja pale Chake Chake maeneo yoyote hata ya Wawi yenye hadhi maana yake watoto wakilelewa kijeshi wanakuwa wakakamavu. Mhe. Waziri nenda ukatembelee hawa vijana wetu walioko katika skuli ya *Ali Khamis Camp* uangalie jinsi ya ukakamavu wao walionao. Lakini pia Mheshimiwa …

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, namalizia tu. Pia nenda kaangalie pia Hospitali ya Jeshini inatusaidia sana. Ningekuomba sana Mhe. Mwenyekiti, Unguja umeshajipanga sana kwenye masuala ya hospitali, lakini nakuomba na Pemba njoo utusaidie na utaisaidia serikali itaisaidia jamii.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho tu ninalomwambia Mhe. Waziri nakuomba sana utakapokuja Chake Chake njoo ufanye ziara kwa sababu mambo yaliomo humu ni mengi na nimeshindwa kuyazungumza. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Awali ya yote, kwanza nichukue fursa hii kuweza kumpongeza sana Mhe. Waziri na msaidizi wake lakini pamoja na watendaji wote wa taasisi zilizo chini wa wizara yako.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii ni muhimu sana kwa sababu karibu ya asilimia 40 ya matumizi ya serikali yapo chini ya wizara hii na hii ni kutokana na ugatuzi. Lakini nimpe pole sana Mhe. Waziri kutokana na majukumu mengi yaliyongezeka katika wizara yake.

Lakini nipongeze juhudi ya serikali katika kuimarisha shughuli mbali mbali zinazofanywa na taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, michango mingi imechangiwa lakini na mimi ningependa niweze kuchangia machache na kuweza kutia mkazo katika baadhi ya mambo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na suala zima la Madiwani wetu. Mhe. Mwenyekiti, Madiwani ni viongozi ambao wamechaguliwa kama tulivyochaguliwa sisi Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi pamoja wengine ambao wameteuliwa. Mhe. Mwenyerkiti, Madiwani ni viungo muhimu sana katika mustakbali wa maendeleo katika Wadi na Majimbo yetu na wananchi wetu wana mitazamo tofauti juu wa uwezo wa Madiwani. Wakati mwengine wananchi wanawalinganisha Madiwani na Wawakilishi lakini ilivyo ni tofauti kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilizungumza kwamba mafao na stahiki za Madiwani haziridhishi na mwaka huu naendelea unaendelea hivyo. Madiwani wana hali ngumu na sisi tunawatuma Wawakilishi tunapokuwa hatupo katika majimbo yetu. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali itazame maslahi na maposho ya Madiwani ili iendane na hivi vyeo vyao.

Mhe. Mwenyekiti, Madiwani hususan katika Manispaa ya Mjini ambayo nipo hawajatekeleza miradi yoyote katika Wadi zao katika hii miaka miwili na nusu ambayo tunakwenda ukilinganisha na nyuma, kisingizio kinakuwa ni sheria kwamba haijaanza kufanya kazi kwa sababu kuna Kamati za Maendeleo za Wadi. Mhe. Mwenyekiti, hii ni hatari, Madiwani wanatakiwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na wanatakiwa kuandika nini wamekifanya.

Lakini kwa maposho na mipango ambayo haitekelezeki watafanya nini katika Wadi zao. Mhe. Mwenyekiti, ningependa sana Mabaraza ya Manispaa yaweze kukaa na Madiwani kuwasikiliza vilio vyao katika Wadi kama sheria haijaanza kutumika lakini watiliwe pesa za kuweza kutekeleza baadhi ya miradi katika Wadi zao ili wananchi wawe na imani na Madiwani waliowachagua. Vile vile iwe na la kuzungumza katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, hili naomba sana kwa mwaka huu basi wizara inayohusika kuweza kulitazama na tuweze kuona kwamba Madiwani wanashirikiana na Wawakilishi na Wabunge katika kuhimiza na kutekeleza baadhi ya miradi ambayo imo katika Wadi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika suala zima la takwimu. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri katika ripoti ambazo zimekuja za bajeti, basi ripoti yake inaongoza kwa jadweli nyingi za takwimu ukilinganisha. Hii inatupa urahisi kuweza kuona mambo mbali mbali kitakwimu jinsi gani yalivyo na inatuwia rahisi kuweza kuona yepi yametekelezwa kitakwimu.

Mhe. Mwenyekiti, nielekeze tu kwamba baadhi ya takwimu zinagusa taasisi mbali mbali za serikali kwa sababu ni mambo mtambuka. Kuna takwimu ya uandikishaji wa wanafunzi na hii wanaitoa kwa sababu suala la elimu hivi sasa limegatuliwa hususan Elimu ya Msingi. Lakini takwimu hii hii inawezekana tukaja kuipata katika ripoti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenyewe. Tuna idadi ya wazee waliopatiwa misaada takwimu hii tunaweza tukaipata vile vile katika Wizara nyengine ya Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Tuna takwimu za matukio ya udhalilishaji ambazo tunaweza tukazipata wanawake na watoto, Mkurugenzi wa Mashtaka na kadhalika.

Sasa niombe sana takwimu ambazo zinawekwa humu basi chini kule katika taratibu za kitakwimu lazima uweze kusema kiini cha takwimu hizo zimepatikana wapi. Tumegundua mwaka jana takwimu zinagongana katika taasisi mbali mbali anapokuja Wanawake na Watoto wanakwambia kesi za udhalilishaji ni idadi fulani, lakini tunapokuja Ofisi ya Tawala za Mikoa wao wanatupa takwimu nyengine. Sasa hili naomba sana Mhe. Waziri kwa mara nyengine takwimu zioneshe zimepatikana wapi ili ziwe zinaaminika na ziwe za uhakika.

Nije kwa mfano tu katika takwimu ya udhalilishaji kwenye ndoa za umri mdogo Mkoa wa Mjini Magharibi inaonekana tukio ni moja tu la ndoa za umri mdogo hii inatia wasi wasi sana. Mkoa wa Mjini Magharibi ndoa ya umri mdogo tukio lake ambalo limeripotiwa kuwa moja lakini tukitazama Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna matukio manne, wakati mwengine ukizisoma hizi takwimu inaweza ikawa zinakupa wasi wasi kama zipo katika hali nzuri. Kwa hivyo, pamoja na wingi wa takwimu lakini ni vyema tujiridhishe kwamba takwimu hizi zipo vizuri kwa sababu zinasomwa na wengi. Kwa hivyo, tusije tukaweza kuwachanganya wale wasomaji wakaona kwamba takwimu za taasisi mbali mbali za serikali zenyewe hazioani.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa suala zima la mapato katika taasisi mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, taasisi hizi zina uwezo wa kukusanya mapato zaidi kuliko ambavyo inakusanya. Suala ni kuweza kuimarisha njia za ukusanyaji wa mapato, njia ambazo zinatumika hivi sasa kwa kweli zinapitiwa na wakati lazima tuelekee sasa katika njia za ki-*electronic* kwa sababu mapato mengi yanavuja ya serikali katika vyanzo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda wako hauruhusu ilikuwa niendelee zaidi lakini niombe tu kuzungumzia Kikosi cha Valantia. Mhe. Mwenyekiti, kikosi hichi kinahitaji kuongezewa uwezo wa kimapato, kwanza kile Kiwanda cha Viatu lazima harakati zake ziweze kutekelezwa katika bajeti hii ili tuweze kuona kwamba kiwanda kile kinafanya kazi kwa sababu wenzetu hawa mapato yao walitegemea mambo ya ulinzi na hivi sasa yameshaelekea katika wakala.

Vile vile kuweza kuwasomesha watu wake katika masuala ya kilimo kwa sababu wameanza kwenda katika miradi ya kilimo lakini wataalam wao ni wachache sana. Kwa hivyo, hawawezi kuendesha kilimo na kuweza kuleta tija iwapo wataalam wao ni kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kuhusiana na uwiano kuanzia yale mapato ya vikosi vya SMZ tunatarajia kwamba mapato haya huwa asilimia fulani yaende katika Mfuko wa Hazina, lakini hakuna uwiano kati ya Vikosi vya SMZ asilimia ngapi wapeleke hazina na asilimia ngapi waweze kutumia. Hili ningependa sana serikali iliweke wazi kwamba asilimia fulani ya mapato ya vikosi yaende Mfuko wa Hazina na wao watumie asilimia ngapi.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hayo nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa na mimi kwa ufupi naipongeza sana hotuba hii na naiunga mkono asilimia mia kwa mia. Tuiombe serikali iwape fedha hizi ili wenzetu waweze kutekeleza majukumu waliyojipangia. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi sasa namwita Mhe. Bahati Khamis Kombo na Mhe. Bihindi Hamad Khamis ajitayarishe.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi nikaweza kuchangia machache ambayo yamenikabili katika Mkoa wangu wa Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa nichukue fursa hii kuwapongeza Wakuu wote wa Wilaya Unguja na Pemba pamoja na Wakuu wote wa Mikoa ambao ndio walisimamia Wilaya hizo. Mhe. Mwenyekiti, pongezi za pekee ziende kwa Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba pamoja na vikosi vyote vya ulinzi na usalama viliomo katika Mikoa yetu. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika mjadala wetu. Kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Idara ya Uratibu na Utawala - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, tumeona hapa kwamba kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Idara ya Uratibu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia program ya Uratibu wa Utawala na Mikoa na Serikali za Mitaa ilipanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa ugatuzi kufanya mapitio ya mipaka ya kiutawala na kusimamia matengenezo ya barabara za ndani katika mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo jema na tunalipongeza sana serikali kutuwekea suala zima la ugatuzi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hakuna jambo lisilokuwa na changamato zake. Tumwambie tu Mhe. Waziri mimi nakupongeza sana wewe pamoja na Naibu Waziri wako kwa kusimaia vyema Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la ugatuzi la matengenezo ya barabara kwa kweli Mhe. Waziri hapa litakupa changamoto endapo fedha hizo bilioni 4 hakuongezewa kwa sababu fedha hizi tumeona hazitoshi.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mhe. Suleiman Sarahan Said kwamba unahitaji hivi sasa wewe kupatiwa vifaa vya kutosha ili uweze kuzitengeneza barabara zote za ndani. Tukiangalia barabara hizi zilizokukabili ni nyingi Unguja na Pemba lakini vitendea kazi huna. Tunaiomba serikali iangalie kwa kina juu ya tatizo hili ambalo limemkabili Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea niende moja kwa moja katika Mkoa wa Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza sana sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa mashirikiano mazuri anayotupa wakati tukiendelea ndani ya majimbo yetu katika miradi ya maendeleo. Mhe. Mwenyekiti, mheshimiwa hapa amesimamia mambo mengi ikiwemo barabara ya Ole/Kiwani, lakini pia kusimamia barabara ya Kipapo na Mgelema na barabara ya Kuyuni/Ngomeni.

Mhe. Mwenyekiti, barabara hii ya Kuyuni/Ngomeni haina misingi ya kutolea maji na sisi tunachokitaka hivi sasa tunaendelea kutengeneza maendeleo ambayo wananchi hawatopata tabu. Ile barabara ukosefu wake ni mdogo tu kukosa misingi, lakini ile barabara pia ni nyembamba. Tunaiomba serikali hivi sasa ikiendelea kutengeneza barabara basi tuistengeneze barabara za

zamani zile nyembamba, tuendelee na barabara hivi sasa zinazokuja na wakati kwa sababu tukiangalia ile barabara kama utapitisha gari ambalo kuwa lile za *ZCTS* ikapita na gari nyengine basi imekuwa ni tatizo kutokana na ule wembamba ambao inayo. Pia kutokuwekwa misingi ile barabara basi imekuwa vile vile ni tatizo. Mimi naomba hapa Mfuko wa Barabara basi itenge fedha kwa haraka ili barabara hii ya Kuyuni/Ngomeni iweze kuwekewa misingi kabla ya kuharibika.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika kifungu 334 kinachotueleza hapa uezekaji wa paa jipya katika Ofisi ya Wilaya ya Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni jambo jema lakini pia linatia huzuni kwamba ile Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani hivi sasa inahitaji marekebisho ya kutosha. Lakini ukiangalia hasa kama ni Ofisi ya Mkuu wa Wilaya basi haina hadhi, pia hata ile nyumba ambayo anakaa Mkuu wa Wilaya na Afisa Tawala wake zote zile hazina hadhi. Ipo haja ya kupatiwa eneo la kujengwa nyumba zenye ubora na hadhi nzuri zikaonekana kama zile nyumba kweli wanakaa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja Baraza la Mji Mkoani. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani kwa juhudi zake kubwa alizozichukua kuweza kuvuka lengo. Lakini pia niseme tu kwamba Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani ni mashirikiano mazuri aliyotuonesha kwamba anashirikiana na wafanyakazi wake lakini pia anashirikiana na madiwani wake wote waliomo katika Wilaya yake ndio maana akaweza kupita kiwango hichi cha fedha tulichonacho mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto kubwa ambayo tumeiona ni kuwa Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani hana hata gari za kutosha kwa ajili ya uzoaji wa taka hupaswa kukodi gari. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ni vyema Mabaraza yote yakapatiwa haya magari ili kuondosha ule usumbufu ambao wanaupata. Wakipatiwa magari ile fedha ambayo wanakodi zile gari basi itaendelea kurudi katika mapato yao na tutaona jinsi gani ambavyo wanafanyakazi.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyakazi ambao walitakiwa kupewa *arrears* zao na wameshatimia miaka 15 kazini bado wafanyakazi wale hawajapewa *arrears* zao. Nimuombe sana Mhe. Waziri asimamie kwa kina ili waweze kupata zile *arrears* zao. Nadhani mwaka uliopita nililisema hili nikapata jawabu kwamba tayari wameshalipwa, lakini nikwambie tu Mhe. Waziri kwamba bado wapo wale wengine ambao hawajalipwa. Niombe sana sana sina nia mbaya lakini naomba kuwatetea wafanyakazi wenzetu ili waweze kupata haki zao kwa mujibu wa sheria iliyopangwa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze sana Mkurugenzi wa Baraza la Mji kwa juhudi zake alizozichukua kuweza kuelimisha wananchi na hivi sasa tayari wanaendelea na shamba la darasa katika Jimbo langu la Chambani, Shehia ya Chambani. Namuomba sana Mkurugenzi huyo kwamba hili lisiwe ni mwisho liwe endelevu kwa wananchi wote wa Jimbo la Chambani ili

waweze kusimamia mashamba yao na waweze kupata kipato cha kutosha kwa sababu tumezowea kulima kile kilimo cha zamani ambacho hivi sasa hakituletei tija.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi hawa walipolima kilimo hichi mimi mwenyewe binafsi nilifarajika kwa sababu nilikwenda nikaona na matumaini mazuri ambayo wameweza kuyapata ni kuuza mpunga kilo mia kwa kila mwananchi mmoja. Kwa hivyo, naomba sana hili suala liwe endelevu kwa wananchi wote wa Jimbo la Chambani.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika program za Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, hapa niseme tu kwamba ndani ya Jimbo langu la Chambani limo Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambalo zamani ilikuwa ni kikosi ambacho ukiitaja Chambani basi ni Chambani kweli kweli na kikosi chake kizuri. Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, jeshi hili nimeona ile kambi hivi sasa haina hadhi na hadhi yake kubwa ni kuwepo kwa vijana wetu, lakini pale tumeona kwamba vijana waliopo ni kidogo kama ni mapitio tu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri jeshi letu hili lirudi kama zamani.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nikija tena katika jeshi hili hili la kujenga uchumi mwaka jana nilitembelea katika eneo hili la Kwapweza na nilipokuja hapa nikasema kwamba wale vijana wetu wa Kwapeza majengo yao ni mabovu. Lakini kwa bahati nzuri wakati wa kujibiwa swali Mhe. Naibu Waziri alinambia kwamba tayari ule ujenzi umeshaanza. Sasa tulitaka kujua tu kwamba atakapokuja hapa aniambie umeanza umeshakamilika au bado, na kama haujakamilika ni mwaka gani jengo lile alitegemea kumalizika ili vijana wetu waweze kupata hadhi nzuri ya kukaa pale na wao kama ni vijana shababi wa kuleta maendeleo na uchumi katika Jeshi la Kujenga Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti lakini vile vile katika vijana hawa hawa wa Kwapeza ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi mara nyingi dakika zangu zinakuwa ni tatu lakini leo ungeniacha nikachechemua kidogo. Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa wa Kwapweza mwaka jana walilima lakini katika kilimo chao kwa bahati nzuri ukulima wa mboga mboga yule bwanashamba wao alikwenda likizo wakapata bwanashamba mwengine. Yule bwanashamba ilikuwa ile si fani yake, fani yake yeye ni mambo ya magari akaendelea kuwasimamia wale lakini walikula hasara kubwa sana. Hasara ile si yao peke yao ni ya serikali yote kwa jumla. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama inawezekana basi mabwanashamba wale wawekwe wawili wawili kila kituo ili mmoja atakapokwenda likizo basi mmoja awepo na waendeleze kilimo vizuri bila ya kupata athari kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, leo mimi umenionea lakini naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa namwita Mhe. Bihindi Hamad Khamis na atafuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia leo hii nikaweza kusimama hapa kuchangia hotuba hii ambayo ipo mbele yetu. Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kusini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mkuu wa Wilaya ya Micheweni na Mkuu wa Wilaya ya Wete pamoja na watendaji wao wote. Pia nisisahau kumpongeza Mkurugenzi wa Baraza la Mji Wete na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni pamoja na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, nianzie kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kama unavyojua Ofisi yetu ya Mkuu wa Wilaya ya Micheweni ni ofisi ambayo imeshakuwa ni ya zamani sana na jengo lake lile litakuwa ni mjengo wa zamani. Kwa kusema hivyo ni kuwa Mhe. Waziri wizara yako pamoja na serikali kuweza kulisimamia hilo ili kuondosha utaratibu ule uliopo kwenye ofisi ile. Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua ofisi ile ina taasisi nyingi ambazo zimo mle ingawaje kuna Ofisi ya Vitambulisho sasa hivi watahama watakwenda kwenye jengo jengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea mbele niende Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni. Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita nilizungumzia kuhusu jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni nalo pia ni jengo ambalo si la kisasa ni la zamani sana, na kwa kweli pale nilizungumzia kipindi kilichopita cha bajeti kama ukuta ule umejengwa tangu 2011 haujamalizika, lakini lengo na madhumuni ni mazingira ya ofisi yetu ile kwa sababu pale panaingia maji. Pia nilizungumzia kuhusu mtaro mkabala na Kituo cha Afya cha Wingwi, lakini Mhe. Waziri tunaposimama hapa tunapochangia tunakuomba sana unapotoa ufafanuzi uweze kutoa ufafanuzi wa kutosha kwa sababu sisi tunasimamia wananchi wetu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Wilaya zake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende kwenye Kikosi cha Valantia Micheweni. Narudia tena nilizungumzia kipindi cha bajeti iliyopita kuhusu jengo lile kweli wamejitahidi sana lakini jengo lile au kiwanja kile kimewekwa *foundation* zamani na kikafikia hatua iliyofikia sasa hivi ni hatua ya kupongezwa mmefikia hatua ya kuezekwa. Lakini pia namuomba Mhe. Waziri kwa sababu ofisi ile ina mahitaji mengi, ofisi ile tunajua kwamba bajeti yako ni nzuri Mhe. Waziri lengo na madhumini ni kutekeleza wajibu wako. Lakini jengo lile likiwa na Mhe. Naibu Waziri anatokea kwenye Jimbo la Micheweni najua ni msimamizi mkubwa. Mhe. Waziri tunakuomba sana ofisi ile kwenye bajeti hii angalau iangaliwe ifikie malengo ili vijana wale waweze kuitumia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nimpongeze *DC* wangu wa Micheweni pamoja na Naibu Waziri akiwa ni Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM kuweza kutoa elimu kwa wananchi wa Micheweni ili kuweza kupata eneo la *parking* ya magari. Kwa sababu kama tunavyojua Micheweni *parking* iko maeneo ambayo pana skuli na kwa kweli inahatarisha maisha ya wananchi. Niwapongeze sana Mhe. Naibu Waziri pamoja na Wizara yake pamoja na kushirikiana na *DC* wa Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye udhalilishaji kama tulivyoelezwa zimetolewa takwimu Mkoa wa Kaskazini Pemba kuhusu ndoa ambazo ni za utotoni ni watu wanne kwa kweli hili ni kuhusu takwimu hizi zimefanywa kwa ufanisi zaidi. Niwapongeze lakini pia nitoe wito kwa wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Pemba hususan Wilaya ya Micheweni kuhusu udhalilishaji. Kama tunavyojua kwamba Mhe. Mkuu wa Wilaya anasimamia kuhusu udhalilishaji pamoja na dawa za kulevya amepiga hatua kubwa. Mtu sifa anapewa kwao, tunampa sifa Mkuu wa Wilaya ya Micheweni kwa kushirikiana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Micheweni kwa juhudi zake za kuwaepusha vijana wetu wasishiriki kwenye dawa za kulevya, ndoa za utotoni na udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele niende kwenye Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kikosi hiki kimefanyakazi kubwa sana kinastahiki kupewa motisha kwa sababu huwa wanakamata watu wa magendo zimepatikana asilimia kubwa ya pesa kama shilingi milioni 118. Kwa hivyo, iko haja kikosi hiki na wao kupewa motisha yoyote ili kuweza kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia nirudie kwenye Baraza la Mji la Wete. Mhe. Mwenyekiti, tuna Mkurugenzi ambaye ni kijana wetu mwanamama shupavu, anafanyakazi ambazo zinastahiki, ni mvumilivu na anachapa kazi, kijana huyu ameshakaimu. Kwa hivyo, tunakuomba Mhe. Waziri uweze kumuona ili kuweza kufanyakazi zake zaidi za kuongeza mapato kwenye Baraza la Mji la Wete pamoja na Mkoa wa Kaskazini Pemba. Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba sana Mhe. Waziri kwamba kijana huyu ni mwanamke, ni mwanamama mwenzetu aweze kulisimamia hili ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi mchango wangu ni huo. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na naipongeza hotuba hii kwa asilimia mia, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako niweze kutoa angalau machache katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyoisimamia serikali yake. Pia nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo naomba radhi kwa sababu hali yangu ya kiafya sio nzuri. Mimi nilikuwa na michango katika baadhi ya maeneo mawili au matatu. Moja ilikuwa katika

suala zima la barabara za ndani. Nimeangalia katika kitabu hiki lakini kadri ninavyosoma sijajitosheleza ipasavyo, lakini Mhe. Waziri atakapokuja atanitosheleza kwa sababu sijaona fedha zilizotengwa, lakini pia sijaziona hizo barabara zenyewe zilizoainishwa. Kwa bahati juzi nilileta swali hapa kwa wizara husika na nikajibiwa kwamba unachokihitaji kitakuja kwenye bajeti. Sasa nilifikiria kuwa kitakuwemo ndani katika hii bajeti nikiangalia nitakiona na kwa sababu ananifahamu Mhe. Waziri, nina kiu kubwa katika jimbo langu ya barabara ya ndani ambapo kwa muda mrefu nilikuwa nikipiga kelele, sio kwa maslahi ya Jimbo la Kwahani, lakini pia kwa maslahi ya wananchi katika Mkoa wetu wa Mjini.

Mhe. Mwenyekiti, eneo kubwa ninalozungumzia ni barabara ya Muungano, Kibanda Maiti, Kwa Kassim Ali kuelekea Kidongo Chekundu. Ile barabara ilikuwa ni barabara ya asili na ina mahitaji makubwa na kubwa ninalozungumzia ni kwamba ule uwanja unatumika kwa mambo mengi lakini kwa *security* haiko salama. Kwa sababu unakuta njia moja tu ya mbele ndio inaweza kupitika, lakini inapotokezea dhahma watu hawajui wakimbilie wapi inakuwa mtafaruku. Sasa nina imani kwamba Mhe. Waziri amenisikia na atazingatia na hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika sehemu hii najua tu tunapiga kelele kuzungumzia barabara zetu, lakini sote tunafahamu kwamba jitihada za serikali zimekuwa kubwa katika kutengeneza barabara za ndani. Nasema hili ndio maana nilianza kumpongeza Mhe. Waziri na kuipongeza wizara, kwamba jitihada katika kutengeneza barabara za ndani *almost* ziko katika hali ya juu na tunaridhika kila kitu, najua uwezo wao wa kifedha lakini wajitahidi kuangalia yale maeneo ambayo ni muhimu zaidi ambayo wanahisi wanaweza kuwatekelezea. Sasa hivi wananchi wengi wa Zanzibar wanaridhika na hali halisi ya barabara kutoka Magogoni kuelekea maeneo ya Mashine ya Maji, mtafaruku ulioingia huu unaweza kutusaidia ili kuepusha muda kuweza kukimbilia. Lakini barabara nyingi ambayo nasema kwa kweli serikali inajitahidi, pamoja na jitihada hizo basi na maeneo yaliyobakia wayaangalie uwezo utakapopatikana basi waweze kutuondoshea kero katika maeneo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nilikuwa nataka kuzungumzia eneo jengine la usafi katika mji wetu. Tumeona mabadiliko kwa muda mrefu lakini kumekuwa kukitokezea matatizo. Sasa suala hili nilikuwa nataka nitoe indhari kwa taasisi ya Baraza la Manispaa Zanzibar na wao wenyewe najua watakiri hilo, kuangalia mazingira ya kuweza kubadilisha bajeti zao ili kuendana na mahitaji na wakati uliokuwepo. Kwa sababu kunatokezea baadhi ya wakati mataka yanakuwa yanafurika katika maeneo, taka zinakuwa hazichukuliwi kwa muda mrefu na zinapokuwa hazichukuliwi kwa muda mrefu wanapochukua muda wanajitahidi kuja kufanya operesheni, lakini wanapokuja kufanya operesheni basi unakuta taka zimeshachuja na maji machafu yanatiririka katika mitaa na yanaweza kuhatarisha usalama wa watu. Unapokwenda kufuatilia basi unaambiwa bajeti yao ya mafuta haiko vizuri, utakuta wakati mwengine unaambiwa wanadaiwa huko wanakochukua mafuta.

Kwa hivyo, mimi nilikuwa natoa tahadhari namna ya kujipanga vizuri ili kuweza kuliondosha hili tatizo, tusije tukafika pahala kwamba matatizo kama haya yanajirejea kila siku kwa sababu tunajua kwamba wao wanategemea vyanzo vya mapato na vyanzo hivi vinategemea msimu na wakati mwengine msimu uko chini. Kwa sababu muda mrefu ambao wanategemea ni ule muda wa mwisho wa mwaka au mwanzo wa mwaka kwa ajili ya makusanyo ya leseni na mambo

mengine. Sasa ukija katika miezi ya kati kati ilikuwa kidogo wanapata mitihani. Kwa hivyo, ni vyema wakajipanga vizuri katika ile miezi ya kati ili kuweza kuepukana na hayo matatizo ambayo wanaweza kuyapata.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni suala zima la *parking* katika mji wetu. Kumejitokeza utamaduni sasa hivi wa kufunga haya makufuli, ukiweka gari dakika mbili au tatu kufuli limefungwa. Sasa tatizo hili wakati mwengine ni jema kwa sababu wanaondosha kadhia katika barabara zetu. Lakini mimi nilikuwa naomba wajipange ili baadae kuondosha huo mtafaruku kwa sababu unafungua gari lakini pakuweka hiyo gari yenyewe hupapati, sasa hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, mfano mkubwa ambao nataka niutoe ni katika soko la Mwanakwerekwe. Kwa mtu ambaye anahitaji huduma za soko la Mwanakwerekwe ambaye atatokea Fuoni hana eneo la ku-*park* gari zaidi mpaka azungushe gari kwa upande wa pili wa kulia, na eneo lenyewe huo upande wa kulia unataka ku-*park* gari eneo halitoshelezi. Sasa ningeomba wajipange katika bajeti zao ili kuandaa mazingira ambayo yanaweza yakasaidia, najua waliandaa eneo kwa ajili ya gari zinazoshusha mizigo lakini kuegesha gari hawataki. Kwa hivyo, ni vyema basi eneo lile wakaweza kulitanua katika bajeti zao ili wakaweza kuondosha hizo kadhia kwa sababu zinaleta mtafaruku mkubwa. Mtu anakuja anafunga komeo ukimuuliza niweke gari wapi hawana eneo. Sasa ni vyema basi na wao wajipange watengeneze maeneo ili kuweza kuondosha haya matatizo. Najua wananchi wote wapo tayari kufuata sheria hawataki kuweka magari barabarani, lakini wapi waweke tatizo hakuna. Kwa hivyo, hili ni suala ambalo linahitaji kujipanga zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nizungumzie,mimi nilikuwa nipongeze. Wajumbe wenzangu wengine hapa wamelalamika sana juu ya suala zima la *CCTV camera* gharama kubwa. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nipongeze kwa sababu sisi wengine kabla ya kuzungumza tumejaribu kufanya *research* katika maeneo mbali mbali na katika suala hili nilijaribu kuzungumza na swahiba wangu naona hayupo sasa hivi Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa sababu namjua yeye ni mchokozi zaidi na anayekwenda *in deep* katika kila kitu. Lakini akafika pahala akaniambia suala hili limejitosheleza, kazi iliyofanyika ni nzuri na kwa kweli ukiingia humu ndani uko katika hiyo *master cold room* yao ya *control* ya *CCTV camera*, unaridhika na namna usalama wa nchi unavyoonekana. Sasa mimi sitaki kuzungumzia namna ya mafungu mapesa kurudi najua mafungu haya yana utaratibu wake, Mhe. Waziri atakapokuja atakuja kujibu yeye. Lakini mimi napongeza namna *CCTV camera* ilivyoanza kufanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kutoa tahadhari vile vile kwamba inawezekana makosa tunayaona lakini tukashindwa kuyasimamia. Sasa naomba katika suala hili basi hao watu waliomo katika hiyo *control room* watakapoona makosa watu wafanyiwe kazi kwa sababu bado inaonekana kuna baadhi ya maeneo uzembe unafanyika na maajali yanafanyika, lakini na watu sasa hivi wamekuwa wakigonga watu mavespa wanakimbia na hakuna hatua zinazochukuliwa. Kwa hivyo, tumetumia gharama kubwa sana katika kuweka huu mradi, sasa kama tumetumia gharama kubwa sana basi yanapotokezea matatizo niiombe basi serikali ijitahidi kuchukua hatua kwa wale watu wanaofanya hayo makosa katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa nataka niingie katika hizi taasisi zetu za vikosi vya SMZ. Nimejaribu kuangalia na hususan JKU yale mambo ambayo wanazalisha mali na kuisaidia

serikali katika mapato. Mimi hapa Mhe. Waziri sijaridhika kwamba kinachozalishwa ni kidogo, umeshafahamu, na jeshi letu unalijua lina vijana wengi na sasa hivi wamejenga utamaduni wa kuwachukua vijana kwenda kujitolea. Sijaridhika kwa sababu nataka tusaidiane ili kuwaombeni hebu tukaeni kutafuta namna ya kuweza kuvisaidia hivi vikosi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naishukuru sana serikali na nashukuru juzi mmetuletea boti ya ulinzi sijui katika maeneo yetu ya bahari. Sasa isiwe hiyo boti ya ulinzi tu, tunahitaji maboti ya kuweza kuvisaidia hivi vikosi kwenda kuvua bahari kuu ili vikosi viweze kujitosheleza. Ikiwa wao tunahitaji katika maeneo mengine ya vikosi vyetu vya magereza vya mafunzo, na wao wafike pahala wajimudu, watafutieni matrekta waweze kuzalisha mali ili tuondokane na masuala ya kutegemea serikali. Leo rumande kuna watu wengi tunategemea bajeti ya serikali ndio ikalishe watu. Tukatafute *material* ili wao wale watu ambao wako jela basi wakafanye kazi ili kuweza kujitosheleza kutafuta chakula chao, lakini leo mtu anaona ah! mimi bora unipeleke huo rumande napata chakula cha bure na ninalala bure. Kwa hivyo, tufikie pahala kwamba waingie wanachokihitaji wazalishe wenyewe, wazalishe chao wao na pia wazalishe kuisaidia serikali, sasa hili ni jambo jema. Najua tulikuwa tuna mambo mengi huko nyuma, tulikuwa tuna miradi ya miti na mingine lakini tumekuwa hatwendi mbele na kwa sababu hatuna zana.

Kwa hivyo, mimi nahisi kwamba najua bajeti ndogo na tunafahamu uwezo wa serikali, lakini mipango kupanga ni kupangua, tupange kwanza halafu baadae tuishawishi serikali katika huko tunakoelekea. Nimezungumza katika maeneo mengi, kuna eneo hili lakini nimeona hapa katika masuala ya majengo ya mahospitali, hospitali ya Kibweni inawasaidia wananchi, lakini pia nimeona idadi ya watu ambao mnakwenda kuwasomesha, pia unafika pahala huridhiki. Kwa hivyo, kuna haja ya kufanya hizo jitihada za kuwa na madaktari wengi kwa kupitia vikosi vyetu vya JKU au vya KMKM ili hospitali zile ziweze kuwasaidia wananchi wetu. Nasema malengo yenu ni mazuri lakini nafahamu kwamba uwezo ni mdogo, lakini pamoja na hayo kuna haja serikali kujipanga katika maeneo haya ili kuweza kuwasaidia watu wengi sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umemalizika.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, namalizia kwa sababu nilisema sina michango mingi sana. Katika jambo moja ambalo hili namtaka sana Mhe. Waziri nampa tahadhari sana Mhe. Waziri katika hili kwamba tumeanza utamaduni waliokuwa wakiufuata wenzetu wa JKT wa kuwaajiri wafanyakazi kwa kupitia katika maeneo ya kujenga taifa ama iwe JKT ama iwe JKU. Maana yake hapa tunahitaji mtu ambaye anaajiriwa anakuwa mzalendo, anakuwa mkakamavu na anakuwa na mapenzi na nchi yake na anakuwa na uadilifu. Lakini nataka nikwambie na nasema tena, mimi nikizungumza nazungumza kwa ushahidi, sizungumzi kwa kumuonea mtu.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi ya JKU kuna baadhi ya maafisa inawezekana mmoja au wawili mmeshafahamu, wameanza utamaduni wa kughushi *document* ya watu ambao waonekane wameshatoka JKU wakati hawajapata mafunzo na wanayafanya hayo kwa kuchukua fedha za wananchi wetu. Maana yake wanafanya vitu ambavyo haviendani ni kinyume na utaratibu wa nchi yetu, lakini pia kuna hatari ya kutupa watu ambao hawajapata hayo mafunzo ya uzalendo na uadilifu na kuweza kutupotezea haki ambazo ni za msingi tunazojua na kima chao wanachochukua ni shilingi 300,000 mpaka shilingi 350,000. Natoa tahadhari hili lipo na

mlifanyie kazi, ili kuliepusha hili Mhe. Waziri mimi nafikiri kuna haja basi ya kuandaa *database* ya kitaalam ili watu wanapotoka wakimaliza ile kozi yao ile *database* ibakie na wewe mwenyewe uifahamu. Kwa sababu wakati mwengine wanachukua namba za watu wengine jina jengine na namba nyengine, sasa ni vitu ambavyo kwa kweli havitufikishi pale serikali inapohitaji malengo yake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nikizungumza jambo nakuambia lipo ukilitaka ukinitafuta nitakusaidia zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kuweza kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kabla sijaanza mchango wangu nataka niseme tu kwamba katika kitabu hiki au katika hotuba ya Mhe. Waziri kimsingi mambo mengi ambayo aliyoyazungumza ni mazuri na yenye matumaini kwa taifa letu. Lakini tu kuna mambo mawili hayo nitakuja kuzuia mafungu ili kujiridhisha ikiwa Mhe. Waziri pengine majibu yake yatakuwa hayakunitosheleza. Lakini naamini kwa umahairi wake na uadilifu wake naamini haya nitakayoyazungumza atayafuatilia na ataweza kuyafanyia kazi na mengine atayakiri vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na timu yake yote kazi kubwa wanazifanya na kwa kweli tunaziona. Mhe. Mwenyekiti, nataka moja kwa moja nianze nyumbani kwangu yaani jimboni ambako wao ndio walionileta hapa.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri baada ya kilio changu cha muda mrefu cha wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo, kuhusu kadhia ya mtaro unaotoka Darajabovu unaopitia Mboriborini mpaka ukamalizia Shaurimoyo na Saateni.

Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru katika mvua hizi za masika na zilizopita, kwa kweli ingawa mafuriko yalitokezea kila maeneo, lakini kwa kweli katika lile eneo ambalo limekuwa historia kwa ajili ya mafuriko na watu kuhama, kwa kweli tunashukuru sana safari hii tumepata faraja kubwa. Kwa hivyo, tunawaombea kwa Mwenyezi Mungu kuzidi kusimamia kazi zenu, ili wananchi wetu waliotuchangua waweze kuridhika na huduma yetu.

Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa tu kuna eneo moja ambalo pia nashukuru kwa mashirikia ninayoyapata kupitia Baraza la Manispaa, kupitia Mkurugenzi na kwa msaidizi wake ndugu Bwana Mzee, kwa kweli kuna changamoto ya vile vivuko au madaraja katika ule mtaro. Kuna eneo la pale Kwamtipura kwenye eneo ya Uwanja wa Kivumi Msikitini, kuna changamoto kidogo ya ujenzi wa lile daraja na nilimuomba kwamba leo tukitoka kwenye hiki kikao basi twende pale ili tuwasikilize wananchi wanahitaji nini. Lakini kimsingi hiyo nia ya kujenga hiyo daraja au hicho kivuko ipo lakini naomba waendelee kutupa mashirikiano, ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu baada ya kumalizika mtaro ule basi kile kivuko waweze kukitumia kama ilivyokuwa huko awali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nije katika yake maeneo ambayo nilikuwa nitahitaji ufafanuzi ili Mhe. Waziri na timu ya wataalamu wake wapate kujiandaa kwa ajili ya kufuatilia. Mhe. Mwenyekiti, nakusudia kuja kuzuia fungu la Idara ya Utumishi na Uendeshaji kutoka na kadhia ambayo iliyopo na inayoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna tatizo la wastaafu wa Idara Maalum, tunajua utaratibu watumishi wa serikali wanafanyakazi wanajituma wanapoteza muda wao mwingi, badala ya kwenda kondeni wanakwenda kutumikia majukumu ya serikali. Lakini kitu ambacho kinaumiza na kinasikitisha, wanapofika wakati wa kustaafu basi zile stahiki ambazo zipo kwa mujibu wa sheria na kanuni hazifuatwi zinafuatwa miongozo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii ni kubwa kwa kweli kuna idadi kubwa ya wastaafu wa Idara zetu Maalum na kila siku wanaongezeka. Suala hili naomba sana Mhe. Waziri ajaribu kulifanya kazi kwa sababu vikosi vyetu au Idara yetu Maalum wanafanya kazi nzuri sana, tena kazi kubwa sana kwa ulinzi wa taifa letu, lakini vile kwa uhai na ustawi wa nchi yetu, amani tuliyokuwa nayo katika nchi bila ya wao amani hii tusingekuwa tunajivunia.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nadhani kilio hiki kimeshafika wizarani na kama nilivyosema kwamba kuna baadhi ya wastaafu wa Idara Maalum baada ya kuona haki zao wakati wa kutotolewa hazikupatana waliamua kukimbilia Mahakamani, na walipokimbilia Mahakamani karibu watumishi 59 Mahakama iliweze kuagiza Idara Maalum iwape zile haki zao na walipewa hizo haki zao. Lakini sasa wale ambao amri ya Mahakama ilitoa wamepewa haki zao, lakini bado wale wengine utaratibu ule ule wa mwanzo unaendelea. Kwa hivyo, ina maana hapa tunatengeneza *rumor* na hawa kukimbilia Mahakamani, na si busara hasa *nature* ya kazi zao watu hawa baada ya kustaafu kukimbilia mahakamani kwasababu ina maana tutajenga *precedent* mbaya kwa waliokuwepo sasa, leo mtu anaweza akawa na madaraka na magari na nini, akisha kustaafu yale yote yanaondoka kitu anachotegemea ile hatma yake. Sasa hili Mhe. Waziri nitaomba ulifuatilie naomba zifuatwe sheria na kanuni iliopo kwa sababu bado haijabadilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka kuja kulizungumza au kuja kuzuia fungu katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti, nimejaribu kuangalia kifungu cha 22 nitaomba nikizungumzie ile *paragraph* ya mwisho tu. Mradi wa kuimarisha… Samahani Mhe. Mwenyekiti, labda nizungumzie kile kitu nilichokusudia kwamba katika kifungu cha 22 ufungaji wa vifaa katika kituo cha kupokea mawasiliano umekamilika hivi karibuni na unatarajia shughuli hiyo itaanza rasmi. Nakubaliana hoja ya Mhe. Mnadhimu wangu Mhe. Ali Salum Haji amezungumza kwamba mwanzo tulikuwa tuna wasi wasi wa ubora kwa hizi *CCTV camera,* lakini tumejaribu kufanya *research* fupi wenzetu wametupa taarifa zipo vizuri. Nafikiri huu mtambo ukija ukikamilika hapa kazi ya wale wahalifu itakuwa imefikia mwisho wao kwa sababu chochote watakachokifanya kibaya tutaweza kuyaona. Kwa mfano, hivi karibuni tumesikia kuna matukio mbali mbali ya uhalifu na nini. Kwa hivyo, hizi *CCTV camera* zitatusaidia sana katika kuweka kumbukumbu za wale waliokuwa wanafanya uhalifu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nilipojaribu kuangalia *paragraph* hii ya 22 kwa kweli haikubaliani na yale mafungu ya fedha yaliyoombwa katika mwaka huu unaokuja, maana yake huu mradi safari

hii umeombewa karibu bilioni 20, wakati huku katika maelezo mradi umekaribia kukamilika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi sikusudii hizi bilioni 20 zote ziondoke lakini naomba katika hili fungu ambalo la uboreshaji uendelezaji huu mradi ya bilioni 20. Mhe. Mwenyekiti, naomba fungu hili tupunguze shilingi bilioni 5 na fedha hizi ziende katika barabara kama tulivyosema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuangalia kifungu cha 38 mwenyewe Mhe. Waziri amesema hapa kwamba mahitaji ya matengenezo ya barabara zilizo chini ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Serikali za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ni makubwa, ukilinganisha na uwezo halisi wa kifedha uliopo hivi sasa kwa kipindi cha miaka mitatu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imepokea shilingi bilioni 4,600,000,000/-.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kadhia ya mvua kubwa ambayo bado tunaendelea nayo na ukiangalia bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi kupitia Idara ya UUB zile fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipya sitegemei kama itakwenda kwenye ujenzi ule, itarudi kwenye ukarabati wa barabara. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema fungu hili ni kubwa na kwa kuwa kazi kubwa iliyokuwa inafanywa imekaribia kumaliza mimi fungu hili nitaling'ang'ania mpaka kwenye kura *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi bado zitaendelea kuwemo kwenye wizara hii hii ya Tawala za Mikoa fedha sisemi ziende kwenye mfuko wa barabara, ziende kwenye maboresho ya barabara zetu za ndani. Mhe. Mwenyekiti, sisi wananchi ambao tuna majimbo kila mmoja hakuna hata mmoja barabara zake zilokuwa salama ndani ya jimbo lake, ukiangalia kuna maeneo mbali mbali ikiwemo barabara yangu ya Shaurimoyo. Najua Mhe. Waziri katika mipango yake nafikiri akija atatutolea ufafanuzi ni namna gani. Tunamshukuru sana Rais wetu alivyotoa maelekezo kwa Mawaziri watati, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, pamoja na Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi namna gani ya kuziboresha na kuzishughulikia hizi barabara za ndani na zile za *MIVARF*.

Mhe. Mwenyekiti, naamini bilioni 5 hizi tukiziotoa tukizirejesha huku katika sehemu ya uboreshaji wa barabara naamini utekelezaji wa Ilani karibu asilimia 40 itaongezeka. Mhe. Mwenyekiti, hapa palipobakia tuna mwaka mmoja na nusu kwa miaka miwili tunakwenda uchaguzi tunahitaji kuwaambia wananchi tumewaboreshea barabara zao tumewatilia lami na zile nyengine ndogo ndogo tumeweza kuwatilia kifusi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio mambo mawili makubwa ambayo nitaomba sana Mhe. Waziri aje anikubalie. Naamini hata yeye katika jimbo lake pesa hizi anazihitaji kwa sababu kama nakumbuka kule Tumbatu kuna barabara imejengwa muda mrefu lakini mpaka leo haijamalizika. Naamini katika hizi bilioni 5 na yeye vile vile ataweza kwenda kuwaboreshea wananchi wake wa Tumbatu ili wazidi kummiminia kura mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja sasa kwa mambo mengine mazuri waliyoyafanya. Mhe. Mwenyekiti, lazima tukiri. Waswahili wanasema "Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni". Mhe. Mwenyekiti, tunakushukuruni sana, kwanza nataka nimpongeze Mwenyekiti wangu kijana,

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Mjini. Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tuliona kwenye vyombo vya habari aliwaita Masheha karibu wote wa Mkoa wa Mjini kichama na aliwakabidhi zile *fire-extinguisher,* sasa hivi katika shehia zetu katika Wilaya yetu ya Mjini naamini kila Sheha amekabidhiwa *fire-extinguisher.* Kwa hiyo, kutokana na moto aliouzungumza Mwenyekiti wetu yule amesema ametoa *fire-extinguisher* kwa kutoa *message* kwa wale watu wabaya hataki kuona moto ukiwaka mjini. Mhe. Mwenyekiti, *fire-extinguisher* zile alizozitoa naamini Masheha wataweza kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nataka niseme kwamba katika eneo la ofisi yetu ya Mkuu wa Mkoa mimi kwanza nampongeza kwa kazi nzuri anazozifanya lakini namuomba sana azidishe nguvu katika maeneo ya ulinzi. Lakini vile vile ajitahidi sana kuwasimamia vijana wake katika kufuata sheria hasa katika mambo ya ulinzi. Lakini kubwa ambalo ninalotaka kulisema kwamba ofisi yetu ile ya kwa Mkuu wa Mkoa pale Amani kile ni kiwanja chetu yale mabati kwa kweli yameshakaa muda mrefu. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri kulikuwa kuna mpango wa kujenga Ofisi za Wakuu wa Mikoa, tayari Kusini, tayari Kaskazini, Mkoa Mjini tumeganda. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri katika mpango wake kazi ajaribu kuangalia ili kujenga ofisi yetu ile ya Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie la mwisho kabisa kuhusu JKT na JKU. Mhe. Mwenyekiti, tunakubali na tumesikia kauli ya serikali kwamba sasa hivi ajira hasa za Idara zetu Maalum pamoja na Jeshi na Polisi vijana wetu wapitie JKU, lakini tatizo tulilokuwa nalo JKU si kama vijana wote wanaotaka kwenda wanapata hizo nafasi kwa sababu zile nafasi kule ni chache. Kwa hivyo, tunaweza tukaweka *room* nyengine vijana wetu wameshamaliza skuli wanabakia majumbani ajira hawana, ajira zinakuja moja kwa sababu wanaambiwa hawana sifa za kwenda JKU. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi vya kutosha *otherwise* tutakuja kutengeneza kundi ambalo litakuwa wale wana haki ya kuajiriwa na hawa hawana haki ya kuajiriwa jambo ambalo kwa upande wa vijana halitotusaidia sana. Baada ya haya machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 80 na ile asilimia 20 naibakisha kwa yale mambo mawili. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mheshimiwa, sasa namwita Mhe. Maryam Thani akifuatiwa na Mhe. Mussa Ali Mussa. *(Makofi)*

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia machache katika hotuba hii ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niwapongeze Wakuu wa Wilaya wote na Wakuu wa Mikoa wa Zanzibar kwa kazi nzuri wanazozifanya katika jamii zetu au katika nchi yetu. Niwapongeze kwa kusimamia vyema uingiaji na utumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wamefanya kazi nzuri sana kuhakikisha dawa za kulevya hazitumiwi nchini kwetu. Mimi niseme jitihada hii waliyoichukua ya kusimamia dawa za kulevya wajitahidi kusimamia na mambo mengine ambayo yamo kwenye

nchi yetu na ambayo si mazuri tukizingatia kwamba Zanzibar asilimia kubwa ni waislamu na hasa kipindi hiki cha mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia pande zote za Zanzibar sehemu tunazotembea akinamama na akinababa mavazi mengine hayastahiki kuvaliwa. Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wawe na mkakati maalum wa kuzuia mavazi mabaya yanayovaliwa Zanzibar. Enzi za Karume kulikuwa na mavazi mazuri yaliyokuwa yakivaliwa wanaojua. Kwa nini sasa hatuwezi kudhibiti mavazi Zanzibar hali mbaya. Sasa tujiulize Zanzibar tumekumbwa na nini? Kumbe ni hali mbaya ya mavazi na mambo mabaya ambayo yanafanywa katika Zanzibar yetu. Leo Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, juzi tumepata taarifa waliokwenda mahotelini mimi sijui yalivyokuwa. Lakini katika matembezi yetu ya mahoteli tuliambiwa kwamba kuna taarifa mwisho saa 6:00 usiku sehemu za starehe. Kwa nini hii isizingatiwe kwenye sehemu za starehe ikiwemo mahoteli mwisho saa 6:00 usiku si kiwango kidogo cha starehe.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kupitia hawa Wakuu wa Mikoa na Wilaya saa 6:00 usiku iwe ni kiwango wasizidishe inatosha, jamani Zanzibar tunaipeleka pabaya, uislamu tunaupeleka pabaya. Leo watu mitaani wanaojiuza wapo wengi, kwa nini Wakuu wa Wilaya na Mikoa wasidhibiti wanawake wanaojiuza? Wasiwepo Zanzibar hatuwataki ni karaha. Nawaomba wasimamie hili wasiwepo ikiwa hawaliwezi askari jamii tunao katika shehia zetu wasimamie haya. Na ikiwezekana wanaovaa mavazi haya wapigwe mikwaju. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti niendelee katika sehemu hii ya vikosi vyetu hawa JKU. Mhe. Mwenyekiti, katika jibu lake mama Mhe. Waziri juzi alisema kwamba kwa upande wa Pemba vijana hawahamasiki kwenda JKU, lakini niwaambie vijana wa Pemba wanahamasika sana kwenda JKU tena wanahamasika, kinachowarejesha nyuma baadhi yao vijana ambao wapo JKU mwaka mmoja au miaka miwili leo ajira zinapokuja anayekuja pale siku tatu ndie anayechukuliwa na kuajiriwa. Kwa nini iwe hivi? Kwa nini wasiajiriwe vijana wale wanaojitolea mwaka mzima wapo JKU anachukuliwa mtu kaja pale siku mbili ndio anaajiriwa. Mhe. Mwenyekiti, kweli tutawakatisha tamaa vijana wale kutokujiunga na JKU. Namuomba Mhe. Waziri hili alizingatie, vijana wa Pemba wapo tayari kujiunga na JKU, au vijana wote wa Zanzibar wapo tayari kinachowarejesha nyuma ni hiki. Vile vile vijana hawa wameshajitolea miaka mitatu wapo nyumbani leo anayekuja kuajiriwa aliyepo JKU. Yule aliyepitia JKU anaambiwa kazidi umri kwa nini nae miaka ameshaipoteza JKU kufanyakazi ameshajitolea, ameshajenga uzalendo, ameshakuwa mkakamavu, lakini leo baada ya kutoka JKU anaambiwa aliyepo JKU ndie anayechukuliwa na kuajiriwa. Tunawakatisha tamaa vijana wetu kujiunga na JKU. Mhe. Waziri mimi nikwambie vijana wapo tayari lakini haya ndio mambo yanayowarejesha nyuma kujiunga na JKU.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye vikosi vyetu. Vikosi vyetu vyote vya Zanzibar kwa kweli vinafanya kazi nzuri sana tena vinastahiki kupongezwa kwa hali na mali kwa kazi wanazozifanya wanajitahidi na hawa kama serikali wawape tuzo maalum. Niseme kwamba KMKM wanajitahidi kuzuia mapato, wanajitahidi kuzuia mambo mabaya yanayoingia ikiwemo kuzuia magendo ya karafuu, uingiaji wa dawa za kulevya, wanajitahidi kwa hali na mali kuhakikisha mambo haya wanayadhibiti.

Lakini leo Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya vikosi au niseme vikosi vyote posho lao la likizo hawapewi kwa nini, maposho ya miezi hawapewi na ni vijana ambao wanafanyakazi kwa jitihada zao zote. Lakini leo stahiki zao hizi ambazo ni muhimu na kazi wanazozifanya ni ngumu hawapewi Mhe. Waziri tuwahurumie. Kwa hiyo, mimi nawaambia kwa kuwa wenyewe hawawezi kuwaambia wakubwa zao kwa haya lakini sisi tuliomo katika jamii tunayaona na ni kweli hawapewi. Kwa hiyo, naiomba sana Wizara iwaonee huruma kuwapa maposho yao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nizungumzie kituo changu cha KMKM Gando. Kwa kweli kituo hichi niwapongeze sana na wao kwa kazi wanayoifanya kwa sababu sehemu waliopo ni sehemu ya bahari vitu vinavyoingia na kutoka wao wapo na wanajitahidi kuvidhibiti. Lakini katika kambi ile niseme Mhe. Mwenyekiti, wanasumbuka sana hawana umeme, naomba wizara iwaone kwa jicho la huruma wanatoka masafa marefu kwenda kufuata umeme angalau kutia simu zao *charge* ili kupata mawasiliano. Sehemu wanayokwenda kutafuta huduma hiyo ni ndefu, kwa hiyo kama wizara naiomba sana ijitahidi kuwashughulikia hawa nao kuweza kufanya mambo yao kwa haraka.

Mhe. Mwenyekiti, niende Baraza la Mji Wete nawapongeza sana Mkurugenzi pamoja na watendaji kwa jitihada zao wanazozichukua kuhakikisha mji wetu wa Wete uko vizuri. Niseme mji wa Wete kwanza ni msafi na Halmashauri ya Wete inajitahidi kufanya miradi ambayo tumeiona katika kitabu hichi niwapongeze sana. Wanasimamia miradi hii kuhakikisha kwamba wameitekeleza katika maeneo tofauti, ila nawaomba sana kwa heshima na taadhima barabara ya ndani ambayo ipo Bopwe Kiwanda cha Sabuni hali ni mbaya kuliko maelezo. Ukizingatia wakaazi wengi wa kule wanatoka kutafuta huduma kama mfano wakiwa na wagonjwa kuja hospitali ni ngumu hasa katika kipindi hiki cha mvua.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba Wizara pamoja na Halmashauri hii iweze kuwatengenezea barabara ile kwa hali na mali. Ingawa tumeambiwa kwenye ukurasa wa 14 wa kitabu kwamba wameingiza shilingi bilioni 4,600,000,000/- kwa Mfuko wa Barabara na matengenezo ya barabara za ndani. Kiasi hichi cha fedha ni kidogo, mimi nasema hata kama ni kidogo lakini ukizingatia hatukuainishiwa ni barabara zipi za ndani ambazo zitafanyiwa ukarabati huo. Hivyo naiomba wizara iitazame barabara hii ya Bopwe kwa hali na mali.

Mhe. Mwenyekiti, nirudie tena kikosi hichi cha KMKM. Mhe. Mwenyekiti, kikosi hichi kwa taarifa ziliopo hawana sare, wakija ofisini kudai katika vikosi vyao wanaambiwa sare zitakuwepo kwa ajili ya vikosi hivi ya KMKM, lakini hadi hii leo hawajapatiwa sare. Kwa hivyo, naiomba wizara ifanye jitihada hiyo kama vikosi vilivyopo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache na mimi naiunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja, ahsante. *(Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Maryam Thani Juma, sasa namwita Mhe. Mussa Ali Mussa na Mhe. Makame Said Juma ajitayarishe.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii nipate kuchangia machache kwenye bajeti hii ya wizara husika. Kwanza mimi nataka niingie kwenye vikosi. Kwa kweli vikosi vyetu hasa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), maana ya Jeshi la

Kujenga Uchumi ni kujenga uchumi kwa kuzalisha mali pamoja na ulinzi. Mhe. Mwenyekiti, sasa leo tunawachukua vijana tunawapeleka katika Jeshi la Kujenga Uchumi, tukishakuwapeleka huko tunakaa nao miaka miwili tunawapa mafunzo ya ulinzi pamoja na kujenga uchumi wenyewe. Lakini matokeo yenyewe wakishamaliza miaka miwili tunawarejesha majumbani wanakuwa hawana kazi nyengine yoyote wamepoteza muda bure na serikali imepoteza pesa bure. Sasa namuomba Waziri anayehusika, Waziri mzoefu, Waziri shupavu,Waziri hodari jambo hili aliangalie na alikatae, JKU aiboreshe kwa kuipatia vifaa, awapatie mafunzo ya ulinzi, mafunzo ya uchumi, ni lazima awatafutie matrekta pamoja na vifaa mbali mbali waende wakazalishe chakula.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar haina haja ya kununua chakula iwapo jeshi hili litaimarishwa kwa kuzalisha uchumi, uchumi tunaoutaka ni kupata chakula. Leo wenzetu JKT kule Tanzania Bara wanazalisha chakula wanaweza kulilisha jeshi pamoja na kuuza kwa watu binafsi. Sisi jeshi letu halifanyi hivyo, tukishamtoa kijana miaka miwili tunamrejesha mitaani, sasa tukimrejesha mitaani huyu kjana anabadilika na hatari yenyewe ni kwamba tumeshamuandaa kijeshi tunamuingiza katika mazingira ambayo si mazuri. Sasa Mhe. Waziri nakuomba sana ujenge kambi, ujenge majumba ya kuwaweka vijana hawa, uwapatie vifaa ambavyo vitafanya wazalishe mali na ikiwezekana utafute nchi ambazo zina imani na Zanzibar kama China uwapeleke wakasome hawa mambo ya kilimo. Ikiwa ni kazi kuwapeleka kule kwenda kusoma waletee wataalam kutoka China wenzetu wameendelea kwa mambo ya kilimo waje hapa wawafundishe hawa kulima.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kazi chungu nzima za kupata ajira wakaweza kujilipa wenyewe. Kwa mfano, viwanda vyetu vya Maruhubi kule vilivyokuwa vikitengeneza viatu vimekaa ovyo havina kazi yoyote hawa wanaweza kwenda kuzalisha mali, kutengeneza viatu tukauza ndani ya nchi yetu, tukauza nchi za nje uwezo huo wanao. Wanachotakiwa hawa ni kuendelezwa tu na kupatiwa nyenzo za kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikitoka hapo nizungumzie vikosi hivi hivi kwa upande wa Zimamoto. Mhe. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri azitake Wizara zote, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya, kila wizara ichangie vikosi vya Zimamoto kwa sababu vikosi hivi vina kazi kubwa kila mtu anategemea katika wizara yake kuja kupata janga la moto. Kwa hivyo, vikosi hivi viwepo na viwe na uwezo wakae pale maofisini wakague wizara, kwenye mawizara waweke *fire extinguisher* waende wakazikague kama hazija-*expire*. Watengenezewe mazingira ya kupata maji inapotokezea moto, leo ukitokezea moto Shangani maji hamna yapo Kilimani, lakini ukitokea moto pahala pawe na *fire extinguisher*, pawe na kisima vile vile cha kupata maji hawa waweze kufanya kazi zao vizuri. Hawa vijana ni wazuri wanafanya kazi nzuri wanajitahidi lakini hawana nyenzo. Leo ile mipira ya kukamata mikononi imepitwa na wakati, Mhe Waziri watafutie magari hawa ya kisasa ya kuzimia moto waweze kuzima moto hata kama nyumba ikiwa ina ghorofa sita au saba, waweze ku-*press* kwa kutumia magari yao. Sio mambo ya zamani yameshapitwa na wakati ya kujitwika mipira mabegani yale mambo hayapo tena.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kwa sababu muda hautoshi sasa nataka niende kwenye vyeti vya vizazi na vifo. Kwa kweli tatizo la vyeti vya kuzaliwa limekuwa sugu, mtoto anazaliwa

mpaka anafika miaka mitatu au minne bado hajapata cheti cha kuzaliwa, haiwezekani mtoto wa nchi hii Mzanzibari awe hana cheti cha kuzaliwa. Masheha baadhi yao wamekuwa wakipoteza kumbukumbu hizi na unakuta watoto mitaani wanataka kuingizwa skuli, mtoto anaingizwa skuli kwa cheti cha upimaji mimba cha mama yake. Hili jambo nalo watendaji wetu waliangalie vizuri sana kwa sababu litatuweka pabaya, leo mtoto wa Zanzibar hana cheti cha kuzaliwa itakuwaje, mpaka anafikia miaka mitatu hajapata cheti cha kuzaliwa. Ukienda kwa Sheha kikaratasi kile hajui alipokiweka, sijui atakwambia wilayani nasumbuliwa kumbe si kweli cheti kakiweka juu ya meza mtoto wake amekichezea hakipo tena kimeshapotea ukienda kule nako unasumbuka. Kwa hivyo, tunataka mtoto akizaliwa baba mtoto moja kwa moja achukue cheti chake kile cha kuzaliwa kwa mtoto aende ofisi husika.

Mhe. Mwenyekiti, Wakuu wa Wilaya kwa sababu ni mahodari na ni watendaji wazuri wa kazi walishughulikie jambo hilo mtoto ndani ya wiki moja awe ameshapata cheti chake cha kuzaliwa. Kwa sababu sasa tuna Wakuu wa Wilaya wazuri, tuna Wakuu wa Mikoa mahodari tena watendaji hasa kule Pemba, Pemba Wakuu wa Mikoa ni Majemedari wa Kijeshi. Mkoa wa Kusini Pemba una Jemedari, Mkoa wa Kaskazini una Brigedia wao hawakai ovyo, hawalali wanachangamkia nchi hii. Hasa kule Kaskazini namsifu sana Mkuu wa Mkoa wa kule. Kaskazini kulikuwa hakukaliki, leo Mwenyezi Mungu amejaalia Kaskazini ukimpa mtu *Asalaam aleikum* anaitikia kwa utendaji mzuri wa bwana huyu, huyu bwana ni hodari na ni Brigedia kweli wa siasa.

Leo Kaskazini watu wanaswali pamoja, watu wanazikana kwa ushupavu wa bwana huyu. Sawa na Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Kusini aliyepo nasema ni kiongozi hodari sana, mtendaji wa aina yake. Leo Kusini ukija unafikiri Unguja tena Unguja yenyewe Mjini Magharibi, maduka yamejaa vitu kila unachokitaka unakipata, hayapo tena yale mambo leo Kusini ya kungojea tarehe zije. Leo kila mtu ana tarehe yake, kila mtu ana biashara yake hakuna tena kungojea mguu nyuma, hakuna kitu kama hicho, tunakwenda kama inavyoagiza CCM mbele kwa mbele, hata kama kuna ukuta tunakwenda tu mbele tunavunja ukuta tunakwenda mbele haturudi nyuma, hatuweki mguu nyuma kwa uhodari wa Mkuu wa Mkoa huyu. Umeondoka mguu hauko nyuma utaweka mguu nyuma utafika lini na mguu uko nyuma unadanganya watu, mguu uko mbele kwa mbele.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba ahsanteni sana Wakuu wa Mikoa pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Mjini nimefurahi sana, sasa leo mpaka ikifika 2019 nadhani dawa za kulevya itakuwa historia katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Huyu bwana yuko vizuri tena yuko vizuri sana nampongeza sana hawa ndio Wakuu wa Mikoa tuliokuwa tunawataka.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umekwisha nakupa dakika mbili.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Nataka nikueleze kwamba kuna muda wa uzee kwa hivyo nipe dakika tatu za uzee.
Mhe. Mwenyekiti: Nakupa dakika mbili.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Twende kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliyogatuliwa. Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Haji Omar Kheri, waziri mtendaji, waziri makini, maskuli

hayana walimu, watoto hawawezi kufaulu bila walimu, na walimu wazalendo tunao, kuna walimu wapo maskulini wanajitolea huu ni mwaka wa saba bado hawajaajiriwa. Fanya maarifa yako, fanya juhudi yako pamoja na serikali vijana hawa waajiriwe wakatusomeshee watoto wetu. Huwezi kuwa na elimu bila kuwa na walimu, walimu ni kidogo maskulini. Kwa mfano, skuli yangu ya Ole wamestaafu walimu kumi na tatu ajira hizi za mara hii imepata walimu wawili, tunataka walimu, walimu wazalendo wanaoumwa na nchi hii ambao wapo pale miaka saba, nane wanajenga taifa wanangojea ajira hawajaajiriwa mpaka tunafikia sisi Wawakilishi sasa kuwatafutia sabuni. Kwa hivyo, idara hii iangalie sana kama ni ugatuzi igatuliwe kweli tupate elimu haraka watoto wetu wanakaa darasani watoto 120 mwalimu atasomesha vipi, mwalimu mmoja ana vipindi karibu tisa. Lakini pakiwa na walimu patakuwa na elimu nzuri na elimu sasa imepanda Zanzibar asikudanganye mtu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi naunga mkono asilimia mia.

Mhe. Mwenyekiti: Anayefuata ni Mhe. Makame Said Juma na Mheshimiwa Tatu Mohammed Ussi ajitayarishe pamoja na Mhe. Mohamed Said Mohammed.

Mhe. Makame Said Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia japo kidogo katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika siku ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu mimi utakuwa ni mdogo sana lakini udogo wake lazima niuseme. Kwanza, niipongeze Ofisi yetu ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Mkuu wa Mkoa wake pamoja na Wilaya zake kwa juhudi zao wanazozifanya nzuri sana. Lakini hususan pongezi hizi ziende sana kwa Mkuu wa Mkoa kwa sababu Mkuu wa Mkoa naamini kama ni nahodha anasafirisha chombo, basi angepewa shahada rasmi ya kuongoza chombo mpaka akakipeleka bandarini. Kwa sababu mkondo aliouvuka ni mkubwa sana mkondo wa siasa Kaskazini Pemba ulikuwa kama si mtu mahiri hawezi kuuvuka, lakini naamini kama vile aliyesafirisha chombo ndani ya mkondo wa Nungwi wakati wa kaskazi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote hayo naipongeza sana serikali katika wizara hii wakati iliposimamia majengo ya vikosi vyetu vya KMKM kwa sababu naamini katika kituo chetu cha Kojani bandarini pale ilikuwa jeshi lile linakaa katika mabanda ya dago. Lakini sasa hivi limepata sehemu nzuri tena inastahiki na inafaa hasa wizara hii kupewa pongezi kwa sababu pale ilikuwa kama kichaka watu wamejificha, lakini sasa imekuwa ni ofisi rasmi na ni kituo rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, kituo kile baada ya kujengwa na hadhi yake ilivyo sasa mimi nauliza tu kama kituo kile kina usajili rasmi? Lakini kama hakina basi kifanyiwe utaratibu kipatiwe usajili rasmi na hususan kituo itabidi kipate uzio kutokana na ule urasmi wake, ukubwa wake, umaarufu wake na ubora wake. Kwa sababu watu wanajingiza ndani ya kituo kile kiholela itafika wakati mtu atakuja kupata adhabu kwa kuingia maeneo sio yeye hajui lakini akapata adhabu kwa sababu kile kituo si eneo la kuchezea. Sasa naomba kipate uzio ambao utakifanya kituo kile kuwa kizuri zaidi na kuwa na ubora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naingia kwenye ugatuzi. Kwanza na mimi niipongeze sana serikali kufanya jambo hili la ugatuzi ambao unatusaidia sana. Nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri baada ya ugatuzi jinsi alivyochukua juhudi zake nimpigie mfano, toka ugatuzi ulipokuja ameshafika mara mbili katika kituo changu cha Kojani. Naamini ufuatiliaji wake mzuri tena ni muhimu sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi huyu Naibu Waziri sijui nimfananishe na mfano gani jinsi anavyofuatilia shughuli zake vizuri, na kama vile Mhe. Waziri alipomwambia kuwa ipo haja ya kuvaa viatu vyangu na mimi nasema ipo haja ya kuvaa viatu vyake kwa sababu anafanya kazi vizuri na anafuatilia vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kituo kile cha hospitali ya Kojani kwanza kimefikwa na changamoto ya uzio kwa sababu vituo navyo vinataka huduma na kile kituo kipo karibu na wananchi, sasa kuna haja ya kupatiwa uzio wa kudumu sio uzio ule uliokuwepo wa nyaya karatasi ambazo waya zile baada ya siku kidogo tu zinaoza. Sasa hivi hazifai tena.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kwa sababu ya muda niingie katika Ofisi ya Wilaya Ndogo, mimi nasikitika sana serikali ilifanya jambo zuri sana na tukaona fahari kubwa Wilaya Ndogo Kojani ilitangazwa toka mwaka 1991. Miaka mingapi hapo imeshapita lakini mpaka hii leo ninavyosema ilipotangazwa ikapata wafanyakazi watatu, baadae wakawa wanne, mmoja akafa wakabaki wale wale watatu, baadae akaongezwa mfanyakazi mmoja mlinzi wamebaki wanne, wafanyakazi watatu na walinzi wawili.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana Wilaya Ndogo hii sijui ni udogo wa kufa au wa kupona, lakini naona kama udogo wa kufa kwa sababu kutoka miaka hiyo yote mpaka leo wafanyakazi ndio hao hao. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana. Sasa hili linanikera sana na hii si mara ya kwanza kulisemea, wala si mara ya pili na wala itakuwa si mara ya mwisho kwa sababu linauma sana. Hapa juzi tu niliambiwa kama kuna wafanyakazi watatu tayari wameshaajiriwa yameshapelekwa majina yao na tayari wameshajazishwa mkataba na sasa hivi wapo katika Tume ya Mipango, lakini naona mipango hii ilikuwa mipango ya kuharibu, mpaka leo jambo lile halijafanyiwa kazi inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo lakini lazima nitoe pole kwa jeshi letu la KMKM lilivyopoteza watu wawili ambao ninawafahamu. Kwa sababu juzi tu mwaka huu uliopita nilipoteza mfanyakazi mmoja kutoka bandarini Kojani kuelekea katika doria akenda kukumbana na wimbi la mlango chombo kikabiruliwa kwa bahati mbaya maisha yake yakapotea. Nawapa pole sana na mwengine mmoja akafa Unguja pia namfahamu pia nao nawapa pole.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naamini wazi ugatuzi pia ni jambo muhimu katika suala hili hususan katika barabara zetu za ndani, sambamba na barabara yangu pale kutoka Mzambarauni mpaka Mchanga Mdogo ile barabara nayo inahitaji. Kwa sababu sasa hivi imefanyiwa ukarabati wa kifusi na ikapitika vizuri lakini kabla ya mvua hizi ikaharibika tena, sasa hivi naamini baada ya mvua hizi haipitiki tena ile barabara ni muhimu kwa sababu ndani yake mna vijiji na tena vijiji muhimu. Naomba Mhe. Mwenyekiti, barabara hii nayo ipewe uzito kwa sababu ina haki na ina watu tena muhimu na inakabiliwa na maeneo muhimu ya wakulima ambao wanaweza kuzalisha katika nchi yetu ili mambo yetu yaende vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa kuwahi muda wako naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Makame Said Juma, sasa namwita Mhe. Tatu Mohamed Ussi, akifuatiwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed.

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Fungu 63 lakini nasimamia kifungu 66. Mhe. Mwenyekiti, tangu jana au juzi humu Barazani tumekuwa tukikiuka kifungu 66 ambacho naomba nikisome.

"Mjumbe pamoja na wajibu alionao chini ya vifungu vya katiba atakuwa pia na wajibu juu ya mambo yafuatayo:

(a) Kulinda hadhi ya Baraza na Kamati zake na kutokujiingiza kwa namna yoyote ile katika vitendo vya makusudi vya kutoheshimu Baraza na kusababisha Baraza au Kamati zake kudharauliwa."

Mhe. Mwenyekiti, Baraza maana yake ni Mwenyekiti au Kiti ama Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti lakini imekuwa utaratibu upo, kiti anamuambia mtu muda wako umekwisha mtu anakwambia aa niachie si utaratibu wa Baraza na unavunja hadhi ya Baraza na mnawaachia watu wanaendelea wanachangia mpaka wanamaliza inakuwa si utaratibu, afadhali mtu umtahadharishe bado dakika zako tatu ili amalize kwa wakati. Kwa hivyo, naomba tu utaratibu huo uwe unafuatwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa lakini itambulike kwamba mtu anapochangia hizi saa mbele zina maana yake kuona kwamba anachangia kwa muda uliopangwa, sasa anapoomba ndio pale nampa dakika mbili kwa uwezo niliopewa na yeye bado anaweza kuchangia, sasa si vyema kubishana nipe mbili au tatu ni nyinyi wenyewe mtekeleze hiyo kanuni. Ahsante.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu wewe ndio mwenye kikao na inavyotakiwa kwa Baraza wewe ukisema jambo mjumbe yoyote akae afuate maelekezo yako. Sasa muda hizi saa zote sio tatizo wewe ndio mwenyewe, ukishamwambia na *hansard* zimo leo tukifuata tutaona kuliko watu watatu unawaambia muda tayari anakwambia umenionea dakika mbili si utaratibu.

Mhe. Mwenyekit: Ahsante tunaendelea Mhe. Tatu Mohammed Ussi.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kusimama hapa muda huu ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii, pia nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kutuletea hotuba yake iliyo nzuri ambayo inasomeka, inafahamika na ina michanganuo aina mbali mbali. Baada

ya hayo, nianze mchango wangu na ukurasa wa nne kifungu cha kumi na moja ambacho kimesema pencheni ya wazee wasiojiweza.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Serikali kuwaona hawa wazee lakini kwa kweli kiwango hichi ni kidogo kutokana na hali ya maisha inavyokwenda hivi sasa. Kwa hivyo, naiomba serikali iwaone wazee hawa kuwaongezea angalau iongezeke mara mbili au tatu zaidi ya kiwango hichi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja ukurasa wa tisa kifungu cha 25 ujenzi wa jengo la mama la hospitali ya Kibweni. Vile vile niipongeze wizara hii kuona kwamba wale wananchi wa kijiji cha Makombeni wameshalipwa fidia zao kwa ajili ya kupata sehemu ya kujenga kituo cha askari wetu wapiganaji KMKM.

Pia nimuombe Mhe. Waziri hili jengo la akinamama la hospitali ya Kibweni limeshafikia hatua lakini naomba liezekwe kwa sababu hospitali ya Kibweni ni hospitali inayohudumia wananchi takriban wa Unguja nzima kwa kupata huduma pale. Niwapongeze wafanyakazi hawa kwa jitihada zao wanazofanya kwa sababu wanafanya kazi usiku na mchana na wala hawachoki.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye mikoa yetu kwanza nichukue nafasi ya kuwapongeza Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wote wa Unguja na Pemba kwa jitihada zao za kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi wakishirikiana na Wawakilishi wetu. Pongezi za pekee nimpongeze Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba akishirikiana na Wakuu wake wa Wilaya ya Chake Chake na Mkoani kwa jitihada zao za kusimamia kwa kikamilifu suala zima la upunguzaji wa dawa za kulevya katika Mkoa wetu wa Kusini Pemba. Namuomba Mkuu wa Mkoa aongeze jitihada hii pamoja na kamati yake ya ulinzi kwa sababu dawa za kulevya ni hatari kwa vijana wetu na tukiliachia hili tutakosa nguvu kazi za taifa.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja ukurasa wa 51 kifungu 141 Baraza la Mji Mkoani. Kwanza, nimpongeze Mkurugenzi wa Baraza la Mji Mkoani pamoja na Madiwani wake kwa sababu bila ya Madiwani hawezi kufanya kazi peke yake. Pamoja na kuvuka lengo hili na mengi waliyoyafanya katika mji wetu wa Mkoani lakini namuomba Mkurugenzi kulisimamia holi letu la Umoja na Nguvu Mkoani ili lifanyiwe matengenezo kwa ajili ya wananchi wa pale kwa sababu tuna shida ya sehemu ya kufanyia mikutano. Kwa hivyo, namuomba Mkurugenzi alisimamie hili kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kwa sababu holi hili waliazimwa Wizara ya Afya wakati walipokuwa wanafanya matengenezo ya hospitali. Kwa hivyo, hili naliomba naamini Mkurugenzi ameshalisikia na Serikali imeshanisikia.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye vikosi vyetu vya ulinzi, kwanza naanza na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM). Nichukue nafasi hii kushirikiana na wenzangu wale waliopongeza na mimi napongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuimarisha majengo yetu ya vikosi vya KMKM. Kwa hivyo, naamini matengenezo haya yataendelea kwa vikosi vyote au sehemu zote wanazoishi wapiganaji wetu ili wapate makaazi yaliyo bora na salama.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikija hapo hapo kwenye vikosi vyetu sasa hivi naingia kwenye Kikosi cha Zimamoto, hiki ni kikosi ambacho kinafanya kazi zake wakati wote kama vikosi vyengine. Nashukuru katika hotuba yako hii katika maboresho uliyoyafanya pale Mkoani pana kikosi chetu

cha Zimamoto ambacho kinafanyakazi vizuri na kwa ufanisi zaidi. Kituo kile kimeboreshwa lakini bado nawaombea wapiganaji wetu hawa kupatiwa eneo la kujenga kituo ambacho kitaendana na wakati. Kwa sababu pamoja na kuwa pale pana kituo chetu cha wapiganaji wetu lakini imekuwa ni *stand* ya magari na magari yote yanaingia mle ndani kwenye uzio wao na inakuwa ni tafrani kwa kweli, hususan wakati meli ikifunga gati pale Mkoani. Kwa hivyo, hili Mhe. Mwenyekiti, mara ile nililizungumza na mara hii nalizungumza tena.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naingia kwenye ugatuzi kwanza niishukuru serikali yetu kwa kuleta huo ugatuzi kwenye elimu ya msingi na vituo vya daraja la chini la afya. Tumeshuhudia maendeleo mengi yakifanywa na tumeona tofauti iliyokuwepo na hivi sasa kwa sababu Halmashauri zetu na Mabaraza yetu ya Miji yanajitahidi sana katika kufanya kazi zake. Sasa basi, kwa sababu tumeona maendeleo ya ugatuzi nilikuwa naomba kupitia ile hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati iliyosomwa jana hapa suala la maji nalo ikiwezekana ligatuliwe. Nasema hivi kwa sababu suala la maji limeigusa jamii sana wanawake wanahitaji kupata maji au binaadam wote wanahitaji maji kila wakati, ingawa Wizara yetu ya Ardhi, Maji na Nishati inajitahidi kwa hili lakini bado changamoto za kupatikana kwa maji vijijini baadhi ya maeneo ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba hilo tu.

Mhe. Mwenyekiti, nikirudi nyuma kidogo nilisahau kuhusu Mkurugenzi na Madiwani, madiwani wanafanyakazi na mkurugenzi sasa nilikuwa nawaombea na wao wapatiwe usafiri madiwani wetu ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mengi yamezungumzwa na wenzangu kwa hivyo sina haja ya kuyarudia isipokuwa tu nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote. Baada ya hapo naunga mkono hoja hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa sasa namwita Mhe. Mohamed Said Mohamed akifuatiwa na Mhe. Hamad Ali Rashid.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri Haji Omar Kheri kwetu Donge tunaita Omari kwa uwasilishaji mzuri sana. Pia niipongeze Kamati kwa utendaji wake na kuripoti vizuri sana chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Machano Othman Said, hongereni sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuanza hotuba yangu ndogo sana kwa kupitia ukurasa wa 15 na nitakwenda tofauti na wenzangu lakini sijui kama nitapata muda wa kuyaeleza yote, nitakwenda mpaka kwenye kile kitabu cha makadirio ya 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 15 namba ndogo 41 Mhe. Waziri alieleza jinsi gani ya kutumia mashine za *electronic.* Kwanza, tumpongeze kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kukusanya mapato kwenye *parking* zote lakini kitu ambacho kilikuwa kikitupelekea kupiga kelele ni jinsi gani tunaweza tukayapata mapato yale yasivuje. Moja, tukasema tutumie mashine za *electronic* na serikali ikatukubalia jambo lile ikasema italianza karibuni, lakini Mhe. Waziri kwenye kitabu chake hichi anasema anasubiri mpaka mashine zile za *ZRB* zitakapokuwa tayari ili waweke mfumo wa pamoja, tuupongeze sana mfumo huu wa pamoja pengine unaweza

ukaleta tija sana. Wasi wasi wangu mdogo sana nilikuwa nikijiuliza au nimuulize Mhe. Waziri wakati anapanga lile kulikuwa hakuna *coordination* katika kufanya kazi hizo serikali tuweze kujua hayo, ikiwa hakuna hii *coordination*.

Lakini jengine nielekee kwenye ukurasa wa 29 wa kitabu hichi Mkuu wa Mkoa wa Mjini kwanza tumpongeze kwa kazi zake nzuri sana. Lakini tuwapongeze na ma-*DC* wake wote aliowachagua Mhe. Rais wa hapa Zanzibar ni askari wa miamvuli na wanafanya kazi zao na niwapongeze sana. Lakini amesema Mkuu wa Mkoa katika kazi zake amewakamata hawa wauzaji wakubwa wa dawa za kulevya. Vile vile nimpongeze kwa kuona ile hoja yangu ya dawa za kulevya niliyoitoa kwenye Baraza lako tukufu ameifanyia kazi kikamilifu.

Hofu yangu nilikuwa nataka nijue tu hawa waliokamatwa wauzaji wakubwa wa dawa za kulevya akina nani kwa sababu nao sio wa kuwaficha, sio siri tuwatangaze ili watu wawajue wahalifu wa dawa za kulevya ni akina nani katika nchi yetu. Kwa sababu visije vikakamatwa vidagaa wakati mapapa yapo, sasa nilikuwa nataka kujua tu.

Mhe. Mwenyekiti, niende Baraza la Manispaa katika ukurasa wa 31 niwapongeze wote na nimpongeze Mhe. Waziri sana alikuwa akisikia kilio changu cha kumtaka ampatie gari jipya Mhe. Meya wa Mjini na tumefarajika kwa sababu tumeona gari jipya sasa Meya wetu analitembelea. Huwezi kufananisha Morogoro na Dar es Salaam hiyo ni kitu tofauti, sasa hapa mjini tunakupongeza sana Mhe. Waziri kwa kutupatia hili. Vile vile tupongeze katika mradi huu wa *ZUSP* wa mtaro ambao umechimbwa Migombani, umechimbwa Mpendae, tunakupongeza sana na tunakwambia tu uvute soksi yako juu ili kazi iende kama ulivyojipangia.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye ukurasa wa 33 niwapongeze Manispaa ya Magharibi "A". Nilikuwa nahisi wakati nilipokuwa nakisoma hiki kitabu nasema kwa nini ile Magharibi "A" tuiite Manispaa na pengine haijawa tayari kuitwa Manispaa. Kwa sababu humu nasoma kitabu kinasema maombi ya eka, sasa mjini kunakuwa na maombi ya eka hichi kitu ambacho kinanipa tabu sana. Hii haijawa tayari kuitwa Manispaa mimi ningemuomba Mhe. Waziri bado tuiite Halmashauri ndio inayoombwa huko Mfenesini na kwengine ndiko inakoomba eka huko, lakini bado hii haijawa Manispaa.

Mhe. Mwenyekiti, niwape hongera sana Manispaa ya Magharibi "B" kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya lakini niwaambie tu wapite na huku Chukwani kuna matatizo, kuna wawekezaji wameweka *parking* kubwa za gari lakini wanamwaga mwaga maji nje inaweza ikawa hatari na sijawahi kuliona dampo lolote au chombo chochote cha kutupia taka huko Chukwani. Sasa Mhe. Waziri niombe sana utakapopata nafasi uwaambie watu wako wapite huku ili tuweze kuona.

Mhe. Mwenyekiti, niende haraka haraka kwenye ukurasa wa 42 Mkoa wa Kaskazini Unguja na kwenye fungu lao hilo D 09, lakini imeeleza kazi zao moja inasema Mkoa umefanya ziara katika Sekta za Utalii ambapo inafanya uhamasishaji wawekezaji wa Mahoteli ya Kiwengwa juu ya umuhimu wa kuchangia miradi ya kijamii. Mheshimiwa hapa nilikuwa na wasi wasi nilikaa na wadau wakanambia kuwa sasa imekuwa Halmashauri ya Kaskazini wanakwenda mara kwa mara kupeleka bakuli kuomba ili wafanye kazi zao. Sasa niombe tu kama litakuwa fungu lao dogo la

bajeti basi tuwaongezee fungu hili ili wafanye kazi kikamilifu tuone basi tumekwenda katika kufanikiwa kwenye jambo letu hili.
Mhe. Mwenyekiti, ningerudi na nikasema tuangalie kwenye ukurasa wa 107 imeelezwa hapa idadi ya wazee waliopatiwa msaada kwa mwaka 2017/2018 tumetumia shilingi milioni 412,560,000/=. Sasa mimi nilikuwa najiuliza baada ya fedha zile ambazo anatoa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, fedha hizi zinatoka vipi na kwa kigezo kipi, tuambiwe mtu huyu analipwa kwa kigezo kadhaa. Lakini anapewa hizi vipi, mimi nimesema zibaki tu, mwenzangu Mhe. Tatu Mohamed Ussi amesema pesa zile kidogo, mimi nasema shilingi 20,000/= ni nyingi sana labda kidogo wanapewa watu ambao hawastahili umri wao bado ni mdogo wanaziona matumizi yake makubwa bado inakuwa kidogo. Lakini na hizi shilingi 5,000/= ambazo wanapewa watu tunahitaji kuzitazama vizuri. Mhe. Waziri nataka maelezo ya kina sana ili niweze kujua pesa hizi zinatumikaje.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwenye kitabu kikongwe hichi cha Makadirio ya Bajeti cha 2017/2018 pana fungu hapa ukurasa wa 3 sidhani kama wewe unayo, lakini nikishakupitisha baadae uje ulitazame fungu hili lilikuwaje. Hili ni Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara ya Maalum za SMZ. Programu ya kwanza ambayo ni PD0101 Uratibu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kupitia programu ndogo ya Tawala za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilikadiriwa kuwa na vikao 15 vya uratibu wa Mikoa, Wilaya, Shehia, lakini katika utekelezaji huo vikao vitano tu ndio vilivyofanya vilivyopata. Ni sababu gani zilizopelekea baadhi ya vikao hivyo kutofanyika chini ya programu hii ambayo ina lengo la kuongeza ufanisi wa shughuli za kiuchumi, kijamii ndani ya mikoa yetu.

Ukizingatia programu kuu hii ilitiwa na bajeti yake asilimia mia moja na humu inaonesha kwenye kitabu kipya na humu kwenye makisio walipata asilimia mia moja. Sasa nilikuwa nataka kujua na fedha ambazo iliombewa ni shilingi bilioni 1,601,000,000/=, vile vile programu hii imeombewa tena pesa kama hizo lakini safari hii imeongezwa na imetiliwa shilingi bilioni 5,102,600,000/=. Lakini kule tuna vikao vilipangwa 15 huku kwenye kiashiria inasema imefanya vikao vitano tu. Sasa nilikuwa naanza kupata wasi wasi ufanisi wake ukoje? Sina nia ya kuzuia fungu leo wala sitaki kuhoji chochote wala sipigi buti, lakini nilikuwa nataka maelezo ya kina sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna programu ya PD0101 Uratibu wa Tawala za Mikoa programu ndogo ya SD010101 pia kupitia viashiria vya utekelezaji wake ilikadiriwa kwa idadi ya ripoti nane katika vikao vya kushirikisha jamii. Vile vile ripoti inaonekana katika utekelezaji wake maana inaonekana utekelezaji wake wa shughuli za Uratibu wa Tawala za Mikoa hapa haikutekelezeka vizuri katika jamii. Sasa nilikuwa nataka hii Mhe. Waziri ipo katika ukurasa wa 3 fungu D001 naomba uitazame vizuri, kwa nini havikutekelezwa na viashiria hivi wewe ndio unayetuletea.

Lakini jengine nataka twende kwenye kifungu SP010101 Uratibu wa Serikali za Mitaa kumekuwa na kiashiria *(indicator)* ambayo kimsingi hakipimiki tofauti na viashiria vyengine

ambavyo vimekuwa vikipanda. Maana hichi kiashiria hizi ni *qualitative* huwezi kuvipima kwa maandishi sasa hapa umetuletea hatujui vipi. Tunaomba tu utwambie kimepimwa kwa kiwango gani na lakini ni ripoti moja tu inaonekana katika utekelezaji wake. Sasa Mhe. Waziri utakapokuja unambie shughuli za Uratibu na Utekelezaji wa Mikoa na Mitaa na kutekeleza majukumu yake katika kuhakikisha jamii inashirikishwa ipasavyo, ningeomba hilo.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba univumilie kidogo kwa sababu nakwenda kwenye bajeti ina viashiria vingi sana, sasa kama niende kwengine basi niende kwengine nikikaribia dakika tano unambie.

Mhe. Mwenyekiti: Dakika mbili. Dakika mbili.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Nashukuru sitavimaliza lakini nataka kwenda tena kwenye kitabu kikubwa hichi. Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na makusanyo ya KVZ kwenye fungu DO6 ukurasa wa 5, wamekadiria kukusanya milioni 60,259,000/= lakini mwaka jana walikuwa na 45 sasa imekuwa kubwa. Lakini ukiangalia sasa wale wamenyang'anywa malindo yao mengi imechukua kampuni ambayo tumeiwekea hapa sheria yake ya JKU. Sasa hawa kwa pesa hizi Mhe. Waziri ni kubwa sana kuendelea kwa sababu hii KVZ ina matatizo sana wakati tukitembelea nilipokuwa katika Kamati yao Mhe. Machano Othman Said tuliona mahanga mengi yapo vibaya. Kwa nini pesa hizi zisiwe *retained* kwao ili wajengee na waweke askari wetu katika hali hii. *(Makofi)*

Lakini nilitaka kuishauri serikali kupitia chombo chako kitukufu Mhe. Mwenyekiti, kuwa lazima askari wetu hawa waangaliwe kufanyiwa bima ya afya kwa kazi kubwa wanayoifanya pengine mtu anakuwa kwenye malindo siku saba mpaka nane, lakini huku mtoto anaumwa inakuwa kitu kibaya sana. Kwa hivyo ningeomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama nitawahi utaniruhusu niingie Mkoa wa Mjini kwenye fungu D07 ukurasa wa 12. Mhe. Mwenyekiti, kuna ada ya ndoa na uhaulishaji wa ardhi na usafirishaji wa vyombo. Mwaka jana walipangiwa shilingi milioni 45,580,000/= lakini mwaka huu hamna kitu, fungu tu kubwa lakini kwenye fungu dogo hili hakuna kitu. Sasa nilikuwa nataka nijue Mhe. Waziri unipe tu kidogo kwa nini tulifanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vifungu vyengine nitaviacha kwa sababu ya kukwepa sana muda wako nisiule, lakini niende kwengine kidogo na naomba mengine Mhe. Waziri …

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda umemalizika.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Naomba mengine Mhe. Waziri nikupe kwa maandishi vifungu vyangu vya ufafanuzi. Nikushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa naomba nimwite Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na ikiwa muda utatosha atafuatiwa na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mjumbe, Mheshimiwa subiri nilishamwita Mhe. Hamad Abdalla Rashid lakini nilichanganya hapa, kwa hivyo Hamad nafasi ya kwako. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi nianze kwa kuwashukuru wenzetu hawa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kuanzia watendaji, Mhe. Waziri sina wasi wasi na watendaji wako wote kuanzia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tawala hadi Wakurugenzi. Kuna majembe mazuri ambayo nina hakika kwa ushirikiano na uongozi wako bora pamoja na Naibu Waziri, basi mtaendelea nayo vizuri na tuna hakika kwamba serikali yetu itapiga hatua kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na vikosi moja kwa moja vyote kwa ujumla. Wenzangu wamesema mengi na mimi nasema kwamba vikosi hivi kama tunavipatia nyenzo na kuimarisha vyote kwa pamoja, mafao yao wakapata kwa wakati, wengine wanalalamika hapa hawana sare wakazipata kwa wakati, basi nina hakika kwa asilimia mia vikosi hivi vitafanya kazi nzuri ambayo watafikia malengo haya ambayo wametwambia hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mambo makuu mawili tu na pindipo utayaweka sawa hayo utakapokuja hapa, na ninakwambia kabisa nina lengo la kuzuia fungu katika hayo mambo mawili kama hukuyaweka sawa. Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza kikosi chetu cha JKU lengo la serikali kama walivyosema wenzangu kipate mafunzo na kiweze kujiendeleza kimaendeleo baada ya mafunzo yale na si vyenginevyo. Narudia tena kwa herufi kubwa SI VYENGINEVYO. Inaonekana kikosi chetu hichi kupitia kambi ya pale kwenye jimbo langu Makao Makuu ya JKU hakifanyi kazi hiyo na kazi yake sasa ni kuuza pombe na kupiga walevi wao, lakini kuzuia huduma za kituo cha afya ambacho kipo ndani ya kambi ile ndani ya baa ile. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani hata siku moja kituo cha afya kikawa ndani ya kambi ya baa ya kuuza pombe, naomba kwa sababu *hansard* zipo na wewe mwenyewe ulitamka bayana hapa na nina matukio zaidi ya saba yaliyosababisha kuhatarisha maisha ya wananchi wa jimbo langu. Naomba sasa utimize ile ahadi yako ulioahidi Baraza hili kwamba ile baa utaifunga pale na nina sababu maalum. Sababu ya kwanza haiwezekani kurudia baa ile kuwa na hospitali pale ndani nyanda moja tu. Tafadhali Mhe. Waziri naomba sasa utimize ahadi yako ambayo uliahidi kwenye Baraza hili.

Lakini jambo la pili kubwa Mhe. Mwenyekiti, mimi nasikitika sana tena sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliitaka wizara hii kwa uwezo mkubwa tu na wananchi wote kwamba ni marufuku ng'ombe kutembea kwenye miji. Mhe. Waziri mimi napenda kusikitika kwamba na sipendi hasa, inaonekana kauli ile ya Mhe. Rais watendaji wako bado hawajaikubali. Hawajaikubali kwa sababu gani? *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Chake Chake ng'ombe wanauzwa ndani ya mji inakuwaje amri ile ya Rais kutekelezwa pale, ikiwa ng'ombe watendaji wako wameruhusu wauze ndani ya mji ule. Sasa nakuomba basi umefika wakati Mhe. Waziri kutimiza ahadi ile ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuondoa ng'ombe wale ndani ya Mji wa Chake Chake, wanatukera, wanatuudhi lakini ni kupinga amri ya Mhe. Rais. Pindipo hutoweka sawa haya mimi nitazuia mafungu haya mawili, hiyo natamka bayana kabisa na nina nia hiyo na nitatimiza lengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho mimi naunga mkono wenzangu walivyosema pale kwamba barabara zetu zimechafuka vibaya sana. Sina nia ya kuondoa fungu la *CCTV camera* lakini sababu Waziri wa Fedha nae yupo hapa imefika wakati sasa kuona kwa sababu barabara na mvua zilizonyesha kubwa sana, barabara zetu zimechafuka vibaya mno na ni jambo la aibu. Hata Mhe. Makamo wa Rais akipita pale Ben Bella kwa kweli inachukiza, haipendezi, wala haileti maana. Ni barabara mbaya mbovu zimechimbuka. Kuna haja sasa kwa nguvu zako zote kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji barabara zetu za mji na mitaa ziwe nzima haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, sitaki kuupoteza muda hata kuutimiza sawa sawa, naomba kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia na nasema tena kwamba asilimia mbili naibakisha utakapokuja kueleza majibu hayo. Ahsante Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mheshimiwa sasa namwita Mhe. Mtumwa Peya Yussuf kumalizia muda uliobakia.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanazozifanya za kuweza kutuwekea ulinzi katika nchi yetu. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru na niwapongeze sana Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, pamoja na Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Zanzibar. Hasa ukiangalia katika Mkoa wa Kaskazini Unguja nimpongeze sana Mkuu wangu wa Mkoa, lakini pia nimpongeze sana Mkuu wangu wa Wilaya aliyechaguliwa hivi karibuni, nimpongeze wa dhati kabisa na nimwambie kwamba ile *speed* aliyokuja nayo basi asije akaikatisha njiani aendelee nayo. Nimuombe sana kumwambia kwamba wale ambao wanamwambia serikali hii hawaitambui azidi kuwawekea mkakati ule ule waweze kuitambua hii serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia niwashukuru na niwapongeze sana vikosi vyetu vya SMZ kwa kazi kubwa wanazozifanya. Nianze moja kwa moja kikosi vya KMKM katika kitabu hichi kinaonesha D04 kuna kuimarisha haya majengo yao ya KMKM. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana walipangiwa fungu hili hapa la kupewa shilingi milioni 1,400,620,000/= lakini bahati nzuri hawakukamilishiwa zote walipata pungufu na mwaka huu walikadiriwa kupewa shilingi milioni 1,300,000,000/=. Niombe sana haya makadirio waliyopewa kwa mwaka huu wasipunguziwe isipokuwa wapewe hichi kiasi ambacho wamepangiwa kwa sababu wenzetu hawa tunawaona kazi kubwa wanayoifanya kuimarisha yale majengo yao.

Lakini ukiangalia Mhe. Mwenyekiti, katika majengo haya ya KMKM, kuna kambi ya KMKM iko Mnarani Bumbwini na Mhe. Waziri nimuombe sana, wale vijana wetu wanafanya kazi kubwa lakini lile eneo wanalokaa halistahiki kwa sababu ile nyumba wanayokaa ni banda ambalo limezungushwa bati lote kuanzia pembeni mpaka kuezeka. Kwa hivyo, huwezi kutambua wakati wa joto wala baridi kwa kweli wale wamo kwenye mazingira magumu sana. Niwaombe sana baada ya kupitishwa bajeti hii Mhe. Waziri uwafikirie wale japo banda la chumba cha vyumba viwili uwawekee kwa ajili ya kuweza kufanya kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja jengine mradi wa kujenga jengo la kinamama na watoto pale Kibweni. Niwapongeze sana askari wetu wa KMKM kwa huduma wanazozitoa kwa matibabu kwa kweli wanafanya kazi ngumu sana na kazi kubwa sana, na pale likimalizika jengo lile mtapunguza hata ule msongamano wa kinamama na watoto kule Mnazi Mmoja. Kwa sababu sasa hivi ukenda Mnazi Mmoja waja wazito watatu wamelazwa kitanda kimoja na wengine wapo chini kwenye magodoro, utamkuta mama kajifungua kinamama watatu na watoto wao wanalala kitanda kimoja. Kwa hivyo, likimalizika jengo letu lile pale la Kibweni tutapunguza ule msongamano uliokuwa si wa lazima kule Mnazi Mmoja.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kwa kuongezea hapa lazima kupatikane vifaa muhimu katika hospitali ile kwa sababu sasa hivi unakwenda kupata huduma pale lakini kama nilivyosema mwaka jana na leo nalirejea tena hapana *x-ray*, hapana *CT scan*, hapana vipimo muhimu vyote

ukiangalia sasa hivi ile hospitali ni kubwa na inaendelea kuongeza huduma za afya. Kwa hivyo, niombe sana vifaa hivi kwa hospitali ile waweze kupatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye Mradi wa Mageuzi wa Serikali za Mitaa. Hapa Mhe. Mwenyekiti, hili fungu walilopangiwa kwa kweli ni dogo kwa sababu hawa wana kazi nyingi sana na ukiangalia hizi fedha wanazopewa ni kidogo. Baada ya kuja huu ugatuzi mambo yamehamia kwao lakini ukiangalia kwenye vituo vya afya vyote vilivyomo huduma nyingi sana zinakosekana. Kwa hivyo, lazima hili fungu lizingatiwe waongezewe kifungu ili waweze kuhimili kuweza kuendesha hizi huduma ambazo zimeingia kwao hawa Serikali za Mitaa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwa sababu hawa Halmashauri wana kazi ngumu na wana wakati mgumu fedha wanazotiliwa ni chache lakini kazi wanazofanya ni nyingi sana. Kwa hivyo, hizi fedha wanazozitiliwa haziwatoshi lazima waongezewe.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja jengine suala la hizi barabara za ndani. Mhe. Mwenyekiti, mvua zilizopita kutoka Bumbwini, Pangatupu, Mahonda barabara ile imeharibika sana na bahati nzuri aliyekuwa Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji alikwenda kuiona barabara ile na aliahidi kuitengeneza. Lakini bahati nzuri hadi leo haikufanyiwa matengenezo yoyote, hizi mvua zinazoendelea kunyesha hivi sasa ile barabara kwa kweli haifai, haipitiki na ina hatari. Ukiangalia kule Pangatupu kuna skuli na walimu wote sasa hivi wanatoka maeneo ya juu ndio waende pale, kwa kweli wanafunzi wanakosa huduma muhimu kwa sababu walimu wanashindwa kufika katika eneo lile. Nimuombe sana Mhe. Waziri tukimaliza bajeti hii tutoke pamoja mimi na yeye Mkuu wa Wilaya yangu pamoja Mkurugenzi wa Halmashauri tukaione barabara ile ilivyo na sio kwenda kuiangalia tu, tuipe kipaumbele tuifanyie kazi, tuhakikishe ile barabara inaweza kutumika. Kwa sababu ukiangalia sasa hivi mwananchi wa Pangatupu anashindwa kuja Bumbwini na hakuna njia mbadala pale kama utatengeneza ya kusema wapate huduma ya dharura, hakuna sehemu nyengine yoyote ambayo inapitika. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili tulichukulie kwa umuhimu wake na tuweze kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la uajiri Wizara ya Elimu …

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda umemalizika. Naomba niwajulishe wachangiaji wa jioni watakaoanzia. Kwanza kuna dakika zako tano utamalizia kama utaona kuna umuhimu huo, lakini pia atafuatiwa na Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil kwa wakati wa jioni.

Baada ya hayo, niwashukuru sana kwa kuendelea kuchangia hotuba hii na kuiunga mkono vizuri. Naomba niakhirishe kikao hichi hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea labda nitoe maelezo machache kidogo, tuna orodha kubwa sana bado ya wanaotaka kuchangia. Nakusudia nilivyosema asubuhi nilisema kwambaWajumbe wote wachangie ule wakati wa asubuhi kuanzia sasa hivi Laasiri nianze kuwaita baadhi ya Mawaziri, lakini nashawawishika sana hata kama kwa kupunguza muda hao Wajumbe ambao wamebaki wachangie. *(Makofi)*

Waheshimiwa nitakachokifanya nitakupeni dakika tano tano, jipangeni vizuri kwa sababu najua ukipata kuchangia baadhi yenu mtapata kuelekeza vile vifungu ambavyo Kikanuni mtakuwe na uwezo wa kusimama na kuhoji wakati ule wa kupitisha vifungu. Nitashawishika sana niwape Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu lengo hasa ni kwa ajili ya wananchi na nyinyi ndio Wawakilishi wao.

Lakini kwa baadhi ya Mawaziri ambao wameomba kwa sababu Mawaziri hawa baadhi yao wana Bajeti zao zinakuja basi masuala yale ambayo wanataka kuyachangia kuyazungumza wayazungumze wakati wa Bajeti yao, kila Waziri kwenye Bajeti yake. Mawaziri wenye *portfolio* nitawanyima kuzungumza hivi ili niwape Waheshimiwa Wawakilishi waweze kuchangia na pia kumpa nafasi nzuri zaidi Mhe. Waziri kuweza kujibu hoja mbali mbali ambazo zimetolewa na Wajumbe. Kwa maana hiyo nitawaita baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi na nitawapa dakika tano tano.

Mhe. Naibu Waziri wa Wizara yeye nitampa muwa wake wa kawaida, kwa hivyo atachangia kama kawaida wanavyochangia Manaibu Mawaziri kabla hajachangia Mhe. Waziri husika. Mhe. Waziri wa Fedha nitamruhusu pia.

Baada ya machache hayo naomba sasa tuendelee na mchangiaji wangu wa mwanzo atakuwa Mhe. Salha Mwinjuma akifuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abdul Wakil. Naam Mhe. Mtumwa Peya Yussuf.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Samahani Mhe. Mtumwa ulimalizia, nakuomba utumie dakika tano kumalizia lakini dakika tano hizo hizo watatumia wale nitakaowaita baada yako. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf samahani sana unaweza kuchangia sasa.

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuniruhusu niendelee nimalizie pale nilipofikia.

Mhe. Spika, nilifikia na naendelea na Chuo cha Mfunzo. Mhe. Spika, tukiangalia Chuo chetu cha Mafunzo tuna fani fofauti ambazo tunazifanya pale kwa ajili ya kukuza uchumi ndani ya zile kambi zetu. Ukiangalia ndani ya Kambi ya Mafunzo ya Mafufuni ile kambi kwa kweli ina

wataalamu wa kilimo lakini pia ina wataalamu wafugaji wa samaki. Ukiangalia pale mabwawa yale ya samaki yapo tokea asili, lakini shughui zile zimeachwa ambazo shughuli zile ndizo zinazoweza kuwapatia kipato kikubwa wale watu wetu wa mafunzo waliyokuwepo pale kwenye kambi ile. (*Makofi*).

Nimshauri Mhe. Waziri lile suala la pale Kambi ile ya Mafufuni naomba tulirudishe tena kwa ajili ya kufanya zile kazi za kilimo cha mboga mboga, kilimo cha muhogo tulikuwa tukipata muhogo mzuri pale, kilimo cha samaki na kilimo cha chumvi, vitu hivi vyote vilikuwa vikifanyika ndani ya kambi ile. Nimuombe Mhe. Waziri lile suala lirudi tena.

Jengine Mhe. Spika, kwenye suala hili la ugatuzi limefikia kwenye suala la Wizara ya Elimu. Mhe. Spika, kuna hili suala la kupewa uhamisho kwenda kila baadhi ya skuli. Niombe sana Wizara izingatie na iangalie uwiano wa kila skuli kwa sababu utakuta skuli inaondosha walimu lakini yanaachwa madarasa walimu hapana, utakuta skuli nyengine kunapelekwa walimu ambao ni wa ziada, unakuta hata vile vipindi vyao havitoshelezi, yaani wamekaa kitako hata kazi za kufanya hawana. Kwa hivyo lazima tunapofanya uhamisho huu tuzingatie ule uwiano wa skuli na skuli.

Mhe. Spika, ukiangalia kuna hawa Maafisa wa Elimu ya Wilaya ambao wapo ndani ya Wilaya zetu, unaweza kufanywa uhamisho huu yule Afisa wa Elimu Wilaya hajui kinachoendelea, anatoka mtu na barua yake moja kwa moja Wizarani anaipeleka skuli anahama, anaondoka pale Afisa Elimu hajui nini kinachoendelea. Kwa hivyo hawa tumewaweka kwa madhumuni maalum kwamba wasaidie ndani ya Wilaya zetu, hivyo lazima na wao wawajibike na pia washirikishwe kwenye mambo kama haya yanapofanyika, vyenginevyo hawana faida ya kuwepo kwenye Mawilaya, wamewekwa wanafanya kazi gani.

Jengine Mhe. Spika, nimwambie Mhe. Waziri wa Elimu kuna tetesi ndani ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani hawa walimu watakwenda skuli kama kawaida, tumezoea huko nyuma walimu Mwezi wa Ramadhani wanafungiwa skuli. Mimi nilitaka kuuliza hili suala sijui kama ni kweli au ni mazungumzo tu. Kama ni kweli hawa walimu wanawake sijui tunawafikiria vipi wakati wanaingia skuli asubuhi na jioni na kutoka saa 12, hizi futari watawapikia waume zao sijui saa ngapi na watoto watawahudumia saa ngapi. Hili Mhe. Waziri ukija naomba utusaidie kwamba hili suala lipo kweli na kama halipo basi pia utatwambia lipo vipi.

Mhe. Spika, la mwisho nizungumze suala hili unapofanya tena uwajiri. Kuna walimu unamuajiri anakuja skuli pale akifika anakwambia mimi nimepangiwa vipindi katika skuli nyengine na huku umeshamleta katika Skuli nyengine, ina maana katika wiki anaweza akaja pale siku tatu siku mbili hayupo, ile siku atakayokuja atafanya kazi kujionyesha kwamba yeye tayari yupo pale na anafanya kazi, lakini siku mbili hayupo pale yupo kwenye skuli nyengine anafanya shughuli nyengine. Naomba hili suala nalo tuliangalie na pia tuone watu hawa wameajiriwa kwa utaratibu gani na inakuwaje kutokezea masuala kama haya.

Jengine la mwisho utakuta kwenye uwajiri mwalimu ndio kwanza yupo chuo anaajiriwa anakuja skuli baadhi ya siku na baadhi ya siku hayupo yupo Chuoni, wakati huku nje kuna vijana wengi ambao tayari wameshasoma na wanaweza kufundisha masomo yale, sijui kwa nini hawawezi

kuajiriwa wale wakafanya kazi unakwenda kumchukua mtu aliyekuwepo Chuo unamleta pale. Sijui mategemeo yako unategemea iwe vipi pale na anafundisha kwa muda gani.

Mhe. Spika, kwa hayo machache nishukuru tena na nimshukuru sana Mhe. Waziri lakini niombe tu yale ambayo wenzangu wameyazungumza, Waheshimiwa Wawakilishi tumeyazungumza humu ndani yachukuliwe na yafanyiwe kazi, sio tukitoka humu ndani tuwachiwe sisi wenyewe, tumeyaleta kwenu nyinyi ndiyo msaada wetu sisi. Majimboni tunaonekana tumefanya kazi hii na tunapiga kelele na tunasema. Tunachokiomba serikali iyashughulikie yale yote ambayo tumeyawasilisha hapa na tuyafanyie kazi kwa kushirikiana ili tuweze kuwaondoshea wananchi wetu hizi changamoto zilizowakabili.

Ahsante sana Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Mwisho naunga mkono hoja asilimia mia. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana, sasa namwita Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma atafuatiwa na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini ajiandae.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kuniona na kunipa nafasi ili na mimi niwe mchangiaji katika hotuba hii.

Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Kamati kwa ujumla na watendaji wake wote wa Wizara hii kwa kuweza kushirikiana kuiyunga Bajeti hii ikiwa salama na ikiwa inaeleweka.

Mhe. Spika, nianze pongezi zangu kwa Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, nampongeza na kumshukuru kwa kutuona kwamba vijana tunafaa, tunaweza na kutuamini kwa kutupa nafasi mbali mbali wakiwemo Manaibu Waziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, lakini kizuri zaidi hivi karibuni amemteuwa Mheshimiwa *DC* wa Wilaya ya Kaskazini ‘B’ ni kijana, *DC* mpambanaji, *DC* jembe, nikaamini kwamba *DC* huyu anaweza kupambana wakati wowote. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia niendelee kuwapongeza Wakuu wetu wote wa Mikoa, Wakuu wetu wa Wilaya lakini sana Mkuu wetu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Nampongeza kwa kupambana kwake lakini nampongeza kwa kasi ambayo amekuja nayo kwenye Mkoa wa Kusini kwa kuwaletea wananchi wa Mkoa wa Kusini maendeleo. Mhe. Spika, hili nimeona niliseme kwa vile mabosi wetu hawa wanashirikiana na sisi bega kwa bega kuona wananchi tunawatatulia changamoto zao katika maeneo yao. Tukiangalia kwenye Wilaya ya Kati, lakini Wilaya ya Kusini pia nayo haijabaki nyuma inashirikiana vizuri katika kutatua changamoto za wananchi wake.(*Makofi*).

Mhe. Spika, niendele kuupongeza Mkoa wangu kwa jitihada zangu nzuri kwa kuweza kukusanya mapato na kuvuka asilimia 100, imevuka malengo ambayo yamewekwa. Kiufupi Mkoa wa Kusini umefanya vizuri sana kwenye makusanyo. Pia niombe na Mikoa mengine ituige sisi ili tufikie malengo.

Mhe. Spika, moja kwa moja niende kwenye michango yangu nianze kwenye kesi za ugatuzi. Naamini kwamba serikali lengo lake ni jema sana na zuri lakini kwenye kezi ya ugatuzi bado kuna changamoto nyingi sana. Changamoto ya kwanza majengo chakavu, ukiangalia kwenye maskuli maskuli chakavu, mahospitali chakavu, lakini ukiachilia hiyo vitendea kazi navyo pia shida.

Mhe. Spika, tukiangalia kwenye kesi ya kilimo na elimu pia hatuna wataalamu wa kutosha, wataalamu waliokuwepo ni kidogo, lakini hawa pia hawawezi kutusaidia katika Mkoa wetu wa Kusini kama Mkoa mzima tukiwa tuna wataalamu kidogo. Mhe. Spika, ukiangalia kwenye bajeti iliyopita tumewapa bajeti siyo kubwa lakini cha kusikitisha bajeti hii safari hii imepunguzwa baada ya kuongezeka. Kwa hivyo akija Mhe. Waziri aje kutueleweshe vizuri, kuona kwamba bajeti hii ambayo imepangiwa Mkoa wa Kusini na katika Halmashauri ya Wilaya ya Kati na Wilaya ya Kusini tuone wanajiendesha vipi katika *situation* hii ya ugatuzi.

Mhe. Spika, kiujumla nizipongeze na nizitake sana Halmashauri zetu zote na Mabaraza ya Manispaa katika sheria zao ndogo ndogo. Kwenye kutunga sheria zao ndogo ndogo…..

Mhe. Spika: Dakika moja imabaki.

Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma: Mhe. Spika, niwaombe sana katika Mabaraza haya ya Manispaa na Halmashauri zetu tujaribu kutunga sheria ili tuone vijana wetu *atleast* kuwagaia baadhi ya asilimia katika michango yao, ili vijana hawa na wao waweze kujiendesha katika masuala yao.

Mhe. Spika, kwenye kesi za uwajiri katika sehemu mbali mbali za Manispaa na Halmashauri niwaombe sana watu wa Halmashauri, zinapotokezea nafasi ambazo wanaziweza vijana wetu basi wawaangalie kwa macho mawili, vijana wa maeneo husika wawatizame na wawape vipaumbele ili kuona ufanisi wa kazi katika mazingira yale unafahamika.

Mhe. Spika, kabla sijamaliza dakika zako naomba niende moja kwa moja kwenye Vikosi vya SMZ. Hili nimesema nilisemee, kwanza tuipongeze serikali kwa kuboresha miundombinu mizuri ikiwemo majengo na mambo mengine.

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa muda wako umekwisha. Waheshimiwa jipangeni vizuri kwa sababu muda ni mfupi sana. Kwa hivyo mngepunguza kupongeza mkaenda moja kwa moja kwenye hoja.

Naomba sasa nimwite Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil atafuatiwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na Mhe,. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Spika, jioni hii kwa kuniona na kuwa ni mchangiaji wa pili namshukuru Mwenyezi Mungu.

Mhe. Spika, awali ya yote naanza na kusema kwamba bajeti hii nimeikubali asilimia mia moja *no doubt*. Nakuja katika mambo madogo madogo ambayo nashauri kama yafuatavyo. Katika

bajeti hii nimejaribu sana kuisoma nukta kwa nukta na nawapongeza wote walioiandaa kitaalamu akiwemo Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu wa Wakurugenzi wote.

Katika kitabu hiki kuna *concept* ya ugatuzi, sijaona pahala ambapo serikali imedhamiria kununua zana za kufanyia kazi kwa ajili ya usafi kama greda, kijiko na skaveta. Tuelewe wazi kwamba kuna *concept* ya kwamba utalii kwa wote na hali ya usafi ni miongoni mwa jambo muhimu katika mji wetu ili kuvutia watalii. Nimeshuhudia mara kwa mara wakiwa wanaomba omba au kuazima azima vijiko na greda. Kwa hivyo kupanga ni kuchagua, wajiandae na ununuzi wa zana hizi na hasa tukitilia maanani kwamba barabara ndogo ndogo mzigo karibu unawajia wao, hivyo waanze kwanza kujipanga ili waweze kununua zana hizo.

Mhe. Spika, *concept* ya pili napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi kwa uteuzi wake wa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'B'. Mhe. Rais hakukosea na kajipanga sawa sawa na kwa hakika sisi sote tunatumaini kijana atafanya kazi nzuri kwa huko safari yetu tunapokwenda.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, mimi vikosi vyote vinafanya kazi vizuri, makamanda wote wanafanya kazi vizuri na wamejipanga vizuri na kitabu chao kizuri na muelekeo wao kadhalika ni mzuri katika kufanya vikosi vyetu viwe vinaaminika na viwe vya kisasa.

Ahsante sana Mhe. Spika, nimemaliza shukurani.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil asante pia kwa kutuokolea muda. Naomba sasa nimwite Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini atafuatiwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Ali Khamis Bakar ajiandae.

Mhe. Mwinyihaji MKakame Mwadini: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipatia wasaa huu mchache kuchangia hotuba hii muhimu ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum.

Mhe. Spika, na mimi ipo sentensi moja tu, nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kuiongoza Wizara hii kubwa sana na ndiyo yenye uhai katika Mikoa yetu Wilaya pamoja na Shehia. Naomba moja kwa moja niende kwenye buku kubwa ukurasa wa B07 ukurasa wa 14 ambao unazungumzia Mradi wa PD 0702 Uendeshaji na utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia na ninazungumza Mkoa wa Mjini/Magharib kwa niaba ya Mikoa mengine, *figure* zinatofautiana lakini maelezo nitakayoyasema yote yanawiyana na yana *apply* kwa Mikoa mengine.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha juu yake PD0701 kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa zimetengwa pesa za kusimamia serikali ya Mkoa, lakini kifungu PD0702 kimetajwa tena uendeshaji na utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia. Sasa hoja yangu iko hapa, Mheshimiwa kwa nii tena Mkoa wana vifungu vyao vya uendeshaji kwenye Mkoa, kwa nini tena wateremshiwe kwenye PD0702 na yaingie kwenye pesa za Wilaya na Shehia.

Mhe. Spika, tumefanya ugatuzi na kama ugatuzi na kama ugatuzi madaraka yateremshwe Wilayani, kwenye Wadi, mpaka kwenye Masheha. Lakini sasa kama Mkoa wana jukumu la kuzuia pesa, Wilayani haziteremki wanawagaia wanavyoona wao inafaa, nafikiri hivyo sivyo Mheshimiwa. Kama tumeamua kugatua gasi tugatue kweli kweli mpaka pesa. Nataka nishauri Mheshimiwa kwenye mikoa yote nimeona hili lina-*apply,* kama tumeamua kugatua basi pesa na watengenezewe *sub vote* zao, wapewe pesa watumie kwa mujibu, kwa sababu wao ndio wametenga majukumu tutatengeneza moja, mbili, tatu lakini pesa waende kwa Mkuu wa Mkoa wakaombe mzee tupe hichi kwa kweli haipendezi. Kwa hivyo kufanikisha utendaji kwa Wakuu wetu wa Wilaya pesa Mhe. Spika, tunashauri sana ziteremshwe, zigatuliwe.

Mhe. Spika, sambamba linaendana na hilo nimeangalia kwa watenda kazi sikuona ajira za wahasibu, nimefatilia sana unaona wahasibu kila Mkoa yupo mmoja mmoja kwa miaka yote mitatu, kwa nini Wahasibu wasiajiriwe, waajiriwe ili waende kule wakasimamie vizuri mapato na mengineyo, ni lazima tugatue kivitendo. Naomba niondoka hapa nirudi kwenye kitabu kidogo kwenye mapato ukurasa wa 83 na hii ina-*apply* mpaka 88, yaani D01 mpaka D012. Mhe. Spika, hapa naomba Mhe. Waziri anisikilize vizuri kwenye makusanyo mapato yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2017/2018 ukurasa wa 83 wa kitabu chetu.

Mhe. Spika, *column* ya kwanza inasema makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2017/2018, *fine* Shs.781,000/-, halafu makadirio ya makusanyo Julai/March, 2018 *column* ya pili lakini *fiqure* ndio hiyo hiyo, *column* ya tatu makusanyo halisi *actual* Julai/March 2018. Sasa suala langu lipo hapa asilimia makusanyo kwa mwaka imewekwa sabini na saba imepatikana vipi hii. Lakini mbele kuna asilimia makusanyo Julai/March asilimia 77 tena sasa tukamate ipi.

Mhe. Spika: Dakika moja imebakia Mhe. Dkt Mwinyi Haji Makame umemaliza.

Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame: Ahsante, eeh! namalizia Mhe. Spika. Sasa naomba sana kuanzia ukurasa huo wa 83-88 namuomba sana Mhe. Waziri kuna *figures* hazi *tally*, haziendi vizuri kabisa naomba azicheki. Mwisho kabisa naomba kumalizia.

Mhe. Spika, suala la ulinzi na usalama hasa wakulima wetu, visoko vya barabarani vya mazao vimezidi kwenye Wilaya zetu, utakuta watu wameweka ndizi, muhogo, nazi hasa nazi na mwezi Mtukufu Ramadhan unakuja kuna wengine sijui wanafunga vipi lakini utakuta wanaiba nazi wanakwenda uza. Sasa naomba sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa turudishe utaratibu wa zamani Masheha kutoa vibali ili mazao yapelekwe sokoni.

Mhe. Spika, leo tumemkamata mtu Mazizini hapo kaiba ndizi tatu alfajiri, tunatoka Msikitini kaiba ndizi tatu anapeleka sokoni. Mhe. Spika, naomba kuuliza sana suala la ulinzi na usalama wa mazao yetu kwa wakulima.

Mhe. Spika nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia moja ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini. Naomba sasa nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa ninakuona umenyanyuka. Mhe. Ali Khamis Bakar atafuatia na Mhe. Hidaya Ali Makame ajiandae.

Mhe. Miraji Khamis Mussa, ahsante Mhe. Spika kwa kunipa nafasi na naomba nende moja kwa moja kwenye mchango wangu kwa sababu hakuna shukurani kwa dakika zangu.

Mhe. Spika, mimi naomba nende kwenye Mabaraza ya Miji, mchango wangu na utakwenda kwa ujumla kwa sababu nilipokuwa nafuatilia baadhi ya michango ya Wajumbe kwa kuwa sana wanajaribu kumshauri Waziri baadhi ya mambo yatendeke kwenye baadhi ya Manispaa zile tatu nakusudia Mjini, Magharibi "A" na Magharibi "B".

Mhe. Spika, mimi naomba niizungumze Manispaa ya Mjini, imekuwa ikukumbwa na kadhia kubwa sana hasa vile vianzio vyake mara nyingi taasisi nyengine zimekuwa zinawaingilia na mara zinahamishwa. Ninakukumbuka mara ya mwanzo zilihamishwa *driving license* pale na zikaambiwa tu katika sura nzuri kwa serikali inakwenda kuandaa mfumo bora na mfumo huu baada ya muda ukikamilika, basi zoezi hili litarudi, halikurudi tena. Maana yake katika sura ya kawaida kweli pesa zote zinaweza zikakusanywa na taasisi ya *ZRB* lakini hizi makubaliano na mfumo hasa wa uhamishaji ulikuwa na sura hiyo. Mpaka leo hatuoni kurejeshwa kwa kianzio kile lakini leo hii kuna lugha zilikuwa zinazungumzwa humu, kwa kuwa kuna uhamishaji wa yale masoko wenzetu wanaomba yatoke kunako eneo la Manispaa ya mjini yaende kunako Manispaa nyengine.

Mimi nilikumbushe tu Mhe. Waziri, masoko haya kwa sababu na yeye alikuwa mfanyakazi mwenzetu pale yalipatikana kwenye utaratibu wa urafiki hasa soko la Mombasa, urafiki baina ya China na Manispaa Mjini, katika utaratibu wao likajengwa soko hili. Lakini soko la Mwanakwerekwe na upatikanaji wake pia ulikuwa katika utaratibu wa kuandika mradi wa kuwasaidia vijana katika kuwasaidia vijana kwenye kujiajiri kwenye kupitia ufadhili wa *UNDP*.

Lakini Manispaa wenyewe wameandika mradi na wakatafuta eneo wakajua sasa tunakwenda kuwekeza wapi, wamekwenda kuwekeza Mwanakwerekwe. Sasa leo kuna watu wanakuja kudai masoko haya yamo ndani ya eneo la Magharibi yahamishiwe kwenda Magharini, mbona hatufikiri kuhamisha benki, maana iko Mwanakwerekwe na imeekeza katika utaratibu wa Magharibi lakini kwenye sura ya kawaida basi Manispaa yenyewe imiliki soko kama utaratibu wa sasa hivi ulivyo. Sasa kuna huduma za uendeshaji kama wafanyabiashara wa ndani si wanakata leseni, Manispaa husika kwa sababu eneo lao wachukue leseni zao lakini uendeshaji ubakie kwa wenye mradi wenyewe. Sasa haiwezekani leo tunakwenda katika utaratibu wa kuonekana Wajumbe wanasimama wanamshawishi Waziri eneo moja hili liondoke kwenye eneo jengine hatuwezi kwenda katika utaratibu huo.

Mhe. Mjumbe Fulani: Hiyari yetu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Waziri kwenye eneo hili sisi tunasubiri majibu yatakayokwenda na kuingia akilini vyenginevyo na sisi tutazuia fungu mpaka kieleweke. Maana utaratibu wa kawaida Manispaa yenyewe inasema ya Magharibi "A" na Magharibi "B" wana uwezo wa kuwekeza Mjini. Kama wana jengo wanaweza kujenga na waka *invest* wana uwezo huo, zile taratibu nyengine zitafuatilia lakini kwenye eneo hili nasema Mhe. Spika, ninasubiri katika majibu.

Nakwenda kwenye ugatuzi haraka haraka kumalizia dakika zangu. Mhe. Waziri na hapa nisikilize, kuna kijana mmoja anatokea Skuli ya Upenja, *primary* amesomesha muda wa miaka miwili kwa kujitolea. Walimu na viongozi wa skuli ile ukichanganya na Kamati kwa ujumla wakenda Wizarani zimetokea ajira nyingi wakamuombea lakini hakubahatika. Lakini wakatoa muongozo wako vijana waliojitolea tunawafikiria na huyu kajitolea kwa miaka miwili, imeandikwa barua imekwenda Wilayani katika Halmashauri na utaratibu husika wakaambiwa huyu sasa tutamchukua katika utaratibu ule ule wa makubaliano na Wizara kwa sababu ndio iliyotoa maelekezo hayo.

Mhe. Spika, kinachoshangaza kunako eneo hili kaletwa mtu wao wenyewe skuli ya Upenja wakashangaa, wakasema katika utaratibu huu huyu vipi, walipokwenda kuuliza Wilayani mbona mnatuchanganya watu wa Upenja, huyu ndio mliyetuletea nyinyi na sio sahihi,

Mhe. Spika: Bado dakika moja Mheshimiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, hakuletwa kabisa na huyo ambaye alitumikia pale anaitwa Zeyana Mohammed Mussa, na barua zake zote za maombi zipo taratibu zote zilifuatwa, lakini nasema cha kushangaza eneo hilo. Sasa kuna ruzuku humu ya Halmashauri ya Wilaya hii wafike pahala tupate majibu yanayostahiki vyenginevyo kwenye hili hatuwezi kwenda katika utaratibu huo. Mtoto wa kinyonge kajitolea utaratibu umefuatwa leo Halmashauri wanakwenda kufanya wanachokitaka wao, maana hichi kilichoombo kwa mujibu wa utaratibu hawakukielekeza. Sasa huo sio utaratibu mzuri, wasipewe watu madaraka yale yanayotakiwa kufanywa maana yake wao wakafanya kinyume na utaratibu mwengine.

Mhe. Waziri mimi sina tatizo na bajeti yako kunako maeneo yote lakini maeneo haya mawili majibu yake nayasubiri na mimi naomba kuchangia hutuba hii kwa asilimia 50 na 50 nabakisha (*Makofi*)

Mhe. Ali Khamis Bakar (Doholo): Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo kuweza kuchangia ripoti hii au bajeti hii ya Tawala za Mikoa.

Mhe. Spika, mimi niende haraka haraka nianze kuwapongeza Wizara kwa mashirikiano yote ambayo wametupatia kuanzia Waziri na Naibu Waziri na watendaji wake wote lakini pia Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote, lakini vile vile Vikosi vyetu vya Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa walioifanya wakati tukiwa kwenye Kamati na kutoa mashirikiano ya hali ya juu.

Mhe. Spika, mimi niende haraka haraka katika mchango wangu nianze kwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kumjaalia Mkuu wa Mkoa huyu jembe ambaye anasimamia vyema majukumu yake nimpongeze sana, lakini pia nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kazi kubwa aliyoifanya kuweza kuvuna miti ya mipira kwa ajili ya uundaji wa viti na meza. Kwa hivyo hapa nimuombe Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba aige nyayo hizi za Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ambaye alivuna miti hii ya mipira kwa

ajili ya uundaji wa viti na meza maskulini, nimwambie tu Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kama na sisi tunayo mipira katika eneo letu haina faida yoyote imekaa tu watu wanajivunia ovyo hata mapato hayapatikani serikalini. Tuiombe mipira ile na sisi tuweze kuunda viti na meza ili skuli zetu kupitia Mkoa wa Kaskazini Pemba ziweze kupata viti na meza.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nikienda haraka haraka nije katika suala la magari ya zimamoto. Mhe. Spika, magari haya yapo mazuri tena mapya ambayo yamepatikana lakini bado magari haya yamekaa yanapigwa na jua na mvua hayana eneo maalum la kuwekwa magari haya na badala yake, baada ya kupata mapya tutakuja kupata vipuri. Mhe. Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri afanye taratibu zake zote ili kuona magari haya yanapata sehemu ya kukaa yaani zile *parking*.

Mhe. Spika, lakini vile vile kuhusu Vikosi vyetu, navipongeza sana kwa kazi kubwa wanayofanya lakini niende katika Kikosi cha Valantia. Hapa nimeangalia katika kitabu kimeambiwa kwamba kikosi cha Valantia kikusanye Shs.45,530,000. Mhe. Spika, makusanyo haya ni makubwa wakati Kikosi hichi nimekwenda kukitembelea katika Kamati pale Ndugukitu, majengo yao ni mabovu, hawana ofisi na hata yale mabanda ambayo yamekusudiwa kukaa wale askari kwa ajili ya kutoa huduma, kwa kweli hali hairidhishi. Mimi nilikuwa hapa niombe tu au nitoa ushauri kwamba ile sehemu kwa kweli kwanza imeshakuwa finyu wananchi washaivamia, lakini vile vile kuna eneo la Micheweni ambalo limejengwa kwa kikosi hichi.

Mimi nishauri tu kwamba ni vyema kuihamishia kambi ile pale Chake Chake Ndugukitu kapelekwa kule kwanza eneo lake zuri, lakini vile vile udongo wake unaweza hata kujengeka na mchango wangu nimeupeleka vile vile kwa maandishi nashukuru uliponipa nafasi ya kuweza kuchangia nimeona hili vile vile niliseme.

Mhe. Spika, kwa kweli eneo lao zuri liliopo Micheweni wakipewa pale eneo lile basi watapata kujenga mabweni na ofisi zao ili wataweza kuimarika. Lakini vile vile kwa haraka haraka Mhe. Spika, nende katika barabara. Ninashukuru sana Mkurugenzi wa Halmashauri ya Micheweni kupitia barabara ya Tumbemapofu katika kipindi hichi cha mvua daraja lile lilikuwa limekatika, lakini nimepata dondoo hapa nikamuuliza, akanambia tayari kishalirekebisha. Kwa hivyo namshukuru sana Mwenyezi Mungu amjaalie ampe pumzi zaidi ili tushirikiane katika kuhakikisha kwamba mambo haya yanaendelea siku hadi siku.

Lakini mwisho Mhe. Spika, kwa kumalizia nimuombe tu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Micheweni kuna skuli yangu ya Chimba ambayo tumeianzisha sote kwa pamoja, bado skuli ile haijafikia hatua nzuri. Nimuombe tu kwamba katika bajeti hii tunayokwenda nayo tukifikiria pamoja na kuchanganya pesa za mfuko wa jimbo tushirikiane ili kuona kwamba lile lengo lililokusudiwa linapatikana ili wananchi wale na wanafunzi waweze kupata huduma kama ilivyo.

Mhe. Spika, nakushukuru sana naunga mkono hoja asilimia mia moja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mhe. Hidaya Ali Makame atafuatiwa na Mhe. Said Soud Said na Mhe. Waziri wa Fedha ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame : Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia mimi nafasi kwa kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Tawala za Mikoa.

Mhe. Spika, kwa vile wenzangu wengi tayari wameshasifu na masifio yameshakuwa mengi mimi moja kwa moja nendelee kwenye mchango. Kwa kuanza mimi moja kwa moja nitaeleke Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuhusu kambi ya KMKM iliopo Kibwengo (*Makofi)*

Mhe. Spika, katika kambi ile iliyopo pale Kibwengo kambi ile ni yetu ambayo tunaifahamu na inafanya kazi ndani ya Wilaya ile ya Kaskazini "A", lakini kambi ile inakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa umeme.

Mhe. Spika, mimi ningemuomba sana tu Mhe. Waziri hapa katika bajeti hii ambayo tunaipitisha leo hii, atwambie je, kaandaa nini katika kambi ile ya KMKM iliyopo pale Kibwengo kuhusu suala la umeme na mengine yote yale madogo madogo ambayo yanaikwaza ile kambi kuweza kupatiwa marekebisho na kuweza kuekewa sawa baadhi ya hizo changamoto zao zikaweza kukaa sawa na wakaendelea na kazi zao. Lakini pia nizungumzie na Kambi ya Zimamoto ambayo ipo Kigunda kwa (Juma Rama), pale pia tumeekewa kile Kituo cha Zimamoto ambacho kinaendelea kufanya kazi yake ndani ya Wilaya yetu ya Kaskazini "A".

Lakini Mhe. Spika, kiukweli kambi ndio kambi na waliopo pale ni binadamu lakini ni ofisi maalum kiufupi, lakini hatuoni kitambulisho cho chote ambacho kimewekwa pale kikaweza kutambulisha mtu yoyote anaeweza akapita ukiachilia yale magari ambayo yanakuwa yanawekwa pale yale ya Zimamoto. Mfano wakati imeondoka ile gari imeshuka bondeni kwenda kufanya kazi zake nyengine mtu yeyote akipita pale hawezi kujua kwamba hii ni kambi ya aina au hapa hizi nyumba zimejengwa za namna gani.

Kwa hivyo mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri ukiachilia mbali bendera na vitu vyengine iwepo nembo maalum ambayo itaonesha hapa pana kituo fulani ambacho kinafanyakazi fulani. Lakini ukiachilia mbali hizo nembo basi ningeiomba sana Wizara Mhe. Waziri katika bajeti hii ambayo tunapitisha, ukiliangalia lile eneo kuhusu suala la uzio ili kuweza kuwahifadhi wale watu na kazi zao na mambo yao mengine ambayo wanakuwa wanaendelea kuyafanya katika pirika zao zote na mazoezi na kila kitu.

Lakini nikitoka hapo Mhe. Spika, moja kwa moja nende kwenye suala la masoko. Nampongeza sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein katufungulia soko karibuni tu katika Kijiji cha Kinyasini. Mimi ningeomba hapa nikaja nikapewa majibu katika kijiji cha Wilaya ya Mahonda Jimbo la Donge kuna msingi ambao umewekwa labda pengine tangu mimi sijazaliwa au sijui siku za mbele karibuni, msingi huo ni wa soko ambalo soko hilo lingewafaa wananchi waliokuwepo maeneo yale pale yote, kuanzia pengine Kitope mpaka maeneo ya Donge baadhi na maeneo ya Kinduni kuja pale wakafanya biashara zao ili kuweza kuwasadia wananchi wa pale na mahitaji mengine.

Lakini mpaka kufikia leo hii, soko lile limebakia msingi tu kwamba halifahamiki mwaka gani litajengwa na mwaka gani litaanzishwa. Kwa hiyo mimi hapa ningemtaka Mhe. Waziri akajaa akatupa maelekezo. Je, ni lini lita fanyiwa ujenzi soko lile na kama labda halihusiki kwenye

bajeti yao je, kuna taratibu gani ambazo watazichukua ili soko lile nalo liweze kujengwa liweze kukamilika na wananchi wa maeneo yale waweze kufaidika na soko lile (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kumalizia niende moja kwa moja kwenye suala la ugatuzi. Kwenye suala la ugatuzi mimi ningependa kuwazungumzia hapa Madiwani na Wakurugenzi ambao moja moja kwa ndio limewagusa hasa suala hili la ugatuzi. Katika Wizara ambazo zimegatuliwa ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya na Wizara ya Kilimo.

Lakini mpaka muda huu hapa bado kuna changamoto nyingi ambazo zinaikabili hii gatuzi. Sasa huu ugatuzi mimi ningewaomba tu Waheshimiwa Mawaziri wote ambao wanahusika na huu ugatuzi wakakaa pamoja ili wakaweza kukamilisha hili suala hususan Wizara ya Kilimo ili kuwaondoshea mzigo mzigo unaowakabili Wakurugenzi na Madiwani katika utendaji wao wa kazi. Lakini ningeiomba wizara hii katika bajeti hii inayofanyika pia wakawaangalia Madiwani na Wakurugenzi katika shughuli zao za kiutendaji wa kazi zao, kuhusu usafiri lakini pia kuhusu hata lile posho ambalo wanakuwa wanapatiwa kwa sababu wanakuwa wanasumbuka sana ukiangalia pia kwamba ndio wameongezewa ule mzigo wa kufuatilia mpaka vituo vya afya.

Mhe. Spika, kwa hayo machache na mimi niseme kwamba naiunga mkono hutuba hii asilimia 89 na hayo maelezo yatakapokuja na majibu yake nitaiunga mkono asilimia 100.

Ahsante Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mhe. Spika, naomba na mimi kutoa mchango wangu kidogo katika kuunga mkono bajeti hii, na naunga mkono kwanza mia kwa mia kabla ya kusema yote.

Lakini pia nachukua nafasi kusema kwamba Wizara hii imefanikiwa kutekeleza majukumu yake yote kupitia Ilani hii ya uchaguzi, ukisoma kifungu cha 124 utakuta yote ambao yanatekelezwa na Wizara hii yako kwenye Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Lakini pia ningechukua nafasi hii kuwashukuru sana Wakuu wa Mikoa na kuwaambia kwamba wameweza kufanikiwa sana katika kulea demokrasia katika nchi yetu, kutokana na kuwashirikisha viongozi wa vyama vya siasa ndani ya nchi hii bila ya kubagua, pale pote panapotakiwa kushirikishwa viongozi wa vyama vya siasa, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wanawaita viongozi na kuwashirikisha. Kwa mfano mwenge, upandaji wa miti, usafi wa mazingira mambo kama haya yanafanywa chini ya uongozi wa Serikali za Mikoa. Na ni jambo la kufurahisha sana kwamba wanaielea demokrasia kama inavyotakiwa ndani ya Tanzania yetu. Vile vile nawapongeza Wakuu wa Mikoa kwa kusimamia vyema mazingira ya nchi yetu kulingana na utamaduni ambao sasa hivi ndio mali pekee ya kuringia Wazanzibari.

Mhe. Spika, nachukua nafasi ya pekee kumpongeza Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kusimamia vyema utamaduni wa Mzanzibari. Kwa sababu Zanzibar kama Zanzibar inajiuza kwa jina lake peke yake, lile jina tu la Zanzibar basi ni mali katika dunia na kwa nini ni mali kwa sababu utamaduni wa Zanzibar ndio unaomfanya Mazanzibari kujulikana popote duniani na kupewa heshima yake, sasa kuusimamia utamaduni wa Zanzibar ni jambo muhimu sana na

linalopaswa kufanywa na Mikoa yote ya Zanzibar. Zanzibar inaringia utamaduni wake na sisi kama Wazanzibari lazima tuhakikishe kwamba tunaulea utamaduni wa Zanzibar, tuache tabia ya kuigiza desturi za mila za watu Zanzibar itabaki kama Zanzibar ndani ya Tanzania hii lakini utamaduni wake ni mali.

Mhe. Spika, Wazanzibari wanatakiwa wote wazazi walezi kusimamia tamaduni si serikali peke yake wazazi na walezi tusimamie utamaduni wa nchi yetu na tukiusimamia vyema mafanikio ya Zanzibar yataendelea kupatikana. Pia nachukua nafasi ya kupongeza Rais wa Zanzibar kwa kukubali ugatuzi. Ugatuzi huu ambao unasimamiwa sasa na Makamu wa Pili wa Rais katika mazingira ya utekelezaji wake ni vyema tukakubali kuupa nafasi ili kuleta mafanikio kwa sababu lengo la ugatuzi ni kupeleka maendeleo kwa wananchi na kuwafanya wananchi vijijini waweze kushirikishwa kikamilifu katika kuleta maendeleo yao.

Sasa hautafanikiwa ugatuzi kama sisi wenyewe hatutokuwa tayari kuupokea ugatuzi kwa vile inavyotakiwa ni vyema, Wazanzibari sote tukawa tayari kupeleka maendeleo kwa nguvu zetu zote kwa sababu Zanzibar haitojengwa na mtu mwengine yeote ni Wazanzibari wenyewe ndio watajenga Zanzibar na watajenga vipi kwa kuwa tayari kushikamana na kuendeleza umoja wa Wazanzibari.

Mhe Spika, ahsante sana naitumia kwa kusema kwamba ni vyema Watanzania tukawa tayari kulinda na kuudumisha muungano wetu ambao ndio kiyoo na ndio roho ya Tanzania, tukawa tayari kulinda mapinduzi yetu ambayo sasa ndiyo yanatufikisha hapa kuweza kuilea nchi yetu.

Pia nachukua nafasi hii ya dakika moja kuwapongeza makamanda wote wa vikosi vya Zanzibar na Vikosi vya Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kukamilisha ulinzi wa karafuu mara hii na tukaweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupata zao letu ambalo ndio mali kwa nchi yetu na hii waendelee kulinda hadi hivi sasa, kwa sababu wabaya wa nchi hii bado wapo ambao karafuu bado wamezizuia hazijatolewa sasa ni vyema wakawa tayari kulinda na kuhakikisha kwamba karafuu bado inahitaji kulindwa isitoke ndani ya nchi.

Makamanda wote hongera sana kwa kazi hii ambayo wameifanya ahsante sana mheshimiwa.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Waziri naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Fedha Dkt. Khalid Salum Mohamed ambaye atafuatiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ Mhe. Shamata Shaame Khamis.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Spika kwanza nianze kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pia nieleza kwamba ninachangia Hotuba hii ya Bajeti katika maeneo makuu mawili. Eneo la kwanza ni kutoa pongezi na Mhe. Spika, natoa pongezi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Vikosi, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji wote na mheshimiwa natoa pongezi hizi kutokana na utekelezaji mzuri sana wa miradi katika wizara hii katika mwaka huu tunaoendelea nao wa 2017/2018.

Mhe. Spika, na nitaanza kuitaja baadhi ya miradi hiyo ni kwamba tulikuwa na tatizo kubwa sana la mahanga katika vikosi vyetu, lakini kwa juhudi iliyochukuliwa na Mhe. Rais mwenyewe kwanza ya kuunda kamati ya kufuatilia na kwa bahati nzuri na mimi nilikuwa mmoja katika Wajumbe wa kamaati hiyo, kwa hali niliyoiona katika vituo mbali mbali ya hali ilivyokuwa ya mahanga ya askari huyu na kwa mafanikio makubwa sana ujenzi wa mahanga hayo katika maeneo mbali mbali hasa Pemba, Tungamaa, Kengeja, Kojani, Makombeni imefanyika kwa ufanisi mkubwa sana. Natoa pongezi kwa Mhe. Rais lakini pia nampongeza Mhe. Waziri na Watendaji wake wote kwa mafanikio hayo.

Lakini vile vile kuna fedha zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo ya vikosi vyetu kwa Unguja na Pemba lakini vile vile wamefanya kwa mafaniko makubwa sana ujenzi wa Jengo la Kurekebisha Watoto la Hajengwamchana lipo katika hatua nzuri sana na tunatarajia ujenzi huo utakamilika ndani ya mwaka wa fedha huu 2017/2018. Lakini pia nilipata nafasi ya kutembelea Skuli ya Sekondari ya Mtoni ya JKU kazi inayofanywa pale nayo ni nzuri sana ya jengo lile nayo inakaribia kumalizika na itamalizika ndani ya mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Lakini kwa upande wa KMKM Jengo la Mama Wajawazito na Watoto la Kibweni lipo katika hatua nzuri na linatarajiwa likamilike ndani ya mwaka huu wa fedha 2017/2018, na vifaa tiba vimewekwa katika bajeti 2018/2019 ni mafanikio makubwa sana na hatuna budi kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Wizara hii kwa mafanikio haya. Lakini kutokana na maagizo ya Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, Kiwanda cha Viatu cha Mtoni jengo lake limekamilika lakini vile vile wanaanza ujenzi wa jengo la Kiwanda cha Nguo kushonwa nguo katika eneo hilo hilo na hiyo kazi inafanyika katika mwaka wa fedha 2018/2019. Vifaa kwa viwanda vyote tayari vimeshagizwa na fedha zake zipo, kwa hivyo kila kitu kitakamilika Inshaallah ndani ya mwaka wa fedha ujao kwa viwanda hivyo.

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio mengine ni ununuzi wa boti za uokozi. Nchi yetu ni kisiwa na tayari tumeshapata *incident* za maafa mbili kubwa na tulikuwa na *challenge* kubwa sana katika masuala ya uokozi na kutokana na tatizo hilo serikali imeona kuna haja ya kuweka boti mbili za uokozi na boti mbili hizo tayari zimeshaagizwa. Moja inatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi wa Juni lakini na ya pili itawasili ama mwishoni mwa mwezi wa Julai ama mwanzoni mwa mwezi wa Agosti, boti mbili hizi ambao moja itakuwa Pemba, moja Unguja zina uwezo mkubwa.(*Makofi*).

Boti moja ina uwezo wa kuokoa mpaka watu mia nane kwa maana utakuwa na vifaa vya kutoa ukozi kwa watu mia nane kwa wakati mmoja na ile nyengine itakuwa na uwezo wa kuokoa mpaka watu mia sita kwa wakati mmoja. Haya ni mafanikio makubwa sana ambayo nchi yetu imepata hasa katika suala zima la usalama katika vyombo vyetu vya baharini, tumpongeze sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa mafanikio haya lakini vile vile tuipongeze Wizara kwa juhudi kubwa ambazo wanaendelea kuchukua katika kuhakikisha kwamba usalama katika usafiri wa baharini unakamika kama ilivyotaarajiwa na serikali.(*Makofi*).

Lakini tuna boti tatu za *patrol* ambazo hizo zimeshawasili na kuna moja ya zimamoto ambazo zitakuwa boti nne zote zimeshawasili na la kufurahisha zaidi kwamba haya yote yamefanyika

kwa kupitia fedha zetu wenyewe, hakuna msaada wala hakuna mkopo katika upatikanaji wa vifaa hivyo hizo ni sehemu ya mafanikio ya serikali yetu katika mwaka wa fedha 2017/2018 na tunaamini kabisa mafanikio hayo yataendelezwa na kuwa makubwa zaidi ijayo ya fedha Inshaallah mwaka 2018/2019.

Mhe. Spika, kuwa na boti hizi kwanza zitatusaidia katika suala zima la ulinzi na usalama lakini vile vile sisi tunafarijika zaidi, kwa sababu litatusaidia katika ukusanyaji wa mapato hasa kuthibiti wale wakorofi wanaopeleka bidhaa kwa njia za magendo sasa watadhibitiwa. Na mimi niwaombe tu waache mchezo huo kwa sababu tayari kikosi chetu kinashakuwa na zana kamili za kuweza kuwadhibiti.(*Makofi*).

Mhe. Spika, baada ya hayo nilitaka nitowe ufafanuzi wa baadhi ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe waligusia kwa kifupi sana. Kuna maelezo yalielezwa hapa kwamba tutumie fedha za Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kutengeneza barabara za ndani (*feeder road)* na ikashauriwa ushauri mzuri kwamba ile asilimia kumi na tano ambayo imetengwa kwa *feeder road* iongozwe iwe asilimia thalathini ni wazo zuri. Lakini katika mfumo wa barabara tuna mifumo ya barabara, barabara kuu kwa maana ya *trans road* lakini vile vile na barabara hizi za ndani ni *feeder road*, zote ni muhimu katika masuala ya uchumi, kwa sababu *feeder road* ndizo zinazounganisha maeneo ya uzalishaji kilimo, kuunganisha na maeneo ya barabara kuu zote muhimu.

Lakini ni vyema na naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wakubaliane na ushauri wangu kwamba badala ya kulifikiria juu juu hili suala, ni vyema wakatuachia wizara zetu tukaa pamoja kwa ajili ya kulifanyia *study* ya kina, tutakaa na Wizara hiyo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Wizara ya Fedha, Tume ya Mipango na kazi hiyo tutaifanya ndani ya mwaka wa fedha ujao. Wizara ya Miundombinu tutakaa nao pamoja ili tuweze kujua ni uwiano gani utasaidia, nataka kusema twende kutoka kumi na tano kwenda thalathini basi hiyo *study* na matokeo yake tutaishauri serikali na tutaona tuje na utaratibu gani mzuri zaidi utakaosaidia katika suala hili.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nililitaka nilizungumzie ni suala la fedha ambazo zimezungumzwa sana za ugatuzi na hasa za Wizara ya Kilimo kwamba fedha hizo bado hazikutoka katika Wizara ya Kilimo na kupelekwa kwenye Ofisi ya Rais, Tawala Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum. Ni kweli na najua karibu milioni thamanini bado zipo kule lakini hiyo ilitokana na ugumu wa *exercise* yenyewe kwa mwaka huu wa mwanzo ambao tunaziondoa fedha hizo kuzipeleka kwenye wizara itakayosimami masula ya ugatuzi.

Kwa Wizara ya Afya nikiri kwamba zoezi hilo lilifanyika vizuri na lilifanyika vizuri kutoka na mfumo wa Wizara ya Afya yenyewe ilikuwa tayari imeshagatuliwa, kwa sababu Wizara aya Afya walikuwa na utaratibu wa kuwa na *zone,* lakini kwa Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Elimu kidogo kulikuwa na changamoto zake na nikiri kwamba kuna fedha ambazo ni fedha zinazohusiana na posho la usafiri kwa wafanyakazi. Hili bado halijatoka katika wizara zinazohusika, Wizara ya Elimu kwa upande wa Pemba lakini kwa Wizara hii ya Kilimo za Pemba na Unguja lakini vile vile na baadhi ya vifaa. Sasa sisi tutoe ushauri tu kwamba hili tumeliona na tutakacho kifanya ni kuhaulisha kutoka fungu kwenda kwenye fungu baada ya

bajeti hizi kupita. Kwa hivyo upo utaratibu wa kisheria ya *veymnent*, hizi fedha tunazijua tutazitoa ili kuziweka katika Wizara inayosimamia masuala la ugatuzi.

Mhe. Spika, jengine kwa haraka sana lilikuwa ni suala la uratibu katika masuala ya *EFB*. Ilizungumzwa hapa kwamba kuna uratibu makini katika matumizi ya mfumo wa kieletroniki katika ukusanyaji wa mapato baina ya *ZRB* na Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, hili nisema kwamba sisi hatuhitaji kuunganisha kuwa na mfumo mmoja Serikali za Mitaa zina utaratibu wake, zina mfumo wake na zinataka ziendelee na *autonomy* hiyo kwa sababu ukichukua mapato hayo ukayapeleka *ZRB,* tayari umeshaingilia *region* nyengine katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo tunawataka waendelee na utaratibu huo na *ZRB* ina mapato ambayo imewekewa kwa mujibu wa taratibu za kisheria ya kuyakusanya. Kinachofanyika sasa hivi ni labda kwenye kodi ya nyumba (*property tax),* huu ndio utaratibu uliowekwa kwamba itakusanywa na *ZRB* na *ZRB* itakata asilimia tano ya gharama ya ukusanyaji, asilimia tisini na tano itarudi Serikali za Mitaa kwa utaratibu utakaowekwa na Serikali. Kwa hivyo hapa sisi tukawa na matumaini kwamba mfuko wa *EFB* wa *ZRB* utakuwa unaungana na mfumo wa *EFB* wa Serikali za Mitaa. Lakini jambo la kufurahisha ni kwamba mradi wa *ZUSP* unasaidia Serikali za Mitaa katika kuwapatiwa vifaa vya *EFB,* lakini vile vile mafunzo kwa watendaji wao katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato yanayohusika na Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, la mwisho katika mchango wangu ni hili suala la *safety fee* lilishauriwa hapa *safety fee* itumike ya *Airport* itumike kwa ajili ya kusaidia Kikosi cha Zimamoto pale *Airport.* Ni wazo zuri lakini niliwahi katika kikao hiki kinachoendea, niliwahi kusema kwamba si vyema tukafikiria mapato yanapokusanywa yabakishwe pale kwa matumizi ya eneo hilo, kwa sababu Mhe. Spika tukifanya hivyo unaweza ukajikuta Baraza lako hilo halina vifungu kwa sababu halina mapato, ni lazima mapatio haya kutokana na usimamizi bora wa fedha za umma, lazima yawe *consolidated* na yaingie kwenye mfuko wa Serikali halafu tutizame namna bora ya kugawana kwa mujibu wa *priorities* zilizopo.(*Makofi*)

Sasa suala la *safety free* hutolewa *certain percentage* ili kwenda kwenye Zimamoto nafikiri si jambo la busara sana. Lakini jambo ambalo naweza kukubaliana nalo ni kwamba tutazingatia mahitaji ya Kikosi cha Zimamoto pale *Airport*, najua wana mahitaji ya kuweka barabara kwenda kwenye henga lao lakini vile vile watahitaji fedha za uendeshaji na pia watahitaji kujenga bwawa na kuhifadhia maji katika eneo lao. Hilo sisi tutalichukua tutakaa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, tuone ni mahitaji gani hayo ya fedha yanayohitajika ili kwa utaratibu wa kawaida wa kibajeti tuweze kuwapatia fedha hizo.

Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja nakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha naomba sasa nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ili aje atowe mchango wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, na mimi kwa ruhusa yako nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia angalau machache katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ lakini kabla sijaanza naomba nitumie fursa hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini vile vile kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna ambavyo Ofisi hii atatupa maelekezo lakini kwa namna ambavyo anaitekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa uhakika na umamkini wa hali ya juu.

Mhe. Spika, mimi pia naomba nitumie fursa hii kuwapongeza wote wafanyakazi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maluum za SMZ kuanzia Waziri mpaka Watendaji wa chini, ukweli ni kwamba namna ambavyo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamechangia Makadirio ya Hotuba hii ya Bajeti na mimi niungane nao kwamba ni kazi kubwa ambayo imefanywa na ndio maana zikashuka pongezi nyingi, licha yakuwepo kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanahitaji ufafanuzi katika baadhi ya mambo ambayo waliona kidogo wanataka kuelewa zaidi.

Lakini naomba nitumie fursa hii kuwaomba tena Waheshimiwa Wajumbe kwamba tuendelee kuunga mkono hotuba hii, lakini vile vile tuwe tayari kuipitisha pasi na kuwepo vikwazo kwa sababu ni dhahiri kwamba kila mmoja wetu alivyokuwa akichangia ameonesha ni namna gani ambavyo tumeweza kufanya kazi kwa bidii ya hali ya juu.

Mhe. Spika, katika michango yangu mimi naomba nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo labda nitagusia ijapokuwa walochangia ni wengi na yaliyosemwa ni mengi na kutokana na muda basi naomba niende haraka haraka pasi na kumtaja mtu yeyote au Mheshimwa yeyote kutokana umuhimu.

Mheshimiwa kwanza nianze lile ambalo limezungumzwa kuhusiana na askari tisa ambao wa Kikosi cha KMKM ambao walisimamishwa kazi. Ni kweli waheshimiwa wameshukuru juhudi ambayo imefanyika na sisi tunasema tumezipokea pongezi hizo. Lakini kuhusu madai ambayo askari wale walikuwa wanadai basi utaratibu utaendelea kufuatwa ili kuona mwisho wa siku kama ambavyo alipata fursa ya kurudi tena basi madai yao yaweze kufikiwa na yaweze kupatika, kwani sasa hivi tayari malalamiko yale yameshapelekwa katika taasisi zinazohusika ili kusudi kuona kwamba fedha zao zile wanazipata kwa mujibu wa vile ambavyo sheria itakuwa imeruhusu.

Mhe. Spika, Waheshimiwa wengine walizungumzia sana Waheshimiwa Madiwani, na mimi naomba nikiri kweli Madiwani wamekuwa wakitusaidia sana na wanafanya kazi kubwa sana. Hayo ambayo ya ugatuzi na yale mengine wamekuwa wakijitahidi kuona wanapigania huduma zetu kwenye maeneo yetu zinakwenda vizuri zaidi. Niseme suala la posho zao tumesema posho hizi zinapatikana kwa mujibu wa utaratibu kama vile posho ambazo zimeonekana kwa kadri Manispaa au Halmashauri husika inapokuwa mstari wa mbele zaidi kukusanya, na ndio hivyo hivyo Ofisi ile ilipata fursa ya kuona inatengeneza miundombinu ya kuziangalia zaidi posho na stahiki nyengine za Waheshimiwa Madiwani.

Mhe. Spika, kwa hivi sasa hali ya maboresho kwa maposho ya Waheshimiwa Madiwani zinaendelea vizuri na kwa zile Halmashauri ambazo hazijafanya mabadiliko kidogo, basi tunategemea kwamba ifikapo Julai mwaka huu nazo zitaanza kuongeza maposho na stahiki nyengine kwa Waheshimiwa Madiwani. Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe wafahamu na sisi tunalielewa hilo na tumeuchukua ushauri huo na hiyo juhudi tayari imeshaanza kufanyika na tutaendelea na hatutosita pale tutakapoona kwamba hali inaruhusu kufanya hivyo.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa mmoja aliyezungumzia nyumba mbovu au wananchi wetu ambao wanaka katika nyumba za maendeleo kule Kengeja, kuhusiana na wale watu waliokuwemo mle ni watu wetu. Naomba nijibu kwamba hilo nalo tumelichukua na tutahakikisha tunafanya mawasiliano mazuri na Shirika la Nyumba tuweze kuona ni namna gani tunaweza kuokoa maisha ya wananchi katika maeneo yale kabla hakujatokea madhara mengine.

Mhe. Spika, vile vile kulikuwa na Waheshimiwa Wajumbe walitoa mawazo yao namna ambavyo wameona umekuwa uvamizi mkubwa katika kambi yetu na Ndugukitu kule kisiwani Pemba, kutushauri tuweze kuondoa kambi katika eneo lile na badala yake tuweze kuwaachia wananchi wawepo katika maeneo yale.

Mhe. Spika, niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe suala la ulinzi ni suala ambalo ni la lazima sana, na hatuwezi kulinda katika eneo ambalo tume-*plan* tunaweza tukaweka kambi zetu. Hivyo niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe tuwasaidie wananchi wetu kuwaelimisha kwamba wasiendelee kuvamia maeneo ya kambi na sio Ndugukitu tu bali na maeneo mengine, kwa sababu kwa historia ni kwamba kambi ile imetangulia sana baadhi ya majengo mengine ambayo tunayashuhudia sasa hivi yakiendelea. Kwa hivyo ni vyema Waheshimiwa tutumie fursa hii kuwaomba wananchi wetu wasijenge kwenye maeneo ya kambi na sio Ndugukitu lakini na vikosi vyengine tuna changamoto kama hizo ambazo Waheshimiwa Wajumbe wengine waliweza kuyazungumzia.

Mhe. Spika, kuhusu usafiri kwa Waheshimiwa Madiwani nalo ni jambo ambalo limezungumzwa sana na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wameonesha hisia zao ni namna gani Waheshimiwa Madiwani wetu wanapata nyenzo za usafiri ili kusudi waweze kumudu shughuli zao katika mazingira haya ya sasa tunayoendana na ugatuzi.

Mhe. Spika, naomba nitoe ufafanuzi kwamba suala hili tayari Mhe. Waziri alishalitolea maelekezo, na kwa kiwango kikubwa jambo hili limeweza kufanyika sasa hivi. Mpaka sasa hivi kuna baadhi ya Waheshimiwa Madiwani ambao walikuwa na mahitaji ya kupata usafiri, sasa hivi wameshapatiwa usafiri. Kwa mfano, katika Baraza la Mji Mkoani madiwani wote asilimia 100 tayari wameshapatiwa vyombo vya usafiri. Vile vile kuna baadhi ya Madiwani kwa mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni nao pia asilimia 50 wameshapatiwa vyombo vya usafiri na wengine hatua zinaendelea.

Mhe. Spika, kwa kuokoa muda niseme tu kwamba katika makundi haya Waheshimiwa Madiwani wako ambao walitaka usafiri na wengine waliona kwamba wao wangepata kitu chengine zaidi. Hayo yote tumeyazingatia na mambo haya yameshafanikiwa kulingana na Waheshimiwa Madiwani wetu namna ambavyo na wao walikuwa wametaka wafanikishe. Kwa

hivyo suala hili limeshafanikiwa na halina tatizo na pale ambapo hajakamilisha, tunategemea kwamba ndani ya mwezi wa Julai baada ya kumalizika mkutano huu wa bajeti basi tutaona na wao wanafanikiwa kupata vyombo vya usafiri kwa wale wanaohitaji usafiri.

Mhe. Spika, kuhusu Mradi wa Ugatuzi Waheshimiwa wengi wamepongeza sana namna juhudi zimefanyika. Ni kweli mwanzo ilionekana Waheshimiwa Wajumbe wengi walikuwa na hofu lakini baada ya utekelezaji tumeona kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa. Kwa mfano, kama sekta ya elimu sasa hivi tumeanza ufuatiliaji na tumeshaanza kuelekeza nguvu zetu huko baadhi ya mikakati imeshafanyika. Vile vile hata sera zimeshaanza kutumika kukabiliana na mazingira yaliyopo na Waheshimiwa Wajumbe wameonesha hisia wengi hususan maeneo ambayo yametajwa mfano kama Mwambe, Ole na kwengineko kuhusiana na changamoto kubwa ambayo inaonekana kujitokeza ya uhaba wa walimu katika maskuli yetu pamoja na miundombinu.

Mhe. Spika, niseme kwamba yale ambayo yako ndani ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa tutayafanyia kazi na tutahakikisha kwamba tunafuatilia ili tuone huo mgao ambao ulifanyika kwa namna gani. Na sisi tutakaa na Wizara ya Elimu kushauriana *modality* gani itumike ili kuona tunakabiliana na changamoto hiyo, sambamba na kutafuta namna nyengine ya kuishauri serikali kuona ajira mpya ziweze kupatikana kwa ajili ya kuziba hayo mapengo ambayo yanaonekana ni *gape* kubwa.

Mhe. Spika, vile vile katika sekta ya afya. Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali waliweza kuchangia wakaonesha changamoto tulizokuwa nazo katika vituo vyetu lakini wengine mpaka wakafika kusema suala zima la upungufu wa madawa. Niseme tu kwa sasa hivi vituo vya afya kutokuwa na madawa ni jambo ambalo suala la madawa bado lipo katika majukumu ya Wizara ya Afya. Lakini kwa kuwa na sisi vituo hivi vilivyogatuliwa ni wajibu wetu kuona ni utaratibu gani ambao unatumika ili madawa yaweze kupatikana kwa mujibu yale yanayoagizwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, niseme kwamba hili nalo tutalichukua tutahakikisha tunafuatilia ili kuona ni namna gani bora zaidi dawa hizo zinapatikana na si kwamba dawa hazipo, lakini inaonekana utaratibu labda kidogo baadhi ya watendaji wetu bado hawajaufanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, kutokana na hili pia Waheshimiwa ni mashahidi wale waliosema vituo vya afya vibovu, vyengine havina meza. Ukweli ni kwamba vituo vya afya kwa kiwango kikubwa tumeona juhudi ambayo imeshaanza kufanyika katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba au katika Halmashauri zetu na Mabaraza yetu. Ukienda Kaskazini maeneo ya Potoa ni juhudi kubwa Waheshimiwa ambao wapo maeneo ya kule, Tundauwa na kwengineko katika vituo mbali mbali ugatuzi umeshaanza kufanya kazi na unaonekana kwa vitendo zaidi. Mhe. Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe ambao wameonesha pongezi zao katika kufanikisha shughuli hii.

Mhe. Spika, vile vile kuhusu suala la pembejeo za kilimo imeonekana nalo ni jambo ambalo Waheshimiwa Wajumbe baadhi yao wamezungumza. Katika ugatuzi huu hili tunalichukua kwa namna gani tunaongeza ukaribu zaidi kuona huduma hizi za kilimo na mambo ya elimu kwa

wakulima yanaweza kupatikana kwa juhudi kubwa ambayo kwa sasa hivi nimeiona naamini tutafikia vizuri.

Mhe. Spika, pia naomba nitumie fursa hii kuwapa pongezi sana Waheshimiwa mbali mbali hususan wa Chama ambao wameweza kusimamia Ilani kwa kupita katika mabonde ya mpunga. Kwa mfano, kama Bumbwisudi tumeweza kuwaona Waheshimiwa wengine ambao waliweza kutoa ahadi na kupeleka matrekta. Nimpongeze sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, vile vile kuna Waheshimiwa Wajumbe wengine walikuwa na hofu kwamba tokea kupata mfuko huu wa kujenga barabara za ndani, kutaka kujua ni barabara zipi ambazo zimefanyiwa kazi mpaka sasa hivi na ngapi ambazo zimefanyiwa upembuzi yakinifu kutaka kuzijua hizo barabara ni zipi. Mhe. Spika, kiufupi barabara ambazo tumezifanyia upembuzi yakinifu ambazo zinahitaji kujengwa zilikuwa ni kati ya kilomita 50 Unguja na Pemba. Lakini katika utekelezaji wake ni barabara chache ambazo tayari tumeshaanza kuzifanyia kazi, na kwa orodha ni kubwa mno jambo ambalo ningeomba Mhe. Mjumbe yule ambaye alitaka kujua kwa kuwa orodha ni kubwa ningeomba apate muda baadae orodha tunayo tunaweza tukamuonesha ni kwa namna gani barabara ambazo tumeweza kuzitekeleza na kwa kilomita ngapi. Vile vile tufahamu kwamba barabara ambazo ni *feeder road* na tuna wajibu mkubwa sisi kuzingalia katika kuzitengeneza kwake, tujue kama ni nyingi ziko tayari ambazo tushaziorodhesha lakini bado kuna nyengine hatujazifanyia upembuzi na kuweza kuzitambua tukaweza kuzifanyia kazi.

Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi anayetaka kupata taarifa basi tunazo kwa maandishi ambazo tayari tumeshazifanyia kazi…

Mhe. Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba pia ushauri wa Kamati nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti pamoja na kamati yake ya kisekta tayari na wao wameonesha ushauri wao kuhusiana na kuongeza mapato au ukusanyaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni na Baraza la Mji Wete. Niseme tu kwamba ushauri huu tumeuchukua na tutajitahidi kuona hapo tulifikia tunakwenda zaidi ili kusudi huduma zinazotarajiwa katika Baraza la Mji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba ziweze kuonekana zinafanikiwa zaidi.

Mhe. Spika, baada ya mchangio huo na mimi naomba niseme tu kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wao waipitishe. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe sasa naomba nimwite mtoa hoja Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Karibu Mhe. Waziri una saa nzima.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nichukue fursa hii kutoa ufafanuzi kwa hoja

mbali mbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu katika mchango wa kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kipindi cha mwaka 2018-2019.

Kabla sijaanza kutoa ufafanuzi naomba niwatambue wale wote ambao wamechangia hotuba hii. Kwa ujumla hotuba hii imechangiwa na Wajumbe 52. Wajumbe 37 wamechangia kwa kusema moja kwa moja na Wajumbe 15 wamechangia kwa maandishi, na najua kwa nini wamechangia lazima nikiri kwamba bajeti hii ni bajeti ya wananchi na Wawakilishi wamechaguliwa na wananchi.(*Makofi*).

Kwa hiyo, kama muda ungekuwepo zaidi nadhani wajumbe wote wangeweza kuchangia. Kwa hivyo nawashukuru na nawapongeza sana wale wote ambao wamechangia bajeti hii, wametoa ushauri, wameomba ufafanuzi na namuomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe kuweza kutoa ufafanuzi, na nitatoa ufafanuzi wa jumla kwa sababu michango iliyotolewa ni mingi kama nitakwenda Mwakilishi mmoja baada ya mwengine Mhe. Spika, saa moja hainitoshi na michango iliyotolewa yote ni ya msingi na ni ya maana sana.

Kwa hiyo, nitatoa michango ya jumla, nitakapokuwa natoa michango ya jumla kila mmoja najua hamu yetu hata mimi ningependa nisikike nimetetea nini Jimboni kwangu Tumbatu, lakini kwa sababu ya muda nadhani naweza kila mmoja nikisema yale ambayo amechangia ajue tu, naweza tu nikanukuu kwa baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika, naomba niwatambue waheshimiwa waliochangia:-

1. Mhe. Machano Othman Said
2. Mhe. Ali Suleima Ali (Shihata)
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
5. Mhe. Omar Seif Abeid
6. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
7. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
8. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
9. Mhe. Simai Mohamed Said
10. Mhe. Abdalla Ali Kombo
11. Mhe. Asha Abdalla Mussa
12. Mhe. Mussa Foum Mussa
13. Mhe. Said Omar Said
14. Mhe. Suleiman Makame Ali
15. Mhe. Ame Haji Ali
16. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
17. Mhe. Suleiman Sarahan Said
18. Mhe. Rashid Makame Shamsi
19. Mhe. Bahati Khamis Kombo
20. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
21. Mhe. Ali Salum Haji

22. Mhe. Hamza Hassan Juma
23. Mhe. Maryam Thani Juma
24. Mhe. Mussa Ali Mussa
25. Mhe. Makame Said Juma
26. Mhe. Tatu Mohamed Ussi
27. Mhe. Mohamed Said Mohamed
28. Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei)
29. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
30. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma
31. Mhe. Ahmada Yahya Abdul-wakil
32. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
33. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
34. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Ali Khamis Bakar lakini pia amepata fursa ya kuchangia
2. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar
4. Mhe. Khadija Omar Kibano
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa
6. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma
7. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha
8. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
9. Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo
10. Mhe. Nassor Salum Ali
11. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
12. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
13. Mhe. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
14. Mhe. Juma Ali Khatib (MBM),
15. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
16. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale.

Baada ya kwisha kuwataja waliochangia sasa naomba nitoe ufafanuzi kwa Waheshimiwa Wajumbe ambao wamechangia hoja hii ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kwanza niwashukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo ameyasema na nisingependa kuyarejea Mhe. Spika, ili kwa kuokoa muda. Nakubaliana na yale yote ambayo ameyasema na hivyo ndivyo serikali ilivyoyafanyiwa kazi yale yote ambayo ameyasema. Kwa hivyo mchango wake umenisaidia sana kutoa ufafanuzi hasa kwenye maeneo yale ya miradi ya maendeleo ya Vikosi vyetu vya Idara Maalum. Mimi nataka niwapongeze sana makamanda kwamba wamesimamia kwa umahiri mkubwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika matumizi ya fedha za serikali. Miradi hii yote imefanikiwa kwa

kiwango kikubwa na wale Wajumbe ambao hawajapata nafasi ya kwenda kutembelea basi tunawakaribisha ili wakaone namna ya miradi ilivyofanikiwa na imefanikiwa kwa sababu fedha za serikali zimetumika vizuri na zimetumika na thamani yake pia imepatikana.

Pia nimshukuru sana Naibu Waziri wangu kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo kama alivyosema. Mimi nataka nianzie pale pale ambapo amemalizia, hasa katika eneo la barabara. Lazima tukubaliane kwamba barabara ambazo tumezijenga ni kilomita saba mpaka sasa na tuna barabara kilomita 146 tulizokabidhiwa kupitia Mradi wa *MIVARF* na tuna barabara kilomita 50 ambazo tayari tumezifanyia upembuzi yakinifu. Barabara kilomita 50 lakini barabara ni 36 kwa ujumla wake, katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kama alivyosema Naibu Waziri wangu kwamba *list* yake hapa tunayo, najua Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja angetaka kujua ni barabara zipi hizo, lakini *list* tunayo kwa kuokoa muda niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wale wote waliozungumza barabara nyingi hizi zimo na barabara karibu kilomita 250 nyengine ambazo hatujazifanyia upembuzi yakinifu na zile ambazo tumepewa na *MIVARF*. Hizi kilomita 50 zote ni barabara ambazo tuna jukumu sisi kama Tawala za Mikoa kwa mujibu wa sheria kuzijenga kwa kiwango cha lami.

Sisi utaratibu wetu hatutaki kujenga barabara kwa kiwango cha kifusi, barabara lazima tutazijenga kwa kiwango cha lami. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe kila mmoja angependa niitaje barabara yake, barabara hizi pia zinazingatia zile barabara ambazo Mhe. Rais amezitolea ahadi. Hivi sasa tuko katika *site* tunajenga barabara ile ya kutoka Kijitoupele- Fuoni Mambosasa, ile ni ahadi ya Rais. Barabara kama hizi nyengine zipo nyingi tu ikiwemo ile ya Shaurimoyo, amezitolea ahadi Rais na nyingi nyengine siwezi kuzitaja zote.

Barabara hizi tuna maelekezo maalum kati ya Ofisi yetu Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na Mfuko wa Barabara. Hizi zote ambazo amezitolea ahadi Mhe. Rais tuzifanyie kazi katika mwaka ujao wa fedha, yaani hii bajeti ambayo tunaipitisha. Kwa hivyo niwaombe wale waheshimiwa wote ambao wana barabara ambazo zimetolewa ahadi na Mhe. Rais barabara hizo tunazo na wao wenyewe wakifuatilia fUatilia kuja kutukumbusha tutawaonesha, lakini niwaambie tu kwamba serikali tumejipanga katika kuona ahadi zile za Mhe. Rais nyingi tunazitekeleza kwa asilimia kubwa, ili Mhe. Rais wetu aweze kuondoka na jina na sifa nzuri ambaye anatekeleza ahadi zake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini kama nilivyosema tatizo hili ni tatizo kubwa na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe kama wengi walivyosema baada ya kumaliza bajeti hii kwa maana Mkutano wa Bajeti, sio bajeti ya Ofisi ya Rais, Mkutano wa Bajeti tutazitembelea barabara hizi zote na Waheshimiwa Wawakilishi tutakuwa na nyinyi bega kwa bega ili twende tukaone uhalisia halafu serikali iweze kujipanga vizuri…

(Hapa Kipaza Sauti (microphone) kiligoma)

Waziri wa Fedha kwamba tayari na kama tulivyosema kwenye hotuba yetu kitabu chetu cha bajeti kwamba serikali imetoa muongozo wa namna gani hizi barabara za *local government* au za halmashauri au zinazosimamiwa na Tawala za Mikoa tutazijenga, serikali iwe na mkakati gani. Tayari serikali imeunda timu kama alivyoitaja Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, timu ambayo

inaongozwa na mimi Waziri wa Tawala za Mikoa, Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Tutaifanya kazi hii kwa umahiri zaidi hasa kwa kuzingatia utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi.(*Makofi*)

Kwa hivyo nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wote kwa eneo hili wasipige buti. Serikali ina mipango madhubuti katika kuzijenga barabara hizi, lakini kama nilivyosema siwezi kutaja barabara moja moja itachukua muda sana. Lakini ile barabara ya Mpendae - Jang'ombe hii tulishamalizana toka mwaka jana. Barabara hii Mhe. Spika, dhamana ilichukuliwa na Wizara ya Miundombinu nafikiri Mhe. Mwakilishi wewe huwende tu kwa Mhe. Waziri wa Ujenzi mwende mkajue namna gani utaratibu wa utekelezaji wa barabara ile utafanyika. Kwa sababu kama ulivyosema kwamba kulikuwa na *deposit* ya *100 million*s walizotoa. Sasa mimi nadhani utaratibu upo tu kafuatilia, nikuombe sana Bamkwe wangu uaende huko.*(Makofi)*

Mhe. Spika, yeye atatafuta namna sio kwamba kesho ukienda atajenga, atatafuta namna kwa mujbu wa mipangilio ya serikali barabara hiyo inajengeka vipi. Sisi hatukatai shilingi milioni mia moja tumechukua serikali, haki ya mtu haipotei na wala serikali haina nia ya kuwadhulumu wananchi wa Mpendae na Jang'ombe. Kwa hivyo nimuombe sana kuhusu hilo na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu maelezo yanayohusu barabara ningependa niseme hayo, sina hakika kama ni machache au ni mengi sana.

Eneo jengine ambalo nataka nilizungumze kwa jumla ni suala la ajira. Limetolewa wazo hapa ni vizuri tukashauriana na Wawakilishi. Mimi nadhani tujikumbushe kwamba kuna Sheria Nam. 2 ya mwaka 2011, Sheria ya Utumishi wa Umma inatoa miongozo namna gani watu wataajiriwa. Sasa mashauriano nadhani kama jambo hili linafanyika vizuri au halifanyiki vizuri, nadhani mnapokuja kufuatilia sasa shughuli zetu za utekelezaji baada ya kupitisha bajeti hii, tushauriane kwenye Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, ili tuweze kuliongoza jambo hili vizuri. Lakini hatuwezi kuweka utaratibu ambao haupo kwa mujibu wa sheria. Ajira za Idara Maalum zinaajiriwa kwa mujibu wa Sheria hiyo ya Nam. 2 ambayo imewapa Mamlaka Tume ya Utumishi Idara Maalum kuajiri. Sasa nadhani utaratibu huo uko *very clear* na nadhani inabidi tuufuate.(*Makofi*).

Mafao ya Wastaafu wa Idara Maalum. Napenda kuliarifu Baraza hili Tukufu kwamba kweli tulikuwa na tatizo na tatizo hili lilikuwa linasababishwa na *formula* ambayo ilikuwepo kwa chini ya uongozi wa Rais wetu mpendewa Dkt. Ali Mohamed Shein. Wizara husika tumekaa au serikali tumekaa tumejua tatizo liko wapi na tatizo hili limesharekebishwa. Kifungu kile cha Kanuni ambacho Waziri wa Tawala za Mikoa na Waziri wa Fedha alikiweka kufuata *formula* ile, kifungu kile tumekirekebisha na tayari nimeshasaini *legal notice* ya kuweza kuwalipa mafao wastaafu wa Idara Maalum za SMZ. Kwa hivyo kulikuwa na utata kidogo *formula* gani ifuatwe, *formula* ya *ZSSF* au *formula* ipi. Kwa hivyo *formula* hiyo sasa imewekwa sawa na nadhani ni mambo tu ya fungu lile la mafao Waziri wa Fedha kama litakuwa limekaa sawa, sasa wakienda wastaafu wetu mafao yao watapata kwa mujibu wa utumishi wao na kwa mujibu wa stahiki zao zilivyo tofauti na lile tatizo ambalo lilikuwa limejitokeza.

Hili jambo tumelizungumza nje ya Mahakama tumemalizana na sitarajii kama litatokea tena na hasa kwa sababu kulikuwa na utata wa kifungu na hicho kifungu nimeshakirekebisha, nimeshakitangaza rasmi kwenye Gazeti Rasmi la Serikali.

Suala la fedha za msaada limezungumzwa pia kwa nini tunawapa hawa msaada wa shilingi 5,000 na kuna ile pencheni jamii. Haya ni mafungu mawili tofauti lakini nini lengo la serikali. Hizi fedha ziliwekwa na Muasisi wetu wa Mapinduzi, Jemedari wetu wa Mapinduzi Marehemu Mzee Abeid Amani Karume kuwasaidia wanyonge wale ambao walikuwa hawakupata nafasi ya kwenda kuishi kwenye nyumba za wazee. Nakiri kwamba jambo hili sasa limekuwa ni changamoto, tunachofanya hatutaki moja kwa moja kuzikatisha lakini sasa hivi tumekuwa makini zaidi katika yule mtu anayepewa ule msaada wa shilingi 5,000. Kwa hivyo serikali haikusudii kuongeza pesa hizi wala serikali haitaki kupanua wigo wa kuwaongeza hao watu wanaosaidiwa shilingi 5,000, anayefikia umri wa miaka 70 ataingia kwenye pencheni jamii na wakishamalizika wote maana yake pesa hizi zitakuwa hazitolewi. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe wasiwe na wasi wasi kuhusu pesa hizi. Sasa hivi tunazisimamia vizuri na *Inshaallah* wote hawa wakifikia umri wa miaka 70 basi watahama fedha hizi shilingi 5,000 watakuwa hawapati, maana yake wako ambao tayari sasa hivi hawapati kwa sababu wanapata zile shilingi 20,000.

Mhe. Spika, mesi ya JKU Wawi. Mhe. Hamad Abdalla Rashid kamanda yule pale ananisikia nimeshamuagiza kwamba akaifunge. (*Makofi*).

Mhe. Spika, bima ya afya. suala hili tumelisikia na serikali inalifanyia kazi kuhusu wapiganaji wa Idara Maalum. Kwa hivyo watupe muda ili twende tukalifanyie kazi kwa sababu kuna timu maalum ambayo imeundwa kwa ajili ya kufanya *study* ndogo kuhusu jambo hili. Kwa hivyo tunaomba watupe muda kidogo ili twende tukalifanyie kazi.

Mhe. Spika, vijana wa JKU kujitolea halafu wasipewe kazi. Kwanza nataka nitoe taarifa kwamba kujiunga na JKT, kujiunga na JKU si *qualification* pekee inayokufanya uajiriwe kwenye Idara Maalum au Vikosi vya Ulinzi na Usalama. Ile ni fursa ikitokezea ajira zipo utaajiriwa kama ajira hazipo lengo kuu ni kuwafundisha vijana uzalendo na kuwapa mafunzo ya amali ili waweze kujitegemea.

Mheshimiwa aliyesema sana kwamba kuna kijana au kuna vijana wamejitolea. Kwanza hayo masuala ya yeye kwenda kumueleza mambo hayo yanamfanya akose uadilifu wa kuajiriwa kwenye vikosi. Kwenye vikosi kuna maadili yake, sio kila kitu tu unaweza ukasema. Kwa hivyo mimi niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi tulielewe hili kwamba kujiunga kwa vijana JKU ni fursa sio kwamba lazima ukitoka uajiriwe, isipokuwa tunasisitiza kwamba wale wanaopitia JKT na JKU kwa sasa ndio watakaopata fursa ya kuajiriwa kwenye Vikosi vya Ulinzi na Usalama, lakini haina lazima kwamba ukienda uajiriwe, hilo halipo.

Mhe. Spika, kutembelea maeneo yote ambayo tumeombwa hapa. Napenda niwaahidi kwamba tutafanya kwa wale waliotuomba tutaweka kipaumbele lakini na wale waliokuwa hawakutuomba hasa kwa kuzingatia suala zima la ugatuzi, inabidi sasa tutembelee katika maeneo ya skuli zote

za msingi na maandalizi, vituo vya afya vyote pamoja na maeneo yote ya kilimo. Kwa hivyo tutafanya ziara katika kutembelea na kujua changamoto mbali mbali.

Mhe. Spika, magendo ya karafuu na magendo mengine. Mheshimiwa hili lilizungumzwa zaidi na Mhe. Ali Suleiman Ali. Tunakiri kwamba zile takwimu zilizowekwa pale hazikueleza magendo yote yaliyokamatwa na thamani yake, lakini magendo yote yapo na thamani yake ipo. Lakini suala la magendo ya karafuu kuonekana kwamba ni magunia kidogo yaliyokamatwa kwa sababu sisi kazi yetu ni kuzuia. Kwa hivyo kwa sababu ya udhibiti mkubwa ndio maana kiwango kikubwa hakikujitokeza katika kukiripoti kwa sababu walinzi wetu wameweza kudhibiti vizuri magendo ya karafuu katika msimu uliopita.

Mhe. Spika, majengo ya Mikoa na Wilaya. Tunakiri kwamba kuna tatizo kubwa sana na ufinyu wa majengo ya Mikoa na Wilaya, sio majengo ya Mikoa na Wilaya tu, hata jengo analotumia Waziri wakija pale watatuonea huruma. Lakini serikali hatua kwa hatua haya mambo inayafanyia kazi, *priority* nini? Kwa sasa miradi ambayo tuliyoonesha ni *priority* yale ambayo walikuwa wanatushauri hapa Barazani, mahanga ya askari, zana na nyenginezo. Sasa katika ujenzi Ofisi ya Mkoa wa Kusini na Mkoa wa Kaskazini linaonekana ni jengo jipya au la siku za karibuni, lakini bado kwa ugatuzi huu bado nakiri kabisa maelezo yenu Waheshimiwa Wajumbe tunakiri kwamba hii ni changamoto na sisi kama serikali tutaifanyia kazi.

Kuhusu magari ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya yako njiani, wala hatutawapa magari ambayo sisi tumeyaacha watapata gari zao mpya kama ni viongozi. (*Makofi*)

Lakini nataka nitoe ufafanuzi kuhusu majengo mawili ambayo yamezungumzwa la Wilaya ya Chake Chake. Jengo la Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake hakuhamishwa alihama kwa sababu jengo lilikuwa bovu, alipohama jengo likarudi serikalini, serikali ikawapa Idara ya Nyaraka, Idara ya Nyaraka wakalitengeneza kwa msingi huo hawezi kurudi Mkuu wa Wilaya. Kwa hivyo nataka nieleze kwamba hili zile taarifa nyengine haziko sahihi hakuhamishwa Mkuu wa Wilaya wala hajanyimwa, isipokuwa alihama kwa ubovu alishindwa kulitengeneza akatokea mwenye uwezo wa kulitengenza akalitengeneza. Kwa hivyo tuiache serikali iendelee na utaratibu iliyokwisha kuupanga wa kuwaachia Nyaraka na Mkuu wa Wilaya tutafanya maarifa mengine ya kumtafutia jengo jengine. (*Makofi*)

Kuhusu ujenzi wa jengo la Mkuu wa Mkoa pale Amani. Ni kweli uzio ule umezungushwa muda mwingi, lakini utaratibu unaitumika wa ujenzi wa pale ni utaratibu wa *BOT,* hakuna bajeti ya Serikali iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo lile. Kwa hivyo katika utaratibu huu kwamba anaejenga ni mwekezaji halafu mnaendesha kwa makubaliano, inabidi mikataba yenu muizangie vizuri sana ili msije mkakwazana mbele ya safari. Kwa hivyo napenda kutoa taarifa kwamba hatua iliyofikia Mhe. Mwanasheria Mkuu ameshaidhinisha huo mkataba na taratibu za mwekezaji ambaye atajenga majengo yale, moja litakuwa ni lile linalotizama kwa nyuma Uwanja wa Amaan lile litanunuliwa kama wazo alilolitoa Mhe. Hassan Khamis Hafidh mwaka uliopita, lile la nyuma sio lile la mbele kwa ajili ya usalama wa Uwanja wa Amaan na watumizi wa uwanja wa Amaan hasa wakati wa sherehe za mapinduzi.

Lakini eneo ambali limezungushwa mabati litajengwa *tower* mbili, moja ya usoni itakuwa ya kibiashara na ya nyuma huku itakuwa ni ya Mkuu wa Mkoa na atakuwa anatumia milango miwili tofauti, mlango wa barabarani utakuwa ndio wa biashara kwa ajili ya kurejesha fedha za mwekezaji na *tower* ya nyuma itakuwa ndio Afisi ya Mkuu wa Mkoa. Kwa hivyo tuvute subra kwamba ujenzi huu tunatarajia si muda mrefu utaanza kujengwa. Lakini kama nilivyosema katika shughuli hizi kwa sababu ndio tunaanza ilibidi tuwe makini sana katika kuzingatia mikataba, tusije tukapata matatizo baadae na nyinyi hapa kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunasikia sana ushauri wenu wa kwenda kuingia katika mikataba iliyokuwa siyo mibovu tunajitahidi sana tufanye hivyo.

Mhe. Spika, eneo jengine limezungumzwa suala kwamba *Local Government* hasa Manispaa ya Mjini inafanyakazi hakuna sheria. Mimi nataka niwaambie Waheshimiwa Wajumbe wakumbuke kwamba sisi tulipitisha Sheria Namba 7 ya Halmashauri na Sheria Namba 7 imefuta Sheria ya Manispaa, lakini *replacement* ya sheria hiyo iko kwenye Sheria hii Namba 7, imefuta Sheria ya Halmashauri na Mabaraza ya Miji, *replacement* ya sheria hiyo iliyofutwa ipo kwenye Sheria hii Namba 7, imefuta Sheria ya Serikali za Mitaa, *replacement* ipo kwenye sheria hii.

Katika kifungu cha 95 cha sheria hii kifungu kidogo cha sita kimeeleza vizuri sana na Kanuni ya huduma ambayo mimi nimeshaitangaza kwenye Gazeti Rasmi ni hii na sheria hii kwenye kifungu hichi namba 6 kifungu kidogo cha sita, kifungu cha 65, zile sheria ndogo ndogo hazikufutwa isipokuwa zinaweza zikafanyiwa marekebisho au kuandikwa upya ndivyo tafsiri ya kifungu cha sheria hii kinavyosema. Kwa hivyo nimuombe Mheshimiwa aliyezungumza hoja hii si kwamba tunafanyakazi kinyume na sheria au tunafanyaka kama hakuna sheria. Wanafanyakazi kutumia Kanuni hizi za jumla ambazo tunaziita Kanuni za huduma na tufanyakazi kupitia sheria hii.

Ahsante sana Mheshimiwa nisahau kuwataja Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Hidaya Ali Makame. Naomba radhi nimesahau kuwataja nao wamechangia kwa kusema hawakuchangia kwa maandishi. Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunikumbusha. (*Makofi*)

Kuhusu suala la usafi wa masoko, tunakiri kwamba masoko yetu kwanza ni ya kizamani hasa soko la Mji Mkongwe ni miundombinu ya zamani, wanaohudumiwa pale kwa maana ya wafanyabishara ni wengi na mfumo tunaokwenda nao wa uendeshaji wa lile soko pia unachangia katika kulifanya lile soko lisisafishwe vizuri zaidi. Mfumo wa masoko duniani kwamba soko linafanyakazi inafika muda lazima soko lifungwe lisitowe huduma ili watu waweze kulisafisha vizuri. Sasa mimi niombe Mheshimiwa uliotoa hoja hii ili lile soko liwe safi utukubalie kuanzia saa kumi soko tulifunge watu wasiwepo pale tulisafishe vizuri zaidi. Laa! kama si hivyo kwa mfumo ulio wa soko lile litaendelea kuwa chafu. Hata hivyo Baraza la Manispaa limekuwa likiendelea kulisafisha kwa kadri ya uwezo wake. Lakini tunakiri kwamba hali si nzuri naomba ukubali kwa kukubali huo uungwana wa kukiri. (*Makofi*)

Suala la baa; siyo Bhaa huyu wetu, ni kweli kumekuwepo na baa nyingi katika maeneo yetu na mimi katika hapa naomba nitoe wito kwa wananchi pale katika maeneo, maana ile Sheria ndivyo inavyosema, pale katika eneo ambalo wananchi hawakubaliani na jambo lile basi wapeleke rufaa ili Mahakama ya Vileo iweze kufanya maamuzi. Mimi nina hofu pia kutumia njia nyengine

ambazo mimi sizipendi sana. Kwa hivyo mimi nadhani tutumie sheria, ile sheria ni ya zamani na niishukuru sana Tume ya Urekebishaji wa Sheria imeshatuletea rasimu ya marekebisho ya sheria na sisi tunataka tulifanyie marekebisho ile sheria ili iendane na hali ya sasa na maoni ya wananchi wa sasa. Mhe. Spika, unajua zamani sheria ile ilivyotungwa wanywaji walikuwa wanakunywa kwa leseni maalum, wale wanywaji wale, ndani ya Unguja hii na Zanzibar hii kama huna leseni ilikuwa huendi baa hali imebadilika. Kwa hivyo tutarekebisha sheria kulingana na mazingira ya sasa lakini nakiri kwamba hayo yapo na tutayafanyia kazi, ili kuona wale ambao wanapata starehe hii tusiwaudhi, lakini na wale ambao hawapendi vile vile tusiwaudhi.

Suala la ujenzi wa maduka kiholela, *foundation* inajengwa usiku asubuhi imesimama. Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf nakushukuru sana kwa kulikumbusha hili. Nataka nitumie nafasi hii kuzungumzia pia suala la *kiosks* ambazo ziko Mlandege kwenye *road reserve.* Ni kweli niliitamka na matamshi yangu yanabakia pale, kwa sababu wale watu wamepewa vibali na Mipango Miji na watu wa Ardhi. Tunawaomba wafute vibali vile kwa sababu ile ni *road reserve.* Hofu yetu ni kwamba tukienda tu na *bulldoze* moja kwa moja tutashtakiwa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa hivyo sisi kama serikali tutashauriana aliyetoa kibali cha ardhi afute pahapa pasipostahiki ili sisi Manispaa tuende tukaondoshe vibanda vile hasa kwa sababu sheria za barabara zinahitaji mita maalum kuwe hakuna kitu mbele yake. Kwa hivyo tutalishughulikia hili hasa kwa sababu vibanda vile vipo katika eneo la *road reserve, reserve* ya barabara na pale nyumbani kwako Mheshimiwa samahani kwa kukutaja, nyumbani kwako pale sijui umetoa ridhaa mwenyewe au namna gani. Lakini hata mtu ambaye anatoka Malindi anataka kupinda huku hawezi kuona. Sasa hatuwezi kuendelea kubaki na mji wenye fujo namna hii. Kwa hivyo tutaambizana serikalini ili tuweze kulitafutia ufumbuzi suala hili (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunashukuru sana kwa pongezi ambazo tumepokea kwa ajili ya Mradi wa *ZUSP*. Waheshimiwa wahusika wengine wa majimbo ambao miradi hii imepita Chumbuni, Shaurimoyo, Mpendae, Jangombe, Kikwajuni kwa maana ya viwanja vya Mnazi Mmoja. Mradi huu umefanikiwa kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Lakini nataka nizuungumzie pia kadhia ya maji katika barabara ya Uwanja wa Ndege. Kwanza tuishukuru sana serikali kupitia Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Miundombinu. Nataka niseme tu tayari Wizara ya Ujenzi imeshasaini mkataba na kampuni ya ujenzi kwa ajili ya ujenzi wa kuondosha maji yale yaliopo katika barabara ya Uwanja wa Ndege na kupeleka pwani Mazizini. Hivi karibuni ujenzi utaanza. Mheshimiwa mwenyewe atakuja kujieleza vizuri sana wakati wa bajeti yake, fedha zipo, mkandarasi ameshapatikana tumeshatia saini kwa maana ya serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hivyo kadhia ile karibu itaondoka.(*Makofi*).

Suala la uchafu unaoendelea kuwepo wa tope na mambo mengine. Kama mnavyojua nitoe wito kwa Waheshimiwa kwamba tuwahamasishe watu wetu waache kutupa taka wakati wa mvua inanyesha, kwa sababu taka zile baadae zinakuja kuleta madhara katika maeneo kama yale na sisi kama Manispaa ya Magharibi "B", tutaendelea kusafisha kadri ya hali itakavyowezekana. Lakini ufumbuzi wa tatizo hili unaondoka.

Sambamba na hili niseme pia limezungumzwa suala la maji pale Mwanakwerekwe na maeneo mengine. Nalo hili litatatuka kwa *ZUSP II* ambayo ipo katika hatua za mwisho ya kuweza kumpata mkandarasi na kutangaza zabuni ili wakandarasi waweze kuingia *site* waweze kuondosha kadhia hii. Kwa hivyo Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango madhubuti sana wa kuondosha kadhia hizi na Waheshimiwa wamesema sio kwenye bajeti hii tu hata kwenye bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwamba hivi kila mwaka matukio haya yanajirejea rejea, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein inafanya utaratibu na mkakati madhubuti wa kuweza kuondokana na kadhia hizi.(*Makofi*).

Jambo jengine ambalo limezungumzwa kuhusu suala la utekelezaji wa Idara ya Ugatuzi. Kwenye buku kubwa lile la Bajeti Kuu lile lenye mafungu, linasema ilikuwa tufanye vikao kumi na tano, lakini kwenye kitabu chetu hichi cha mwaka jana katika mambo ambayo tulisema tutayatekeleza hamna kitu hicho cha mikutano, isipokuwa mikutano iliyofanyika ni ile la ugatuzi na imefanyika mikutano kumi na tisa. Mhe. Mohamed Said Mohamed lile suala ulilolisema kwamba tulipanga tufanye mikutano kumi na tano, limeandikwa mle kwenye buku inawezekana kimakosa, utekelezaji wa ugatuzi umo humu katika kitabu hiki mambo ambayo tuliyataja hayamo suala la mikutano kama ni *activity* peke yale. Lakini limo katika mambo ya jumla, lakini baada ya vikao vile vitano ni vya Bodi, pengine inawezekana kuna *error* tu kule. Lakini vikao vya ugatuzi vimefanyika kumi na tisa katika mwaka huu tunaoendelea nao na tunatarajia katika robo hii ya mwisho na vikao vyengine vitafanyika ili kutoa *message* na kuweza kuweka sawa mambo yale ambayo yatagatuliwa. Isipokuwa vile vikao vitano ni vikao vya Bodi nyengine, vikao vya Bodi ya Zabuni vya wizara ambavyo vimekaa kwa ajili ya kupitisha mambo mbali mbali.

Suala la mapapa wa dawa za kulevya, hawa orodha yake tunayo Mheshimiwa na tutakukabidhi ila nahisi kwa sababu kesi zao zipo Mahakamani si vizuri kuweza kuzitaja hapa. Lakini orodha tunazo tutakukabidhi na wala hatutathubutu kuwakamata wale vidagaa lakini orodha tunazo.

Wakala wa Ulinzi umeanza kazi kwa mujibu wa sheria, tulitakiwa tu tuseme au tulishauriwa kwamba Mhe. Omar Seif Abeid tuifanye kama SUMA JKT. Tutaelekea huko baadae lakini kwa sasa tunajikita kwenye ulinzi wa uwekezaji na utalii. Kwa sababu Sekta ya Utalii na Uwekezaji ndio ambayo sekta inaingiza fedha nyingi karibu asilimai 80 ya fedha za kigeni tunazipata kutoka kwenye sekta hii. Kwa hivyo kwa sasa itajikita kwenye ulinzi lakini huko usoni tutakakokwenda tutafikiria kulifikisha huko shirika hili. Lakini kwa sasa limejikita kwenye ulinzi.

Lakini pia liliulizwa tuna watu wangapi tumesema mahoteli ambayo tayari sasa hivi tunayalinda, Taasisi za Serikali ambazo tunazilinda kibiashara. Lakini tumeambiwa tutaje kiasi gani tunatoza. Kamati ina uwezo yoyote ile ya Baraza la Wawakilishi tukaja kuwapa taarifa....

Mhe. Spika: Mhe. Waziri una robo saa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante Mhe. Spika, tukawapa taarifa lakini kwa sababu suala la viwango na ada ni siri ya biashara naomba nisilitaje hapa. (*Makofi*)

Kuhusu uchelewaji wa vyeti tunakiri kwamba jambo hili lipo na hili lilikua linasababishwa na mambo chungu nzima likiwemo suala la kukosekana kwa *material* ile ya kutengenezea vyeti. Hata hivyo hivi sasa jambo hili limeshakaa sawa na jambo hili litarekebishika zaidi hasa kwa vile serikali ina nia ya kubadilisha mfumo, badala ya kwenda kwenye mfumo huu wa *manual* sasa tutakwenda kwenye mfumo wa kieletroniki na kama nilivyosema kwamba Wilaya zote sasa tunaziungansha kwenye mfumo ili mpaka kule Wilayani vyeti hivi vitoke kwenye njia ya kieletroniki, kwa hiyo jambo hilo tutalitatua kwa njia hiyo.

Kuhusu suala la mita moja Mhe. Masoud kwenye Gereza la kule Kinumoshi na Langoni napenda niseme kwamba ni kweli jambo hilo lilikuwepo na sasa watu wa Shirika la Umeme wameshakwenda kuweka kila nyumba mita yake kwenye Gereza la Kinumoshi lakini Langoni nako tunaendelea nako.

Kuhusu suala la Ndugukitu na makaazi ya watu au viwanja vya watu, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri nataka nimshukuru sana amesema vizuri, serikali imeamua vile viwanja ambavyo havijajengwa kupitia Wizara ya Ardhi viwanja vile vitafutwa na eneo lile libakie kama ni eneo la kambi, na wale wananchi watapewa maeneo mengine.

Mhe. Spika, mambo ni mengi lakini muda hautoshi nataka nizungumzie moja tu suala la *CCTV* limeeleweka, tulishauriwa tupunguze fungu tutoe bilioni 5 tupeleke kwenye barabara, barabara zina utaratibu wake na mipango madhubuti itapangwa, serikali itatafuta pesa ya kuzijenga lakini fedha hizi tulikwishasema mwaka jana kwamba mradi huu ni wa miaka mitano. Tusishangae Waheshimiwa Wajumbe kila mwaka tukaona bajeti yake ipo hapa lakini kwa faraja kubwa ninayoweza kuisema mambo yote yaliyokusidiwa kwenye mradi huu yameshawasili nchini, tulichoeleza hapa ni zile *CCTV* kwamba tunategemea mwishoni mwa mwezi ujao tuta-*lunge* rasmi.(*Makofi*)

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aliomba hilo na yeye atakuwa mwelezaji mzuri namshukuru sana, kwa sababu yeye ni Mwenyekiti wa Bajeti nimempeleka ameona. Kwa hivyo turidhike hapo kwamba pesa hizi hatuwezi kuzihamisha kwa sababu maalum. Mhe. Hamza Hassan Juma barabara ya Shaurimoyo itajengwa bila ya kuhamisha pesa hizi. Mhe. Omar Seif Abeid barabara za ndani kule Konde zitajengwa bila ya kuhamishwa pesa hizi, hizi tuziache kama zilivyo naomba Mhe. spika kuhusu jambo hili niishie hapo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda yako mambo mengine nitashindwa kabisa kuweza kuyatolea ufafanuzi, isipokuwa lipo jambo moja limezungumzwa sana hapa juu ya suala la uhalifu ambalo limejitokeza hasa katika Mkoa wa Mjini/Magharib. Serikali hatukukaa kimya na ule ushauri uliotolewa wa kuzidisha doria serikali tumeupokea na tunaufanyia kazi na tutaendelea kuufanyia kazi na ile kadhia iliyotokea *coconut,* kama nilivyosema kwenye kikao kimoja na leo nataka nirejee, Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi na wale watakaobainika hatua za kinidhamu na sheria zitachukuliwa na hili nasema niko *serious* .(*Makofi*)

Serikali haitaki kuona watu wake wananyanyaswa, kama kuna taratibu za kisheria zifuatwe na zitafuatwa na zinafuatwa ili wale wanaokiuka baadhi ya masharti wafikishwe kwenye vyombo vya kisheria kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe naomba jambo hili, bado mutuachie serikali kupitia Jeshi la Polisi tunafanya uchunguzi wa kina na tutakaowabaini tutawachukulia hatua. (*Makofi*)

Mhe. Spika, bado dakika ngapi.

Mhe. Spika: Bado dakika saba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Talawa za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, ilitoka kadhia kwamba kuna fungu la D12 *accounting officer* wake alisimwamisha na lile fungu ikawa linasimimiwa na Katibu Mkuu. Waheshimiwa munatusisitiza hapa kwamba hawa ma-*accounting officer* wawe waadilifu, serikali ilipoona kwamba kuna mambo hayendi vizuri ikamyang'anya huyu *accounting officer* aliyekuwepo na serikali inayo haki ya kufanya hivyo. Kwa hivyo serikali ilichukua taratibu zote maana huwezi kuwa *accounting officer* mpaka uidhinishwe na *pay master general.* Kwa hivyo *pay master general* alitoa idhini ya kumfanya Katibu Mkuu awe *accounting officer* wa muda na kumnyang'anya yule aliyekuwepo.

Na tulifanya hivyo kwa sababu tulikuwa kipindi cha mpito cha kuunda Taasisi ya Matukio ya Kijamii. Sheria tumeipitisha hapa Baraza la Wawakilishi Mhe. Rais ameisaini, Mhe. Rais ameteua watendaji tumepata *accounting officer* mpya Mkurugenzi Mtendaji na Manaibu wake wawili. Katibu Mkuu ameshahamisha kazi hiyo na *pay master general* ameshahamisha kazi hiyo amewarejeshea wenyewe. Hii inaweza ikafanya *accounting officer* yeyote ambaye ataonekana kwamba mambo hayapeleki vizuri, ni wajibu wetu serikali kusimamia hilo na kuweza kuchukua hatua ili athari kubwa zaidi isije ikatokezea.

Waheshimiwa napembua pembua yele niliyokuwa sijayasema, suala la kuvipatia zana vikosi vyetu nadhani limezungumzwa kwa kina hapa na serikali inajitahidi na imejipanga vizuri kuwapatia makaazi mazuri. Kwa sasa hivi tumeanzia Pemba, mwaka unaoishia 2017/2018 tumekwenda Pemba mwaka 2018/2019 tuko Pemba, tukitoka Pemba tunakuja Unguja kwa ajili ya kuwapatia makaazi mazuri.

Suala la kuwapatia zana Manispaa zote na *local government.* Ninapenda niliarifu Baraza lako tukufu kwamba tayari tumeshakaa kuona tunafanyaje katika robo ya mwisho ya mwaka huu kuweza kupata kijiko na *bulldozer* ijapo kwa ubia ili tuweze kuondosha kadhia hii ya taka na kufanyia mambo mengine. Lakini vile vile kwenye bajeti zao ambazo wamezipanga kupitia Madiwa wao, yapo mafungu ambayo kwa sababu tumeona hali ya ukusanyaji wa mapato sasa ni mzuri. Kama alivyosema Waziri wa Fedha vile vianzio vyote vya ambavyo ni vya *local government* vinabakia kuwa ni vya *local government,* hata ili *property tax* ambayo tunahisi ni moja kati ya kianzio kikubwa na kitakuwa na fedha nyingi, wameshasema *ZRB* wanachukua asilimia ile ambayo wanaisema Waziri wa Fedha, zilizobakia hizo zitakusanywa ili ziweze

kununua vifaa na zana mbali mbali ili *local government* ziweze kufanya kazi zake vizuri. Kwa hivyo ushauri wenu Waheshimiwa tunaupokea na tutaufanyia kazi.(*Makofi*).

Mambo mengine yale naomba maana yake ni mengi na ni marefu, kwa hivyo naomba kwa sababu ya muda Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo niliyoyatoa ni imani yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe mtanivumilia kwa wale ambao sikuwataja moja kwa moja na majibu ya moja kwa moja nimekwenda zaidi kwa majibu ya jumla. Lakini niseme moja tu kuhusu masoko na uguwaji wa vibaraza katika masoko. Kwa kweli tunazingatia katika masoko yote huo ndio muongozo wetu na Wakurugenzi wamefanya hivyo hivyo kwamba watarejeshwa wale wote waliokuwepo katika masoko yale zamani na zikibakia nafasi ndio watapewa wapangaji wapya. Hata hivyo watapewa kwa mujibu ya masharti ya mkataba ambayo itakuwa imetengenezwa. Kwa hivyo hakuna suala la kuwapa watu wengine, kuwaacha wale ambao walikuwepo wakifanya biashara pale. Kwa hivyo nalo niliseme niwatowe hofu Waheshimiwa Wajumbe kwamba hili tutalishughulikia.

Mhe. Spika, wale ambao walisema Waheshimiwa wanabakisha asilimia Fulani. Mhe. Hamza nakuomba asilimia zako uzirejeshe kwangu. Mhe. Dimwa samahani sio wewe ni Mhe. Abdala Diwani, ile asilimia yako ndogo uliyoikweka irejeshe. Mhe. Omar Seif Abeid irejeshe, Mhe. Miraji aliyekwambia hayo nani, huna haja ya kuzuia asilimia hamsini. Kwa hivyo asilimia hamisini irejeshe.(*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa heshima zote kabisa na unyenyekevu naomba Waheshimiwa Wajumbe waipitishe bajeti hii kwa sababu hii ni bejeti ya wananchi na nyinyi mmekuja hapa kupitia tiketi za wananchi.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.(*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais. Waheshimiwa ....(*Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika kuhusu utaratibu

Mhe. Spika: Mhe. Jaku naomba ukae kwanza.

Waheshimiwa Wajumbe kabla sijawahoji niseme kwamba Mhe. Waziri ametumia saa moja juu ya alama, lakini pamoja na hivyo kama alivyotangua kusema mwenyewe kwamba kuna mambo mengi sana hakuweza kwa sababu muda huu ulikuwa mdogo sana, angelihitaji muda mwingi zaidi kwa. Kivyo kabla sijawahoji Waheshimiwa tunaenda vifungu lakini nimekuwa napata vi-*note* kutoka huko kwenye *audience* yenu nyinyi waheshimiwa na wengi wenu mlikuwa munanihimiza suala la sala ya *Taraweh.* Sasa kwa maana hiyo tutelekea kwenye vifungu kwa hivyo nadhani mtajua nyinyi wenyewe namna ya ku *balance* hii hali kwa sababu ya wakati.(*Makofi*)

Baada ya hayo naomba sasa niwahoji Waheshimiwa wale wote waliokubaliwa na hoja Waziri wanyanyue mikono. Wananokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwa)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Naomba nimwite Mhe. Waziri aje atoe taarifa. Samahani Mheshimiwa kabla hujatoa taarifa, Mhe. Jaku ilihusu hili hili?

Mhe. Jaku Hashim Ayuob: Mhe. Spika kwanza nikushukuru na niendelee kumshukuru sana waziri Mhe. Haji Omar Kheri kama kuna Mawaziri wa kuiga mfano wake waige amechambua kwa hali na mali. Hoja yangu Mhe. Spika, nasikia mwezi umeandama na hii hoja uzoefu unavyoonesha Wizara hii inachukua muda mrefu. Ningeoma tukatumia Kanuni 147 tukaweka Kanuni kando Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho asubuhi tukaja tukapitisha vifungu kwa ulaini kabisa.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Mheshimiwa muda nadhani tunao tunawahi kwa sababu kisheria lazima tupitishe vifungu nitajaribu kupitisha kwa utaratibu ule ambao utaokoa wakati.

UTARATIBU

Mhe. Nadir Abdul-Latif Yussuf: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu. Mhe. Spika kwa kuwa wizara hii ni nzuri na imeangukia mwezi mtukufu wa Ramadani tumpitishie na kama tulivyowapitishia wengine.(*Makofi*)

Mhe.Spika: Mhe. Waziri

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalim za SMZ: Kwa kuwa Baraza limejadili, na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ sasa naomba baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya ofisi hii, naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU D01-OFISI YA RAIS TALAWA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Kifungu PD01 01 - Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa 5,102,

MUONGOZO

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Muongozo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Naam, Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimewaona maafisa wa serikali wakiwemo Makatibu Wakuu na watendaji wengi hawapo hapa ndani kumsaidia Mhe. Waziri. Kwa hivyo, tungeomba waruhusiwe.

Mhe. Mwenyekiti: Wanaruhusiwa kuja. Mnaruhusiwa watendaji kuja kumsaidia Mhe. Waziri hapa chini. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Naam Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Abdalla Maulid Diwani.

Kifungu PD 0102 -

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa jinsi alivyokuwa mtulivu kwenye ufafanuzi wake na kimsingi mambo mengi ameyajibu kiufasaha.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo, kwa sababu nilipokuwa nazungumzia ile kadhia ya Makamanda wetu wastaafu, namshukuru sana Mhe. Waziri amelizingatia na wamelifanyia kazi. Lakini hofu yangu ilikuwa ni moja, kwa sababu ile sheria ambayo walikuwa wamejaribu kukokotoa, amesema kwamba tayari wameshakaa na wameifanyia marekebisho.

Sasa hofu yangu ni moja, kwa sababu ile *formula* ambayo ilikuwa imetumika ya asilimia 85 ya mshahara, pamoja na asilimia 35 ya posho la nyumba kwa sababu tayari kuna wengine walikuwa wameshaanza ku-*enjoy* hii fursa. Sasa hofu yangu kama watakuwa wamefanya marekebisho katika vile vifungu, inawezekana wakaja wakapunjika. Kwa hivyo sitaki nilizuwie hili fungu lakini nilikuwa nataka kupata ufafanuzi, kwa sababu kama tayari walishaanza kulipa je, kama kuna marekebisho haitokuwa sasa kwamba kuondoa ile sheria ya mwanzo na tayari hawa watu walikwisha kutumikia. Sasa ili nijiridhishe na haya, kwa sababu inawezekana ikajakuwa kama imefanyiwa marekebisho, basi tayari kuna *arrears* ambazo wale wengine wa mwanzo ambao walikuwa wa-*enjoy* kulipwa. Sasa kwa sababu sijajua Mhe. Waziri wamekaa wamefanya marekebisho gani, labda angenisaidia tu ufafanuzi angalau niweze kujua kile ambacho ninakipitisha.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na nimshukuru Mhe. Hamza Hassan Juma. Tatizo lilikuwa ni *formula* ile inayozungumzia mshahara wa mwisho na tumeirekebisha hiyo, kwa sababu kwa Idara Maalum ukizungumzia mshahara wa mwisho sio ule ambao wanapata wafanyakazi wa kawaida. Kwa hivyo *formula* hiyo tumeirekebisha na sasa tutakuwa na *formula* moja lakini hofu ya Mhe. Mjumbe kwamba wale je, ambao wameshalipwa, watapata *arears* zao.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa hilo jawabu la Mhe. Waziri, kwa sababu nia ilikuwa sio kuzuwia, nia ilikuwa ni kupata ufafanuzi lakini vile vile kulinda haki na maslahi ya watumishi wetu ambao wanatutumikia usiku na mchana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sitaki kumsumbua tena Mhe. Waziri na lile fungu jengine kutokana na maelezo yake, kwa sababu wananchi wangu wa Jimbo la Shaurimoyo wamesikia ufafanuzi, lakini bado nitakuja katika Wizara ya Fedha na Mipango, ili kuangalia namna gani ile hoja ambayo Mhe. Waziri nilimshauri ya kuongeza tozo ya mafuta, ili kuongeza Mfuko wa Barabara kumsaidia zaidi. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuja kusaidia kuboresha barabara zetu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi ambao kila mmoja karidhika. Lakini panapo utamu kidogo lazima uchungu wa chumvi uongezeke.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu nilijaribu kusema kwamba nitalizuwia fungu hili la PD01, ilikuwa suala zima la ile kadhia ya wale vijana wetu ambao wametoka kule katika ajira ya mwanzo wamepelekwa katika ulinzi wa JKU. Lakini wale mpaka dakika hii wanapokea mshahara kutoka kule mwanzo ambako walisimamishwa au walipoachishwa. Sasa lakini wana mafao yao wanadai zaidi ya mwaka mmoja.

Je, hili Mhe. Waziri sikulisikia ufafanuzi wake, anijibu hili halafu tutaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa mishahara ya watumishi, unaweza ukahamishwa leo Baraza la Wawakilishi ukapelekwa Wizara ya Fedha na Mipango. Kwa kuwa bajeti ya mshahara ilikuwa Baraza la Wawakilishi basi utaendelea kulipwa Baraza la Wawakilishi. Huo ndio utaratibu wa kiserikali.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuhusu fedha zao. Kasema vizuri Mhe. Naibu Waziri, unaposimamishwa unaweka *block*, ukisimamishwa ukifukuzwa ni lazima *immediately* uwende ukawekewe *block* mshahara, ili kuepuka ile mishahara hewa. Kwa hivyo unapowekewa *block* mshahara maana yake mpaka uombe upya, unaanzia utumishi ili wajiridhishe, iende kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wajiridhishe, iende Wizara ya Fedha na Mipango halafu ndipo mshahara ule urejeshwe katika *payroll* ya taasisi inayohusika. Kwa hivyo, huendi tu kesho unarejeshwa, kesho ukapewa ule mshahara ambao uliwekewa *block*, kuna taratibu lazima zifuatwe, ahsante sana.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimekufahamu, nafikiri kaeleza vizuri na wale wapiga kura wetu wametufahamu na wametusikia naomba tuendelee.

Kifungu PD 0102	-	Programu Kuu ya Uratibu na Usimamizi wa Idara Maalum	5,940,000,000
Kifungu PD 0104	-	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum.	**23,624,000,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 01	**34,666,600,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu D 0201	-	Utawala Unguja	**79,469,000**
		Jumla ya Kifungu D 02	**79,469,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI

Kifungu PD 0201	-	Programu Kuu kwa Mafunzo kwa Vijana na Uzalishaji Mali	2,614,170,000
Kifungu PD 0202	-	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa JKU	**20,060,330,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 02	**22,674,500,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 03 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu D 0301	-	Sheria na Urekebishaji	**70,991,000**
		Jumla Kuu	**70,991,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 03 - CHUO CHA MAFUNZO

Kifungu PD 0301	-	Programu Kuu ya Urekebishaji wa Wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo	68,813,000
Kifungu PD 0302	-	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji	**15,190,888,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 03	**16,059,700,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kidogo. Huku kuna *confusion* kuna D 04, D03 hatuelewi maana yake vitabu vina matatizo au vipi. Maana yake huku unatueleza vyengine na huku kuna vingine. Huku kuna kuna 6 na huku kuna 3.

Mhe. Mwenyekiti: Vimekosewa kidogo Mhe. Mjumbe. Vinaonekana vimekosewa kwa sababu mimi kitabu nilichonacho naona kina marekebisho, kwa hivyo nilitegemea hata hivyo mlivyonavyo nyinyi huko viwe vimesharekebishwa.

Waheshimiwa Wajumbe nafikiri page ya chini inayotajwa, iko sawa. Angalia chini kabisa. Naomba tuendelee ili tuokowe wakati.

FUNGU D 04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUWIA MAGENDO

Kifungu D 0401	-	Utawala Unguja	**33,505,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 04	**33,505,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUWIA MAGENDO

Kifungu PD 0401	-	Programu Kuu ya Ulinzi na Uzuiaji wa Magendo	2,144,000,000
Kifungu PD 0402	-	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo	**26,408,100,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 04	**28,552,100,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu D 0501	-	Utawala Unguja	**74,184,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 05	**74,184,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU D 05 - KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Kifungu PD 0501	-	Programu Kuu ya Uokozi na Uzimaji Moto	600,000,000
Kifungu PD 0502	-	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa KZU	**8,140,800,000**
		Jumla Kuu ya Fungu D 05	**8,740,800,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na
Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nitarudi nitalirejesha Baraza ili tuweze kutengua kanuni ya muda, halafu tutarudi kuendelea kumalizia.

(Baraza lilirudia)

KUWEKA KANDO KANUNI ZA BARAZA

Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba tutumie Kanuni yetu maarufu ya 23(1) hii tuiweke kando kwa sababu tuweze kumaliza shughuli ziliopo mbele yetu. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja tuweke kando Kanuni ya 23(1) ili itupe nafasi ya kumalizia shughuli zilizo mbele yetu. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na Mhe. Waziri. Naomba sasa niwahoji wale wote wanaokubali hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU D 06 – KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu D0601 Utawala Unguja

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mhe.Mwenyekiti, ahsante sana kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake mzuri alioutoa wakati wa kutoa michangio.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nimesema kwamba Vikosi vyetu hivi vina kazi kubwa sana ambayo wanaifanya, kwa kweli wamepangiwa vikusanye na tumeona hapa kwa mwaka 2017/2018 vimekusanya shilingi milioni 45,530,000 lakini vile vile vimekusanya shilingi 600,259,000 na vile vile kwa mwaka huu kimepangiwa Kikosi hichi cha Valantia kukusanya shilingi 80,932,000.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo nalo fungu hili lakini nilisema kwamba niliomba wizara makusanyo haya yakishakusanywa, basi kubakia asilimia fulani irudie kwao ili kwa kujenga matatizo ambayo wanayo, kwa sababu kikosi hichi tumekwenda pale Ndugukitu majengo yao ni mabovu lakini hata wao wana kazi kubwa ambazo wanazizofanya. Kwa hivyo Mhe. Waziri sikumsikia hata kunijibu lolote. Naomba majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru pia Mhe. Ali Khamis Bakar kwa maelezo yake lakini suala la ujenzi wa Ndugukitu, serikali imetoa shilingi milioni 500 kwa mwaka huu wa bajeti tunaokwenda nao na hizi fedha ambazo zimewekwa hapa kwenye mapato, Waheshimiwa wengi tumepokea *concerning* yao lakini hizi tutambue kwamba tayari ndio hizi ambazo zimegawiwa katika kuzikusanya kwake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo serikali tumepokea *concerning* hii tuwachiwe tutakwenda kuzungumza huko serikalini, lakini hili fungu la mapato libakie kwasababu hizi pia ni sehemu ya haya mapato ambayo tutagawiwa katika idara zetu, lakini *concering* ni nzuri na serikali inatambua hili lakini kwa mwaka huu kwa kipindi hichi tuache kwanza ili tukakae serikalini tuweze kulizungumza vizuri zaidi. Lakini kuyaondosha hapa itakuwa ni tatizo kabisa hasa kwa mimi Waziri wa sekta. Kwa hivyo tuliache tukalizungumze na hasa kwa sababu haya ndio mapato ambayo yamepangwa kwa matumizi ya mwaka huu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe Mwenyekiti, kwa vile Waziri wangu amekiri na hili suala na yeye vile vile analitambua mimi nilitaka kumkusha tu ili ajue hii kadhia amekubali basi sawa na tuendelee.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kuzuia fungu isipokuwa nilikuwa nataka ufafanuzi kifungu hichi. Imeelezwa kwamba KVZ msingi wa mapato yao yanayokusanywa serikalini ni kwa ulinzi katika Taasisi zao. Sasa shughuli hii tumeambiwa inakwena kwenye wakala. Je, hawa KVZ watakuwa na kazi nyengine yoyote itakayokuwa inawapatia mapato. Nikipata jibu hili itakuwa sawa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kwa sababu KVZ wameondolewa kianzio kile cha ulinzi nakiri hilo kwa sababu shughuli hii imekabidhiwa rasmi Wakala wa Ulinzi. Lakini kama nilivyosema kwamba serikali sidhani kama itachukua hatua ya kuwafunga wasipopeleka hizi fedha, kwa sababu hicho kianzio hakipo. Kwa hivyo naona mimi tukubaliane tu tumwachie Waziri wa Fedha na serikali kwa jumla ili tukalitafakari, ninachosema mimi kuliondosha hapa kukubali liondoke maana mimi sio mwenye fungu hili la mapato. Mimi ni mkusanyaji sasa yule ambaye anasimamia hili ndio anaweza akatoa msamaha baada ya kuona uhalisia wa mambo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo bado nasema tuiachie serikali kupitia Wizara ya Fedha ili hili jambo twende tukalitafakari kwa kina lakini *concerning* ya Wajumbe ninaipokea na ninaikubali kabisa kwamba kianzio hichi sasa kimehamishiwa Uwakala wa Ulinzi na uhamishaji wa mafungu unatokezea kama vile alivyosema Waziri Fedha. Kwa mfano suala la *OC* ambazo hazijaja kutoka Wizara ya Kilimo kuna utaratibu wa kufanya *vehement. K*wa hivyo mapato haya yanaweza yakatolewa fungu hili yakapelekwa fungu jengine, lakini hilo tumwachie Waziri wa Fedha kwa mujibu wa sheria. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa kwa hili watuachie Mhe. Waziri wa Fedha anayo maelezo anaweza akayatoa kuhusu jambo hili, lakini natambua na huo ndio ukweli ulivyo kwamba KVZ sasa hawana chanzo cha mapato kitokanacho na ulinzi, nakubaliana na hilo.

Mhe. Spika: Mhe. Machano. Msikilize Waziri wa Fedha kidogo.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Waziri hapa kwamba hapa tujue kwamba haya ni makisio, na makisio huenda tukapata hivyo hivo au l*esser* au tukapata zaidi. Kwa hivyo hakuna dhara ya kuwepo hapa. Tutakapo kuja ku-*review* mwakani itaonekana ile hali halisi yenyewe ya makusanyo katika kifungu hichi. Lakini kwa sababu hiyo Taasisi mpya ndio kwanza inaundwa bado yapo mapato ambayo yanaweza yakakusanywa, ikitokea hivyo tutakuja kuyajua hapo mwakani lakini hakuna dhara ya kuwepo hapa kwa sababu haya ni makisio, sio halisi. Mwakani tutaiona hali halisi itakavyokuwa na hichi kifungu kitaondoshwa na kuwekwa kule kwenye Taasisi. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina tatizo na mpango wa serikali, kwa vile mimi nilikuwa naomba tu wanapoandaa bajeti wa zile taasisi zinakutana na kukubaliana mwanzo kwa sababu kama unajua nyumba hii haikaliwi na mtu ukasema mna watu 10 inakuwa tatizo, lakini kwa mwaka huu wacha twende lakini kama wangelikuwa mwanzo wangekutana Wizara ya Fedha na hawa watu wakaelezana uzuri nafikiri tatizo hili lisingeweza kutokea. Kwa hivyo, hivyo hivyo wacha twende.

FUNGU D 06 – KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu D 0601	Utawala Unguja	60,259,000/=
	Jumla Kuu ya Fungu D 06	**60,259,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D 06 – KIKOSI CHA VALANTIA

Kifungu PD0601	-	Program Kuu ya Ulinzi wa Nchi, Raia na Mali zao	896,000,000/=
Kifungu PD0602	-	Program Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Kikosi cha Valantia	**11,269,600,000/=**
		Jumla Kuu ya Fungu D 06	**12,165,600,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D O7 – MKOA MJINI MAGHARIBI

Kifungu PD0701	Mkoa wa Mjini Magharibi	**80,585,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na kamati ya matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU D O7 – MKOA MJINI MAGHARIBI

Kifungu PD 0701 Kusimamia shughuli za Serikali za Katika Mkoa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi ndio akili vile vile kama nitakosea untaniongoza maana yake nisije nikaikosea yote.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa adabu wa mwisho kama kumshukuru Mhe. Waziri kwa mara ya pili Mhe. Haji Omar Kheir kwa jinsi alivyofafanua hoja baada hoja haki yake apewe wa moja ni moja wa mbili ni mbili.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hoja zangu zitakuwa ni mbili ya masoko na *parking*.

Mhe. Mwenyekiti, chombo hichi na alitumia neno kubwa sana Mhe. Haji Omar Kheir na nili-*note* na siku hizi nitalitumia maisha. Serikali haitaki kuona wananchi wake wananyanyaswa tarehe 16/5/2018 saa 1:07 alizungumza na mwezi mtukufu wa Ramadhan tunaanza, jambo kubwa sana Mhe. Haji kalizungumza na Mungu atakulipa kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, tumepitisha Sheria ya *Parking* Namba 7 na Mwanasheria Mkuu tusaidie mimi elimu yangu ndogo ndio maana ukaona mpaka hivi sasa nikawa sijapata Naibu Waziri wala Uwaziri.

Mhe. Mwenyekiti: Nenda kwenye hoja tu Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, *Road Transport Act* ya 2003 mwenye mamlaka ya *parking* ni Waziri wa Miundombinu. Sheria nnayo hii hapa na nitaisoma Mwanasheri Mkuu tusaidie, elimu yangu ndiye ile ile ndogo kizungu kidogo nitakizungumza namba 157. "*The minister may be an order in the gazzette*. Maana yake nini.*(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kama panakushindeni nisaidieni kidogo. Ni Waziri anayeshughulikia masuala ya usafiri ndie mwenye dhamana ya kutangaza *parking.* Si maneno yangu Sheria imepitishwa mwaka 2003 na haijafutwa na Sheria haiwezi kupandiana juu ya Sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nnakuja kuna kifungu (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, kifungu *(a) Set aside part of the road as parking place for search classes of the motorvehicle and search period as may be certify is such order.*

Mhe. Mwenyekiti, nini maana yake. Anaweza kutenga sehemu ya barabara kuwa ni maegesho kwa aina fulani kwa vyombo tena kwa muda ambao utautaja katika hilo tangazo tena la serikali.

Mhe. Mwenyekiti, *(b) Provide suitable places as parking places or stand for stage and town buses, tax, cab and good vehicles.*

Mhe. Mwenyekiti, nini maana yake. Anaweza akatoa eneo la maegesho la stendi za daladala gari na abiri. Mwenye mamlaka ya haya ya barabara, haya maneno nimehangaika kuyatafuta ni Wizara ya Miundombinu. Leo kila uchochoro, kila sehemu mahala hamustahiki mpaka Mhe. Ali Hassan Mwinyi aliekewa *parking* mbele yake pale nikapiga kelele ikaondoshwa.

Mhe. Mwenyekiti, leo barabara ya Mlandege yote, Darajani yote, Mahakamani, wauza madagaa Malindi. Sheria haiji kwa sheria twende kwa sheria tushindane kwa ubabae wala nini, twende kwa sheria baada ya sheria hata Mahakamani tunakwenda sheria baada ya sheria, kama tujenge hoja baada ya hoja, tusipandishe sheria baada ya sheria. Mamlaka haya Mhe. Waziri huna, nipo tayari kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo Mhe. Waziri kila vichochoro na sheria yao walioileta.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja yako moja kwa moja ili tupunguze wakati.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, alizungumza hoja ya wananchi wasinyanyaswe wanaendelea kunyanyaswa na sheria bado hawana sheria haijafutwa, na mwenye mamlaka Mhe Waziri Dkt. Sira Ubwa Mamboya. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mwenyekiti, kwa hiyo hapa na hiyo sheria haijafutwa na inatakiwa iwe kwenye gazeti rasmi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante subiri uisikie serikali na yenyewe itazungumza. Mhe. Waziri ikisha sauti yako kidogo watu wa hansard huko wanasema hawaipati.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka nimshukuru sana Mhe. Jaku Hashim Ayoub na amesoma kifungu cha sheria ile inayompa mamlaka Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kutenga maeneo ya *parking*.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nikubaliane naye kwamba Waziri wa Ujenzi kwa mujibu wa Sheria ndiye anayetenga maeneo ya *parking* na maeneo ya *bus stands* na *parking*. Lakini akishakuyatenga muendeshaji na msimamizi ni *Municipal* si yeye. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na Sheria ili Namba 7 ya mwaka 2014 imeeleza vizuri sana. Sasa mimi nataka nikubaliane nae Mhe. Jaku. Sasa mamlaka ni ya Waziri yule ndio anayesema hapa jenga, *bus stand*, hapa weka *parking*, lakini anayendesha ni *Municipal*, na ndio maana mwaka jana ilipokuja hota ya *bus stands.* Niliwaambia suala hili anayeweza *ku-allocate* eneo la *bus stand* ni Waziri wa Ujenzi, akesha ku-*allocate* sisi tu-*operate,* tunaandesha. Kwa hivyo Mhe. Mwakilishi alewe hivyo na Waheshimiwa waelewe hivyo. Lakini Sheria yetu Namba 7 inatambua kwa kufuata ile Sheria ya Ujenzi na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo alivyosema sipingani naye lakini muendesaji ni Manispaa na muendeshaji Manispaa anapotaka kuendesha ana Kanuni na taratibu lazima nayeye aziweke katika kuweka hivyo viwango. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki kupoteza muda, kila mmoja anasimamia hoja yake ilivyo. Niendelee kumheshimu sana Mhe. Waziri, lakini Sheria haijafutwa hawezwi kupandisha sheria juu ya sheria. Mamlaka nyengine zinazotaka kufanya maegesho lazima zishauriane na Waziri wa Usafirishaji ambaye atatangaza kwenye Gazeti la Serikali liko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja kila chochoro sasa hivi *parking* na hajaweka eneo maalum kwa hii *parking*, duniani kote huwezi kukuta *main road* ikafanywa *parking.*

Mhe. Mwenyekiti: Yaani hoja yako. Mheshimiwa samahani kidogo. Mhe. Waziri hakatai kwamba Mhe. Waziri wa Miundombinu hana Sheria hiyo, hiyo Sheria anaitambua Sheria ya 2003 nadhani na bahati mbaya sana au bahati nzuri, mimi nilikuwa Waziri wakati ule nikaipitisha hiyo sheria.

Hiyo sheria naikubali ipo isipokuwa anasema yeye kazi yake ni kuendesha ku-*oparate* kwa maana ya Manispaa. Hiyo ni wizara yake yeye. Kwa hiyo anaweka Kanuni kuhusiana na hilo sasa sijui hoja yako iko wapi, lazima kuwe na tangazo kwenye la Serikali au vipi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa hata hiyo Kanuni mimi ninayo, hazikuweka maeneo kwa hivyo watasokotwa tu wananchi sasa kinyume na hiyo kauli yake hayo maeneo hayakuwekwa, kila kona Mahakamani kuna huduma kunapakiwa, ukienda soko la Malindi kunapakiwa, kila kona wana maeneo maalum siyo kila uchochoro tuweke *parking* tu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, maana naona sasa anapinga maelezo yake yeye mwenyewe mimi si kazi yangu kutangaza maeneo, kama alivyosema yeye ni kazi ya Waziri wa Ujenzi mimi kazi yangu kutengeneza kanuni zitakazosimamia hizo huduma. Kanuni ndogo ndogo ndio nilivyofanya mimi kuweka viwango vya huduma za hizo *parking.* Sasa mimi nadhani tunazungumza lugha moja na mimi nisingefanya kama Waziri wa Ujenzi hajafanya hiyo kutanganza kwenye *legal notes* ya Serikali. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa hayo maneno sitaki kumtaja mtu hayo maneno yametokea huko huko wenyewe hawakuridhika na utaratibu huu, huu wa *parking* wenyewe barabara na usafiri ndio waliopiga kelele hawajaridhika na hoja hii maana yake sheria haijafutwa wanapandishia sheria juu. Mimi kanuni yake ninayo hapa Mhe. Haji hii hapa nina kanuni ya huku na huku.

Mhe. Mwenyekiti: Subiri akusaidie Mheshimiwa Machano kidogo, Mheshimiwa Machano.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Kanuni kifungu 93 lakini nakwenda kifungu 98(4) (iii) tunapofikia hatua hii ya kamati ya matumizi Mjumbe hatakiwi kuanzisha tena majadiliano aseme hoja yake kwa ufupi na Waziri ajibu kwa ufupi halafu Wajumbe waamue, hakuna kuzunguka zunguka katika matumizi.

M**he.Mwenyekiti:** *Actual* tumesha-*exhaust* mara tatu**,** kwa hivyo twende kwenye kura.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mheshimiwa twende kwenye kura ukweli utabaki ukweli hata nikizungumza lakini wananchi watakuwa wameshafahamu tupige kura Mheshimiwa niko radhi mimi.

M**he.Mwenyekiti:** Unataka kura siyo?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wananachi wanahukumu nje huko.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe naomba kuhoji wale wote wanaokubaliana kwamba serikali tuendelee na suala hili wanyanyue mikono yao, wanaokataa, waliokubali wameshinda. Tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa hoja ya pili iko pale pale nilisema nina hoja mbili ya masoko. Mheshimiwa kwanza niendelee tena kumshukuru sijui mara ya nne au ya tano kakiri masoko machafu na akazidi kusema la Darajani lakini nimwambie la Mombasa kama hujavaa *rain boot* hivi saa huwezi kuingia, Mwanakwerekwe sikwambii, Pemba sikwambii. Hii hali pesa zinapatikana zinakwenda wapi? haileweki huku Mheshimiwa wanasema Serikali hii haitaki kuona wananchi wake wanyanyasike pesa zinakusanywa zinakwenda wapi? Huku Mhe. Waziri anasema Serikali hii haitaki kuona wananchi wake wanyanyasike, pesa zinakusanywa zinakwenda wapi.

M**he.Mwenyekiti:** Mheshimiwa imetosha hiyo, imetosha. Mhe. Waziri,

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalu za SMZ: Fedha zinakwenda kwenye Mfuko wa Manispaa na zinatoa huduma za kuzoa taka ndani Mji huu wa Zanzibar. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mheshimiwa hata Rais leo kahimiza suala la usafi, hawa wanatakiwa wawe kioo Manispaa, kinyume chake sivyo leo katika vyombo vya habari alitutakia tufunge mwezi mtukufu wa Ramadhani,

M**he.Mwenyekiti:** Mheshimiwa hiyo hoja nyingine sasa unaleta kwa sababu hoja yako ilikuwa inauliza fedha zinakwenda wapi, Mheshimiwa Waziri kalijibu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hizo fedha hazitumikii masoko, yale masoko hazitumikii pesa na masoko yote yamejaa maduka kwa hivyo mapato yanazidi lakini usafi unazidi kuwa hauridhishi sasa hizo pesa zinatumika kwa njia gani nyingine?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti lazima tukubaliane, kama tunataka tuwatetee Wananchi tukubaliane na misingi ya utetezi. Serikali inatoa huduma kutokana na makusanyo, wananchi hao hao Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub huja akawatetea hapa tuwapunguzie viwango wanatozwa pesa nyingi, sasa hizo pesa zitapatikana, pesa wanakusanya Manispaa lakini kwa huduma

zinazotakiwa kutolewa hazitoshelezi. Kwa hivyo tukubaliane kwamba kama nilivyomwambia mimi nimekiri, mimi nilikuwa muungwana sana kwake. Nimekiri kwamba jambo hili lipo na tunakubali kwamba ni changamoto tutalifanyia kazi. Sasa anapokuja tena kuleta hoja nyengine ambayo mimi nimemjibu mimi nadhani siyo sahihi. Na lengo lake sijui ninini Mheshimiwa Jaku. Sasa mimi nadhani, maana yake mimi leo nimekuwa rahimu sana, nimekuwa *very diplomatic* nimetumia *diplomatic language* leo hapa. Wajumbe wote wanaonifahamu wameona. Sasa Mhe. Jaku anachotaka nini.

M**he.Mwenyekiti:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub tunaendelea au tunaendelea Waheshimiwa,

Kifungu PD 0701	- Program kuu ya kusimamia shughuli za Serikali katika Mkoa	327,773,000/=
Kifungu PD 0702	- Program kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa Wilaya na Shehia.....	

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante namuona Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti na mimi namshukuru sana Mhe. Waziri kwa maelezo yake ya ufasaha kabisa. Naomba sana Mheshimiwa atutolee ufafanuzi pale aliposema kwamba Mkuu wa Mkoa kukusanya pesa zote za Mkoa halafu kuwapa kwa udoho udoho Wakuu wa Wilaya. Kwa nini kusiwe na *sub vote* katika Wilaya wakawa wanatiliwa na Wizara ya Fedha moja kwa moja wakawa wanaendesha kazi zao hasa katika suala zima la ugatuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. na mimi nataka nimshukuru sana Dkt. Mwinyihaji Makame kwa wazo hili kweli amelitoa na sikupata muda wa kuweza kulitolea ufafanuzi.

Sasa hivi *Accounting Officer* wa Mikoa na Wilaya kwa fedha zinazotoka serikalini ni Katibu Tawala wa Mkoa na hili jambo serikali tumelizungumza tayari na tunatambua, lakini kama unavyojua bajeti hii au mpango huu wa bajeti unakuwa *review* kila baada ya miaka mitatu. Mhe. Mwinyihaji Makame tunashukuru kwa kutukumbusha na *inshallah* mwakani tutakapokuja mambo hayo tutayazingatia. Ahsante.

M**he.Mwenyekiti:**Mhe. Dkt Mwinyihaji, Mheshimiwa ameridhika, anafata Mhe. Omar Seif Abeid,

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi nafasi. Mhe. Mwenyekiti mimi wakati wa kuchangia niligusia kadhia nzima ya mifugo katika maeneo ,ya mjini hasa Wilaya ya Magharib "B" kwamba ng'ombe katika maeneo kuanzia Mbuyumnene wapo wanafungwa na mwaka jana tulianza operesheni hii kwa kasi. Sasa mimi sina nia yoyote isipokuwa nilitaka tupate ufafanuzi na maelezo ya kina juu ya kadhia ya wanyama ambao wanaendelea kufungwa katika maeneo ya mjini. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mheshimiwa na mimi nataka nimshukuru pia Mhe. Omar Seif Abeid kwamba jambo hili amelizungumza na Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerey) kwa kule Pemba na tumeshakubaliana kwa sababu hili zoezi lilifanyika lakini wananchi wetu wanapenda kujaribu jaribu. Sasa mimi nadhani tumeshakubaliana operesheni hii tutaianza tena. Tutaianza tena kwa wale wananchi sugu ambao hawataki kutuelewa, lakini niwaombe Waheshimiwa Wajumbe hawa ng'ombe tukishawakamata Waheshimiwa Wawakilishi msinifate. Mheshimiwa ahsante sana nakushukuru.

M**he. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mheshimiwa tunaendelea.

Kifungu - PD0702	Program kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa Wilaya na Shehia	2,226,527,000/=
Kifungu - PD0703	Program kuu ya kusimamia utekelezaji wa Maendeleo ya Jamii	30,841,700,000/=
Jumla Kuu		**33,396,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yotote)

FUNGU D08 - MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu - D0801	Mipango na Sera	35,733,000/=
Jumla Kuu		**35,733,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yotote)

FUNGU D0812 - MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA POGRAMU NDOGO NA HUDUMA MKOA WA KUSINI UNGUJA

Kifungu PD0801	Programu Kuu ya Kuratibu Utekelezaji wa Shughuli za Serikali katika Mkoa	243,470,000/=
Kifungu PD0802	Programu Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa wa Kusini Unguja	1,389,830,000/=
Kifungu PD0803	Programu Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	110,245,000/=
Jumla Kuu		**12,878.300,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yotote)

FUNGU D09 - MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Kifungu D0902	Wilaya ya Kaskazini "A"	11,424,000/=

Kifungu D0903 Wilaya ya Kaskazini "B" .....

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kwa haraka leo nilichangia mambo mawili, moja likawa linaigusa Wilaya ya Kaskazini "B" na mimi sina dhamira ya kuzuia fungu lakini dhamira yangu mimi na Mhe. Waziri na wananchi wa Skuli ya Upenja wana Kamati kwa sababu tumefanyiwa kitendo ambacho sikufurahia, ni kitendo ambacho kinadhalilisha jamii na watendaji wetu. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilisema wananchi wa Upenja walikuwa na mwalimu pale anajitolea kwa muda wa miaka miwili, wakatoka na mimi nilifatana nao katika sura ile ya kwenda kuwaombea Wizara ya Elimu wakarudi wakaambiwa waandike barua waende Wilayani, tukaandika barua ikenda Wilayani baada ya muda kama wiki sasa tukapokea mfanyakazi mpya tukarudi tena Wilayani

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa, samahani kwa sababu utakuwa unalielezea upya lakini ulilielezea vizuri wakati ule ulipokuwa ukichangia na Mhe. Waziri nadhani atakuwa amelielewa nadhani tumruhusu nadhani hakupata muda wa kutosha alijibu sasa hivi kama utakuwa umeridhika tena tunaweza kuendelea.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Naomba nimalizie na ile *comment* nnayotaka kumwambia tu, nnachotaka kumuomba Mhe. Waziri kwa sababu wananchi hawa baada ya kurudi juzi tu wanasema nyinyi watu wa Upenja mnatushughulisha, kwa ile kauli mimi ndio sikuipenda. Sasa nataka wale niwachukue wale watu wa Upenja wanaowashugulisha wale watendaji niwachukue akae nao ile kazi aifuatilie sasa kama itaonekane wao ndio wanatushughulisha sisi watuombe radhi ikesha limekwisha.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mheshimiwa kwanza na mimi nataka nikushukuru wewe kwanza kwa kuanza kusema kwamba sikupata muda wa kuweza kutoa ufafanuzi hili kutokana na muda lakini nimshukuru Mhe. Miraji Khamis Mussa pia, Lakini jambo lenyewe linakwenda kwenye masuala ya uajiri kama hivi. Nadhani akubali nilichukue kwa sababu suala la uajiri wa walimu kwenye bajeti tunayokwenda nayo watumishi ndo wanahamishiwa kwetu, lakini wacha tulichukue tukalifnayie kazi mimi na yeye tujue ukweli wa mambo ukoje halafu tuone tunaweza tukafanya namna gani.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana na naomba Mhe. Waziri uwe na busara hizo hizo mpaka kufa kwako inshallah.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Kifungu D0903	Wilaya ya Kaskazini "B"	8,424,000/=
Kifungu D0904	Wilaya ya Tumbatu	1,000,000/=
Jumla Kuu		**20,848,000/=**

Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yotote)

Kifungu PD0901	Program kuu ya kuimarisha shughuli za Serikali katika Mkoa	234,547,000/=
Kifungu PD0902	Program Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Mkoa, Wilaya na Shehia	1,513,553,000/=
Kifungu PD0903	Program ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	12,610,700,000/=
Jumla Kuu		**14,358,800,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapa juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yotote)

MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu D 1006	Mkoa wa Kusini Pemba	12,663,000
Jumla Kuu ya Fungu		**12,663,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

D.1010 MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA PROGRAM NDOGO NA HUDUMA MKOA WA KUSINI PEMBA

Kifungu PD1001	Program Kuu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa	176,076,000
Kifungu PD1003	Program Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa, Wilaya na Shehia	1,264,824,000
Kifungu PD1004	Program Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	10,597,600,000

	Jumla Kuu ya Fungu	**12,038,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

D 11 MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu D1101	Mipango na Sera	15,793,000
	Jumla ya Fungu	**11,379,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

D1110 MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA PROGRAM NDOGO NA HUDUMA KWA MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Kifungu PD1101	Program Kuu ya Kusimamia Shughuli za Serikali katika Mkoa	229,457,000
Kifungu PD1103	Program Kuu ya Uendeshaji na Utawala wa Mkoa Wilaya na Shehia	1,535,843,000
Kifungu PD1104	Program Kuu ya Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa	9,614,200,000
	Jumla Kuu ya Fungu	**11,379,500,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

D17 MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO KIKASMA

AFISI YA USAJILI WA VIZAZI NA VIFO NA KADI ZA UTAMBULISHO

Kifungu D1202	Utawala Unguja	128,405,000
Kifungu D1203	Afisi ya Mrajis Vizazi na Vifo	235,899,000
	Jumla Kuu Fungu	**464,304,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

D1210 MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA PROGRAM NDOGO NA HUDUMA

Kifungu PD1201	Program kuu ya kusajili Vizazi, Vifo na Kadi za Utambulisho	1,502,060,000
Kifungu PD1202	Program Kuu ya Utumishi na Uendeshaji wa Afisi ya Usajili wa Vizazi, Vifo na Kadi za Uambulisho	2,309,940,000
	Jumla kuu ya Fungu	**3,315,200,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na

Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha za Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe naomba sasa hoja iamuliwe wale wote ambao wanakubaliana na hoja ya Mheshimiwa ya kupitisha wanyanyue mikono juu, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe naomba nichukue nafasi hii kwanza kukupongezeni nyote lakini zaidi pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa namna ambavyo ameweza kuihitimisha hii hoja yake, nawashukuruni sana kwa sababu muda tuliotumia ni zaidi ya dakika arubaini na tano, zaidi ya ule muda ambao upo wa kikanuni wa kumaliza Baraza na taarifa tuliyonayo ni kwamba watu wameanza kuswali Tarawehe leo kwa maana ya kwamba tumeingia kwenye mwezi mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo nichukue nafasi hii kuwatakieni Ramadhan Kareem sana

Mwenyezi Mungu azikubali Swaumu zetu na wale wote ambao watakuwa wamejiingiza zaidi kwenye ibada katika kipindi hichi ambacho ni kipindi cha kuchuma sana, basi Mwenyezi Mungu awalipe kwa kadri ambavyo wanafanya ibada zao. *(Makofi).*

Waheshimiwa Wajumbe baada ya kusema machache hayo naomba niakhirishe shughuli za Baraza la Wawakilishi mpaka kesho Saa 3.00 Asubuhi.

(Saa 2.26 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 17/05/2018 saa 3.00 asubuhi)